Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 15 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 416

**Makubaliano Kati ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. JOYCE J. MUKYA** aliuliza:-

Makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kifungu 3(a) yaliyosainiwa Mkoani Arusha tarehe 14 Machi, 1996 yanatambua hadhi ya Wafanyakazi wa Kitanzania katika ngazi za *Executives* na *Professional Staff* ya kupata haki zao za msingi ikiwemo ile ya kumiliki pasi za kusafiria za kidiplomasia *(Diplomatic Passports),* lakini baadhi ya wengi wao wakiwa *Professional Staff* wamekuwa wakikataliwa haki hiyo licha ya kufuatilia kwa muda wa miaka minne tangu mwaka 2007;

(a) Je, Serikali inawaeleza nini Watanzania hao wanaokataliwa haki yao ambao huwasababishia usumbufu wakati wa kuomba *VISA* na kwenye viwanja vya ndege?

(b) Je, Serikali haioni kuwa Jumuiya kuwanyima pasi hizo kunawadhalilisha Watanzania hao wanaofanya kazi huko na pia kutengeneza matabaka miongoni mwa nchi Wanachama?

(c) Je, ni lini Serikali itaondoa kero hiyo kwa raia wake hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mkataba wa Uenyeji *(Headquarters Agreement)* uliotiwa saini mwaka 1996 Mjini Arusha umetamka katika kifungu cha 3(a) kuwa Watanzania watakaofanya kazi katika ngazi za Watendaji Wakuu na Wataalamu *(Executives na Professional Staff)* watastahili kupata pamoja na haki nyingine, Pasi ya Kidiplomasia kwa mujibu wa Kifungu 15(b) cha Sheria Na. 5 ya mwaka 1986 ya haki na Kinga za Wanadiplomasia nchini Tanzania. Kifungu 15(b) kinaelekeza haki hizo kutolewa kwa kufuata orodha maalum *(Part III of the Fourth Schedule)* iliyopo sehemu ya tatu ya jedwali la nne katika Sheria hiyo.

Hata hivyo, wakati wa utekelezaji, kulijitokeza tatizo kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki haikuwemo kwenye orodha ya Mashirika ya Kimataifa yaliyoainishwa katika Sheria na ambayo Watanzania wanaofanya kazi katika mashirika hayo kupata haki hizo za Kidiplomasia. Hali hii ilisababishwa na ukweli kuwa, Sheria Na. 5 ya mwaka 1986, ilipitishwa kabla ya kuundwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kusainiwa kwa Mkataba wa Uenyeji kati ya Serikali yetu na Jumuiya hiyo. Hivyo, Jumuiya hiyo kutokuwepo kwenye orodha iliyoainishwa katika Sheria hiyo ya mwaka 1986.

(b) Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki haitoi pasi za kusafiria kwa wafanyakazi wake wa ngazi yoyote. Pasi za kusafiria za wafanyakazi wa Jumuiya hiyo hutolewa na nchi wanazotoka kuendana na matakwa ya kisheria ya nchi hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, kilio cha Watanzania wanaofanya kazi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki katika ngazi za Watendaji Wakuu na Watalaamu *(Executive na Professional)* kimetufikia na tumekifanyia kazi ikiwemo kupokea ushauri wa kitaalamu na kisheria. Wakati wowote kuanzia sasa, Wizara kwa kuzingatia masharti ya Sheria Na. 5 ya mwaka 1986, itaingiza Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye orodha ya Asasi zinazofaidika na kinga na upendeleo wa kidiplomasia ili Watanzani hao waweze kupata haki hiyo.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Kuna baadhi ya Watanzania ambao wanamiliki *pass* hizo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wao wamezipataje wakati wengine hawana *pass* hizo?

Pili, katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa si hakika kupata *pass* hizo. Naomba nisaidiwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, Sheria yetu ya uhamiaji tayari inatoa watu ambao wanastahili kupata *pass* za kidiplomasia, mfano ni wafanyakazi katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, yaani *Foreign Service Officers,* lakini pia, mfano wa Bunge na Maafisa wengine wa ngazi za juu. Mfano ni kama Naibu Katibu Mkuu wa *East Africa* - Ndugu Bukuku ambaye amekwenda akiwa tayari anastahili kupata Viza hiyo ya kidiplomasia.

Bila shaka atakuwepo katika *EAC* na atakuwa tayari anayo Viza ya kidiplomasia na inawezekana pia wengine ambao wameingia katika *EAC* wakiwa tayari wanazo *pass* hizo za Kidiplomasia wataendelea kuwa na *pass* hizo. Tatizo linakuja kwa wale ambao wameingia wakiwa bado hawastahili na wanategemea mkataba ambao umeingiwa baina yetu sisi na Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndiyo hilo ambalo tunalifanyia kazi. Ahsante.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninapenda kujua ni watu gani hasa katika Taifa hili la Tanzania wanaostahili kuwa na hati ya kusafiria ya kidiplomasia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, watu ambao wanastahili kupata *pass* ya kidiplomasia ni wengi na wameorodheshwa katika Sheria, lakini nimetaja mfano, kwanza ni viongozi wote wa nchi, Wabunge, Makatibu Wakuu, Maafisa wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwa maana ya *Foreign Service Officers,* na wengine ambao wametambuliwa na Sheria.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa viongozi wana hati za kidiplomasia na mara nyingi husafiri nchi za nje wakiwa na wake zao au waume zao: Je, wake za viongozi na waume za viongozi wanaruhusiwa kuwa na hati hizo za kidiplomasia wakiwemo Wabunge?

**SPIKA:** Wabunge na wake zao au Wabunge na waume zao? Mheshimiwa Naibu Waziri toa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, jibu rahisi ni ndiyo. Kwa viongozi ambao wanastahili kupata *pass* za kidiplomasia na wenzi wao pia wanastahili kupata *pass* hizo.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa mtaanza kwenda ku-*apply*, mlisahau.

Sasa ni Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 417

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi Chilonwa**

**MHE. HEZEKIA N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Kampuni za simu za Tigo na Zain zilikwishaitikia maombi ya kupeleka huduma ya simu za mkononi kwa wananchi wa vijiji vya Kata za Mambe, Dabalo na Zajilwa kwenye Jimbo la Chilonwa kwa kwenda kufanya utafiti wa kuweka minara ya simu kwenye maeneo hayo:-

(a) Je, ni lini kampuni hizo zitapeleka minara hiyo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma ya simu za mkononi?

(b) Kwa kuwa baadhi ya vikwazo vikubwa vya kupeleka huduma hizo kwenye maeneo mengi ni pamoja na miundombinu mibovu ya barabara na idadi ya watu, lakini kwa sasa maeneo mengi ya Tarafa ya Itisho na chilonwa zina idadi kubwa ya watu wenye uwezo wa kugharamiwa na simu za mkononi: Je, Serikali sasa sinaweza kuharakisha kufikisha huduma hiyo kwa wananchi wa vijiji vyote vya Tarafa za Itiso na Chilonwa?

**SPIKA:** Swali la kwanza limejibiwa vizuri dakika tano na nyongeza watu wawili ni jambo zuri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua umuhimu wa huduma za Mawasiliano katika maeneo ya Kata za Mambe, Dabalo na Zajilwa pamoja na maeneo mengine nchini. Aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itafuatilia matokeao ya utafiti wa Kampuni za Simu za *Tigo* na *Airtel* ili kufahamu

mipango ya utekelazaji kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uwepo wa vikwazo vikubwa vya kupeleka huduma ya mawasiliano kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge pamoja na uhaba wa nishati ya umeme, Serikali itaendelea kushirikiana na makampuni ya siku ili kuweza kufikisha huduma hiyo hata kwenye maeneo yenye upungufu huo. Hii ni pamoja na kutumia jenereta za dizeli, nishati ya jua na pia kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ambapo mfuko huu katika awamu ya kwanza tayari umeainisha jumla ya vijiji 11 vyenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,793 katika Mkoa wa Dodoma.

**MHE. HEZEKIA N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Ili kuwaondolea shauku kubwa kwa muda mrefu kusubiri kupatiwa minara ya simu katika maeneo ambayo tayari yalishafanyiwa utafiti kama haya ya Kata za Dabalo Mambe na Zajilwa, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa ipo haja ya kuwafikishia ratiba wananchi waliofanyiwa utafiti maeneo yao ili waweze kujua watapatiwa lini minara ya simu?

Pili, kama nilivyokuwa nimeeleza katika sehemu (b) ya swali langu la msingi kwamba maeneo mengi ya Tarafa za Itiso na Chilonwa sasa hivi yanafikika kwa urahisi kwa barabara na mengine tayari yana huduma ya umeme: Je, Serikali itakuwa tayari kuhimiza makampuni ya simu za mkononi kwenda kufanya *promotion* katika maeneo haya kwa ajili ya kuwapa elimu na kuhamasisha upatikanaji wa simu za mkononi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema na kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi katika maeneo aliyoyataja kulikuwa na utafiti uliofanyika, lakini utafiti unapofanyika unaangalia uwezo wa watu kulipa simu, wingi wa watu na sehemu za kuweka mtandao kama zinaweza kuwa na huduma ambazo alisema kwamba hazipatikani.

Kwa sasa hivi nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Kampuni ya *Airtel* ina mpango wa kufanya utafiti upya mwezi Septemba katika maeneo aliyoyataja na nitayaomba hayo Makampuni yaweze kufanya hiyo *promotion* wakati wamekwenda kufanya utafiti wa mara ya pili.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Kwa kuwa tatizo la Chilonwa ni sawa na lililopo Ngara ambapo Kata nyingi hazina mawasiliano ya simu na hata Kata za Nyakisasa, Keza, Musagamba, Muganza, Mbuba, Nobeye, Kilusha, Mabawe na Mugoma, wananchi wa Ngara wangependa kujua ni lini Kata hizo zitaweza kupatiwa mawasiliano ya simu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ntukamazima tumeshazungumza naye kuhusiana na maeneo hayo na baadhi ya maeneo yako kwenye Awamu ya Kwanza ya mpango wa *UCAF* kufanyiwa utafiti ili yaweze kuwekewa mtandao. Vilevile maeneo mengine aliyoyataja, nimeshayachukua, nitawasiliana na Wataalamu ili tuone namna ambavyo tunaweza kuyafikishia vilevile mawasiliano katika kipindi hiki cha miaka miwili kama ambavyo siku zote nimekuwa nikisema tuna *program* ya miaka miwili.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa, wananchi wengi wamekuwa wakitoa maeneo yao na kujenga minara hii ya simu na Makampuni haya yamekuwa yakiwasumbua wananchi wakati wa kuwalipa mafao yao: Je, Serikali itawahakikishiaje wananchi hawa waliotoa maeneo yao na ikajengwa minara ya simu wapate pesa zao kwa wakati muafaka?

**SPIKA:** Kama kawaida yako, swali jipya! Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, makubaliano kati ya Kampuni ya Mawasiliano na mwenye ardhi ni mkataba wa watu wawili na wanapoingia wote wanasaini mbele ya watu ambao wanashuhuidia. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Watanzania kwamba wawe makini sana wanapoingia mikataba na makampuni hayo ili kuhakikisha kwamba pale ambapo malipo yanachelewa, basi kuwe na *close* ya *penalty* kama mtu atachelewa kulipa aweze kulipa na riba kidogo.

Na. 418

**Mashamba ya *NAFCO* Mbarali na *NAFCO* Kapunga**

**MHE. MODESTUS D. KILUFI** aliuliza:-

Mashamba ya *NAFCO* Mbarali na *NAFCO* Kapunga yamepewa wawekezaji: Je, Serikali itawasaidiaje wakulima wadogo wadogo wanaozunguka mashamba hayo ambao awali waliishi ndani ya mashamba hayo na kuwasaidia na wale wa nje?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shamba la Mpunga la Mbarali lililokuwa la *NAFCO* lilibinafsishwa kwa Kampuni ya *Highland Estate Ltd,* tarehe 18 Agosti, 2006. Shamba la Mpunga la Kapunga lilibinafsishwa kwa kampuni ya *Export Trading Company Ltd*, tarehe 13 Septemba, 2006. Tangu kubinafsishwa kwa mashamba hayo, kumekuwa na migongano kati ya wawekezaji na wakulima wadogo ambao kabla mashamba hayajabinafsishwa walikuwa wanalima kwa kujikimu maeneo ambayo *NAFCO* haikuweza kuyalima. Migongano inayojitokeza mara kwa mara katika matumizi ya maji ya kumwagilia mashamba na maeneo ya kulima (Mashamba) ni kwa sababu ya matatizo ya uhusiano.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka mashamba yaliyobinafsishwa wana mchango mkubwa katika kusaidiana na mwekezaji kuhakikisha kwamba mashamba yote yanalimwa na kuzalisha chakula kama ilivyopangwa. Aidha, wananchi hao pia wanayo nafasi ya kupata ajira au hata kuzalisha mpunga kwa mkataba maalum.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wananchi wanamiliki mashamba yao nje ya mashamba yaliyobinafsishwa, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo yanayozunguka mashamba yaliyobinafsishwa. Kwa mfano, katika mwaka 2011/2012, Serikali imetenga Shilingi milioni 500 ili kujenga banio la umwagiliaji katika Kijiji cha Mwendamtitu huko Mbarali. Aidha, tarehe 4 Agosti, 2011, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alifanya ziara katika mashamba ya Kapunga na Mbarali na kumwagiza Mhandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ya Mbeya kukagua maeneo yaliyopendekezwa na wananchi kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji huko Kapunga ili Serikali itafute fedha za kuyaendeleza. Mhandisi anaendelea kufanya uchunguzi wa kitaalamu.

Namwomba Mheshimiwa Kilufi na wananchi wa Mbarali na Kapunga kuwa na subira wakati Serikali inaandaa miradi ya kuwasaidia wakulima.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa vile wananchi wa Kapunga ambao sasa hivi ni Kata mbili, Chimala na Kitamboleo walikuwa wanategemea sana eneo hilo na sasa tayari liko chini ya mwekezaji, na eneo ambalo wanaliomba liendelezwe ni eneo la Mpunga Mmoja ambalo lina hekta zaidi ya 4,000 pamoja na eneo la Mwashikamile na Iyala:-

(i) Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuona kwamba wananchi hawa wanaondokana na adha hiyo, na hivyo maeneo yanaboreshwa ili yaweze kulimwa na wananchi hao?

(ii) Naomba nifanye masahihisho, Mwendamtitu siyo kijiji, ni *intake* ambayo inategemewa kujengwa. Kwa vile shamba la *NAFCO* Mbarali lilipokuwa linabinafsishwa, Serikali iliahidi kwamba itawajengea *intake* ambayo ndiyo inaitwa Mwendamtitu ambayo itasaidia Kata za Rujewa, Ubaruku, Usongwe, Malilo na Mapogolo kwa Vijiji vya Msesule na Itamba. Sasa hivi toka Serikali imetoa ahadi hiyo, bado utekelezaji wake haujaonekana na hivyo kusababisha mgogoro mkubwa kati ya wawekezaji na wananchi, na sasa hivi bajeti iliyotengwa ni Shilingi milioni 500 ambayo nina uhakika haiwezi kujenga *intake* ile. Je, Serikali ina jitahada gani nyingine za ziada kuona fedha hizo zinaongezeka na hiyo *intake* inajengwa ili wale wananchi wasiendelee kupata shida na kuwa na mgogoro na mwezekaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu ya msingi, tayari Serikali imetenga Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuboresha maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aende kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ukurasa wa 120, jedwali Na. 5 ataona hizo Shilingi milioni 500 ziko pale. Lakini pamoja na hayo, Serikali inahakikisha kwamba, inayaboresha hayo maeneo hatua kwa hatua kulingana na fedha zinavyopatikana.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kuna mashamba ya *NAFCO* ambayo yalikuwa mashamba ya mifugo, na sasa hakuna mifugo na Serikali inataka kuyabinafsisha: Je, isingekuwa busara kwa Serikali kutenga maeneo ya kuwapa wafugaji wanaozunguka maeneo hayo ili nao wafugie mifugo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inapobinafsisha inakuwa na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba wananchi wanaozunguka maeneo yalipo mashamba na wao wanafikiriwa katika kuhakikisha kwamba wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Kwa hiyo, maeneo hayo yatakavyobinafsishwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hilo alilolisema litaangaliwa na kuhakikisha kwamba wananchi hawapati bugudha kama ambavyo amependekeza.

Na. 419

**Makato ya Zao la Korosho**

**MHE. CLARA D. MWATUKA** aliuliza:-

Ni kawaida kwa mnunuzi yeyote wa mazao ya nafaka kutafuta soko na kusafirisha mazao hayo: Je, ni kwanini muuzaji wa zao la korosho hulazimishwa kugharamia vifaa kama magunia, usafi wa ghala, usafirishaji pamoja na makato mbalimbali bila maridhiano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao lolote linapopelekwa sokoni huwa na gharama zake ambazo haziwezi kukwepeka. Baadhi ya gharama hizo ni pamoja vibebeo, utunzaji ghalani, usafirishaji, usimamizi na uendeshaji. Katika kuuza korosho pia kuna gharama na makato mengine ya kisheria sawa na mazao mengine yanayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa korosho huuza korosho zao kupitia mawakala wao ambao ni Vyama vya Ushirika au Vyama vya Wakulima. Mawakala hao hukusanya korosho na kuzipeleka sokoni kwa maridhiano yao. Wakulima hulipwa malipo ya bei dira *(indicative price)* na pia hulipwa malipo yatokanayo na bei ya soko au mnadani baada ya kutolewa gharama zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuiagiza Bodi ya Korosho, wanunuzi wa korosho na wakulima kuhakikisha kwamba mjengeko wa bei *(price structure)* katika biashara ya korosho unajadiliwa kwa uwazi katika vikao vya wadau wa korosho ili kuondoa manung'uniko. Aidha, tarehe 20 Agosti, 2011, kikao cha wadau wa korosho kitafanyika hapa Dodoma ambapo pamoja na mambo mengine, masuala yanayohusu gharama zinazohusiana na mfumo wa stakabadhi ghalani yanaweza pia kupewa ufafanuzi. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wadau wa korosho kuhudhuria kikao hicho muhimu.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, ni kawaida kila mara Serikali inaweza kusema mazuri wakati ule wanapotaka suala lifanyike, lakini baada ya hapo, matokeo yake yanakuwa ni kinyume na makubaliano yale yaliyotolewa.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutuhakikishia kwamba yale yanayosemwa ndiyo yatakayotekelezwa au yanatekelezwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko makini na inachosema ndicho inachotekeleza. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge tarehe 20 Agosti, 2011 ahudhurie kikao hiki cha wadau na aweze kutoa madukuduku yake na yatajadiliwa na kukubaliwa na watu wote katika kikao hicho.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sababu moja ya wakulima wetu katika kipindi chote cha miaka 50 ya kuendelea kuwa maskini ni kwa sababu bado hatujawa na viwanda vya kutosha vya kuweza kuongeza thamani ya mazao tunayozalisha. Kwa mfano, bado tunasafirisha asilimia tano tu ya pamba ambayo imekuwa *processed*, Korosho kwa asilimia 30 tu, karafuu kwa asilimia 15 tu na kadhalika.

Je, Serikali ina utaratibu na mpango gani wa kuhakikisha angalau hili zao moja la korosho ambalo tayari lina viwanda ambavyo kama vikisaidiwa tunaweza tukasafirisha zaidi ya asilimia 70 ya korosho iliyosafishwa ili wakulima wetu waondokane na umasikini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anatambua na aliona hivi karibuni Serikali imeleta mpango wake wa miaka mitano hapa Bungeni, na katika mambo muhimu yaliyowekewa kipaumbele ni kuhakikisha kwamba tunaendeleza viwanda na kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda ambavyo vitaongeza thamani ya mazao yetu ili tuweze kupata bei nzuri zaidi katika Soko la Dunia. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea na mpango wake huu wa miaka mitano na itatoa kipaumbele katika maeneo ambayo vilevile Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Sambamba na zao la korosho, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Ni lini sasa Serikali itaacha kuweka zuio kwa wakulima wa Mikoa ya Shinyanga hususan Wilaya ya Meatu la kuwazuia kuchanganya pamba pamoja na mahindi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nasikitika sana sio swali lenyewe. Nasikitika sana! Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Mahusiano na Uratibu) unataka kujibu, lakini swali siyo lenyewe kabisa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba swali lililoulizwa ni tofauti na swali la msingi, lakini kwa manufaa ya wakulima wa pamba katika Mkoa wa Shinyanga ambao wamekuwa wakichanganya pamba na mahindi, ningependa kusema kwamba kiutaalam na kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, mazao ya mahindi kwa

kawaida huzalisha wadudu wanaoshambulia pamba na hivyo kufanya gharama ya kulima pamba na mapato yanayopatikana kwa wakulima wa pamba kuwa chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ni marufuku kwa kweli kuchanganya pamba na mahindi, na kwamba viongozi wa kisiasa wanaowaambia wakulima wa kule wachanganye, hawawasaidii sana katika kuzingatia misingi ya kilimo bora. Kwa hiyo, ni vizuri walime pamba mbali na mahindi mbali.

**SPIKA:** Inatosha! Kweli nimekumbuka kwamba huyu alikuwa Waziri wa Kilimo. Nashukuru sana.

Na. 420

**Kuendeleza Ufugaji Nyuki**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Ufugaji Nyuki Kahama na Bukombe ni shughuli ya kiuchumi yenye tija kwa watu wengi kwenye maeneo hayo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza na kuboresha ufugaji nyuki ili uwe wa kisasa zaidi?

(b) Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo ili wawe na mizinga mingi zaidi na viwanda vidogo vidogo vya kusafisha asali na kuifungasha kwenye chupa/makopo maalum ili kuiuza nje ya nchi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inayo mipango ya kuendeleza shughuli za ufugaji nyuki, ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi ya kuendeleza ufugaji nyuki katika Wilaya 30, ambapo Wilaya za Kahama na Bukombe ni kati ya Wilaya hizo. Lengo la kuanzisha miradi hiyo ni kuhakikisha kuwa shughuli za ufugaji nyuki zinakuwa za kisasa zaidi ili kukuza uzalishaji wa mazao ya nyuki.

Katika kuendeleza Miradi hiyo, Wizara imekuwa ikitenga fedha kiasi cha Shilingi milioni 150 kila mwaka kuanzia mwaka 2007/2008 hadi hivi sasa. Fedha hizo hutumika kutoa elimu ya ufugaji nyuki na kuwawezesha wafugaji nyuki kuanzisha vikundi vidogo vidogo vya ufugaji nyuki sambamba na kuwapatia mizinga ya kisasa na mavazi ya kinga. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imekuwa ikitoa mafunzo ya ubora, usalama na mfumo wa ufuatiliaji asali kama kigezo cha kupata soko la ndani na nje.

Pia, Serikali kupitia Wizara yangu, imekuwa ikiandaa maonyesho ya asali kila mwaka kwa lengo la kuwakutanisha wafugaji nyuki, wataalam wa nyuki na watengenezaji wa vifaa bora vya ufugaji wa nyuki. Katika maonyesho ya asali ya mwaka 2009 yaliyofanyika Dar es Salaam, jumla ya wafugaji nyuki watano kutoka Wilaya za Bukombe na Kahama walishiriki.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha wananchi wa maeneo ya Bukombe, Kahama na maeneo mengine nchini, Serikali imewezesha vikundi mbalimbali vya wananchi wa kuvipatia mizinga ya mfano ili waweze kutengeneza mizinga yao wenyewe kwa kuwatumia mafundi seremala walioko kwenye vijiji vyao.

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Serikali ilitoa mavazi ya kinga 15 yenye thamani ya Sh. 975,000/= pamoja na mizinga 48 yenye thamani ya Sh. 1,440,000/= kwa vikundi vitano vya wafugaji nyuki Wilayani Kahama. Vikundi vilivyonufaika ni vya ufugaji nyuki Matumaini (kijiji cha

Nyamigege); Maarifa (kijiji cha Ngongwa); Songambele Mpunze (kijiji cha Mpunze); Ufugaji wa nyuki Mbika (kijiji cha Mbika) na Muungano *Beekeeping* (kijiji cha Kangeme).

Aidha, kwa mwaka wa 2010/2011 kiasi cha Sh. 9,200,000/= zimepelekwa Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora kwa ajili ya kutengeneza mizinga 143 na kuisafirisha kwenda Kahama. Kwa upande wa Bukombe, mwaka 2009/2010, vikundi vitano vilinufaika kwa kupatiwa mavazi ya kinga na mizinga kwa idadi ya thamani sawa na ile iliyotolewa kwa wenzao wa Kahama. Vikundi vilivyonufaika ni Huruma Nyuki *SACCOS* (Kijiji cha Nyamakungwa); Ikwamule Nyuki *SACCOS* (kijiji cha Mbogwe); Nyakasaluma *Beekeepers Group* (kijiji cha Nyakasaluma); Matunda Nyuki *SACCOS* (kijiji cha Ngemo) na Ufugaji nyuki Kagera (kijiji cha Kagera).

Sambamba na kuviwezesha vikundi hivyo, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo kwa mafundi seremala na mafundi cherehani, na wahunzi watawezeshwa mafunzo ya utengenezaji vifaa hivyo ili vipatikane kwa urahisi vijijini. Aidha, Shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* wameandaa mfumo wa 'Kopa Mzinga lipa Asali'. Elimu ya mfumo huu itasambazwa kwa wafugaji nyuki wengi zaidi ikiwemo Kahama na Bukombe.

(c) Mheshimiwa Spika, sambamba na juhudi hizo, Serikali inaendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa mazao ya nyuki kupeleka vifungashio hadi kwenye ngazi ya vijiji kupitia Vyama vya Ushirika na Serikali za vijiji. Mpango huu utarahisisha upatikanaji wa vifungashio vya asali. Kwa sasa, Serikali inaandaa utaratibu wa kuhamasisha wadau wa ufugaji nyuki katika maeneo ya ufugaji nyuki kuanzisha *SACCOS* na vikundi vya wafugaji nyuki ili waweze kukopa na kusaidiwa vifaa.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Waziri kwa majibu ya maswali yangu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Nadhani Waziri anatambua kwamba shughuli ya ufugaji wa nyuki ina tija kiuchumi, na ni shughuli ambayo haihitaji ufuatiliaji sana kama ilivyo kwa shughuli nyingine kama kilimo cha pamba na shughuli nyinginezo, na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli hapa Bungeni kuhusu jambo hilo.

**SPIKA:** Naomba swali sasa!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Swali langu ni kwamba: Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kuandaa mpango mkakati kwa ajili ya ufugaji wa nyuki kitaifa ili hatimaye Tanzania iwe mzalishaji wa mazao ya nyuki namba moja duniani?

Pili, mfumo wa 'Kopa Mzinga lipa Asali' ambao umeandaliwa na *SIDO* na ambao umetajwa katika jibu la msingi utaanza kutekelezwa lini Bukombe na Kahama?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza au kuimarisha sekta ya nyuki nchini, Serikali imeandaa mpango wa ufugaji nyuki wa miaka mitano kuanzia mwaka 2010 - 2015 na sehemu ya utekelezaji wa mpango huo itaanza kuonekana kwenye mawasilisho yetu ya bajeti ya mwaka huu ambapo tumetenga fedha nyingi sana kwa ajili ya kuendeleza sekta ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa kukopa 'Mzinga lipa Asali' ambao unatekelezwa na *SIDO*, tayari umeishaanza kutekelezwa katika maeneo mengine na Wilaya za Kahama na Bukombe zinategemea kushirikishwa kuanzia mwaka huu wa fedha.

Na. 421

**Kupanda kwa Bei ya Mafuta Duniani**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Bei ya mafuta katika soko la Dunia imepanda sana.

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu utekelezaji mradi wa matumizi ya gesi kwa magari hapa nchini?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya utekelezaji wa mpango wa uagizaji wa ununuzi wa mafuta kwa kiwango kikubwa *(bulk purchasing)*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPDC* kwa kushirikiana na *Pan African Energy* walianza mchakato wa mradi wa kutumia gesi asili kwenye magari, viwandani, majumbani na matumizi mengine mbalimbali ya chanzo hiki cha nishati (nishati ya gesi), kwa lengo la kupanua manufaa ya kiuchumi na kijamii yanayopatikana kwa matumizi makubwa ya vyanzo vingine vya nishati kwa mfano bidhaa za petroli *(Hydrocarbons)* na kuni *(Biomass),* ambayo yana athari kubwa za kiuchumi, kijamii kwa mazingira na afya za binadamu kutegemea na matumizi.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa awali mwaka 2008 ulikuwa ni kuanzisha vituo vya mfano na masoko ambapo kituo cha kujaza gesi kwenye magari cha Ubungo, Dar es Salaam kilianzishwa. Kituo hicho kina uwezo wa kujaza magari 200 kwa siku, na kilianza kufanya kazi mwaka 2010 baada ya kazi ya ujenzi kukamilika. Mpaka sasa mifumo ya magari 36 imebadilishwa ili kuweza kutumia gesi asili. Kasi ya ubadilishaji wa mifumo ya magari imekuwa ni ndogo kutokana na gharama za ubadilishaji kuwa kubwa. Takribani, zaidi ya shilingi milioni moja zinahitajika kubadilisha mfumo gesi kwa gari moja linalotumia mafuta ya petroli ili liweze kutumia gesi asili.

Aidha, kasi ndogo ya kazi za masoko zimepelekea ufahamu mdogo kwa wamiliki wa magari wa manufaa ya matumizi ya gesi kwenye magari, ikilinganishwa na matumizi ya petroli.

(b) Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopatikana katika miaka na siku za karibuni katika masuala yanayohusika na sekta ya biashara ya mafuta, zimebaini umuhimu wa ushiriki wa Serikali kwa kupitia taasisi za umma kama *TPDC* na *EWURA* kwa lengo la kulinda maslahi na haki za wadau wote kwa maana ya wafanyabiashara, lakini pia watumiaji *(consumers)* wa nishati hiyo. Mfumo wa uagizaji wa mafuta wa pamoja kwa kiwango kikubwa *(bulk procurement)* umekusudia kukidhi malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huo, utekelezaji wa mpango huu wa *bulk procurement* utatekelezwa baada ya kanuni chini ya Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2008 kusainiwa na Waziri mwezi Juni, 2011. Hivi sasa kazi ya uundwaji wa Kamati ya ununuzi ambayo inahusisha wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi, Mamlaka ya Bandari, *TPDC, EWURA* na Umoja wa Makampuni yanayofanya biashara ya mafuta nchini *(TAOMAC)* imeanza. Mfumo huu unatarajiwa pamoja na kuleta nafuu ya bei ya mafuta nchini, kusaidia kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingizwa nchini na kuboresha makusanyo ya kodi itokanayo na biashara ya mafuta.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba nisisitize tu, kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba bado kuna matatizo ya ufahamu, watu hawajaelewa mfumo huo unavyofanya kazi vizuri. Lakini tatizo lingine kubwa ni vituo vya gesi. Kipo kituo pale Ubungo, mimi nipo Dar es Salaam nakwenda Muheza, wasiwasi wangu ni kwamba nikishajaza gesi pale Ubungo nikifika Muheza Tanga, Moshi, Arusha hakuna vituo. Je, kuna mkakati gani wa kuongeza idadi ya vituo ili angalau watu wawe na uhakika wa kupata huduma hiyo? *(Makofi)*

Swali la pili, naanza kwa ku-*declare interest* kwamba mimi nilikuwa nafanya kazi Shirika la Maendeleo ya Petroli na nilishiriki katika kuanzisha Kampuni tatu zifuatazo:-

Moja ni *COPEC* ambayo hivi karibuni imepewa leseni ya kuanza kuagiza mafuta, lakini ilianzishwa miaka zaidi ya 11 iliyopita. Lakini hapo hapo tulianzisha Kampuni nyingine *COPEC* ishiriki katika usambazaji wa mafuta. Lakini tulianzisha pia Kampuni nyingine ishiriki katika usimamizi wa mfumo wa usambazaji wa gesi, Kampuni inaitwa *GASCO* na nyingine inaitwa *KILAMCO* isaidie kwenye gesi na uzalishaji wa mbolea. Kampuni hizo zote tatu zilizoanzishwa lakini hazikupewa fursa ya kufanya kazi. Je, baada ya kizaazaa ambacho tumepata hivi karibuni cha kudhalilisha Taifa hili kwa Makampuni yaliyokuwa na hisa…

**SPIKA:** Tunaomba usituhubirie. Mheshimiwa Mntangi hiyo ni hotuba sasa. Naomba uulize maswali.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, tunasema nini sasa kuhusu kuirejesha Kampuni ya gesi ya *GASCO* ili iweze kusimamia usambazaji huo wa gesi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na tatizo lenyewe, lakini tunajibu kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tatizo kubwa ni matumizi ya gesi yenyewe. Magari yenyewe ni 36 kituo kinaweza kukidhi magari 200 na hii ilikuwa ni *pilot study* kwa maana ya kwamba kwa magari zaidi ya 10,000 yaliyopo Dar es Salaam, magari yenyewe 200 ni kweli hata ukiwa pale pale Dar es Salaam gari yako iko Mbagala, inaonyesha kwamba tanki imepungua mafuta uende mpaka Ubungo ndio urudi tena mjini, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kazi kubwa ni kuongeza kwanza ufahamu, lakini pia upatikanaji wa *CNG* yenyewe. Sasa tumekusudia kwamba mkakati wa kwanza ni kwamba ile *CNG* na *LPG* haipatikani kutokana na gesi yetu wenyewe. Kwa hiyo, mkakati wa kwanza ni kutoa *LPG instruction* kwa ile gesi ya kwetu wenyewe, hii inayozalishwa hapa, halafu tuboreshe matumizi ya gesi kwa mfano ziko nchi India, China na kadhalika ambako kwenye Halmashauri za Miji magari ya mabasi na kadhalika hayaruhusiwi kutumia petroli kwa sababu ya *environmental resources*. Kwa hiyo, nasi tufike sehemu ambayo mabasi, daladala, teksi na yale magari ambayo yanakwenda kwa mwendo wa kati kwa safari fupi fupi mijini itumie gesi asilia na hapa tutapata matumizi ku-*justify* vituo viongezeke na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, la pili la *COPEC* nimekubaliana naye. Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali imeirejesha *COPEC* ili isimamie zoezi la mafuta. Hili la *GASCO* nadhani ni kweli tunahitaji Kampuni ya kusambaza gesi, lakini litaendana na upatikanaji na kukua kwa matumizi ya hiyo gesi yenyewe katika jamii ya Watanzania.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, kwa sababu sasa tumeambiwa kwamba kuna bei elekezi ya mafuta. Naomba utufahamishe Bunge hili bei ya petroli, mafuta ya taa na dizeli ni shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimemwelewa Mheshimiwa Ndassa, alikuwa anauliza kwamba bei ya mafuta. Sijaelewa vizuri swali lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa, swali lako uliza tena kwa taratibu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Waziri naomba nikuulize swali, kwa sababu sasa tunaambiwa kuna bei elekezi ya mafuta, bei mpya, dizeli ni shilingi ngapi? Mafuta ya taa shilingi ngapi? Na petroli ni shilingi ngapi ili Watanzania wote wajue?

**SPIKA:** Bei elekezi ya *products* hizo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba kuna bei elekezi imetoka jana ambayo imezingatia viwango vilivyonunuliwa mafuta kwa maana ya *purchasing price* iliyokuja kwa haya mafuta yaliyopo nchini sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sijajua bado na siwezi kumhakikishia kwa sasa hivi kwamba bei *exactly*

ya mafuta hasa kwa sababu bei yenyewe ni elekezi kwa kila sehemu ya Tanzania. Bei elekezi ni tofauti kwa Mwanza na ni tofauti kwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, naomba ...

**WABUNGE FULANI:** Aaah!
**SPIKA:** Hamna. Hilo ni jibu. Kwa nini nyie mnabisha?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge atuletee baadaye, tumpe bei elekezi kwa maeneo yote ya Tanzania.

**SPIKA:** Sawa. Ni jibu sahihi kabisa.

Na. 422

**Umuhimu wa Nishati ya Gesi Asilia Katika Kuzalisha Umeme**

**MHE. YUSUPH A. NASSIR** aliuliza:-

Raslimali ya nishati ya gesi asilia ni chanzo muhimu na mahsusi cha kuzalisha umeme, ikiwemo ile ya Songo Songo na *Mnazibay*:-

(a) Je, ni lini vyanzo vingine vilivyopo vitatumika ili kuongeza uzalishaji umeme kwenye gridi ya Taifa?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujihusisha moja kwa moja na ujenzi wa miradi hiyo ili mapungufu yaliyotokea katika ujenzi wa mradi wa Songo Songo yasije kujirudia?

(c) Je, ni lini Mikataba ya Songo Songo na uhalali wa uwepo wa *PAE* kwenye sekta ya gesi asilia utaangaliwa upya ukizingatia hali halisi ya yaliyojitokeza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa jumla ya umeme unaotokana na raslimali yetu ya Gesi Asilia ni MW 400 zinazozalishwa Dar es Salaam kutokea kwenye chanzo cha Songo Songo Kilwa, MW 7.5 zinazozalishwa kwenye Kituo cha Somanga Fungu, Kilwa kwa gesi inayotoka kwa ajili ya Songo Songo, na MW 18 zinazozalishwa kwenye kituo cha umeme Mtwara, kwa gesi inayotokana *Mnazibay* kufanya jumla ya MW 425.5 zinazoingia katika mfumo wa umeme wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili vyanzo hivi vipya vya gesi asili viweze kutumika kukidhi mahitaji ya gesi asilia yanayozidi kuongezeka *TPDC* kwa kushirikiana na Makampuni yanayohusika *(Maurel and Prom, Ndovu Resources,* na *BG)* yamejipanga kuchimba visima zaidi ili kubaini kiasi cha gesi kilichopo. Kazi hii itafuatiwa na shughuli za kuendeleza vyanzo hivyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali zikiwemo kukamilisha bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam ifikapo Desemba, 2013, kuzalisha umeme, matumizi ya gesi viwandani, na pia katika sekta nyingine za uchumi. Aidha, miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme kutokana na vyanzo vingine kama vile makaa ya mawe, maji na upepo vinaendelezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali kwa kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli *TPDC* iko katika mchakato wa maandalizi ya ujenzi wa awamu ya kwanza ya bomba la kusafirisha gesi asili kutoka *Mnazi Bay* hadi Dar es Salaam kupitia Somanga Fungu – Kilwa. Maoni ya Mheshimiwa Mbunge ndiyo msimamo wa sasa kwenda mbele, wa Serikali kuhusiana na miradi hii nyeti ya miundombinu. Uwekezaji na umiliki wa miundombinu hii ya gesi asili itakuwa chini ya Serikali ili kupunguza ukiritimba unaoweza kutokea kwa miundombinu kama hii kumilikiwa na makampuni binafsi.

(c) Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 mikataba ilifanyiwa durusu ili kuruhusu malipo ya mtaji wa mwekezaji na hivi sasa durusu inaendelea kuruhusu mradi wa *Songas* wa upanuzi wa miundombinu ya mradi wa Songo Songo. Aidha, bado Serikali na *TPDC* wako katika mazungumzo na Kampuni ya *PAT* kwa lengo la kurekebisha maeneo kadhaa katika mkataba wa kugawana mapato ya mradi wa Songo Songo.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa kuna mapungufu makubwa katika gharama zinazotolewa na Kampuni ya *Songas* pamoja na *Pan Africa* kwenye miradi mbalimbali. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na kuhusisha Taasisi nyingine kama vile *EWURA*, *Auditor General* na hata *PPRA* kwa ajili ya kuhakiki na kutathmini gharama halisi za miradi hii?

Pili, kwa kuwa kumekuwa na mapungufu ya uadilifu wa kimkataba kati ya *Pan Africa* na *TPDC* kilichopelekea Serikali kupunjwa dola milioni 65 na hatimaye katika Mkutano uliofanyika mwezi Mei wakakubali kulipa dola milioni 28, ni lini fedha hizi zitarejeshwa Serikalini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, katika mfumo wa kufanya *auditing* ya gharama hizo, siyo kwa *Songas* na *Pan Africa* tumegundua kwamba kuna matatizo ambayo yametokea na kama unavyosema baada ya kufanyiwa *auditing* imegundulika na sisi katika upande wetu tumesema kwamba zilizopungua ni milioni 65 wao wamesema ni shilingi milioni 28, tumewaambia basi lipeni hizo kwanza. Lakini mkakati wa ku-*involve* hawa wote kwa maana ya *CAG* na nini, siyo tu kwa mkataba huu, lakini tunatarajia uwe ni utaratibu sasa wa kuwa, tuwe tuna macho zaidi katika mikataba yetu kwa sababu kwa namna hii tunaweza tukawa tunapoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimekubali kwamba Taasisi nyingine ambazo zina uwezo wa kushiriki katika kubaini haya mapato ya Serikali yanayopotea yatashiriki katika kufuatilia mapato haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umeulizwa, ni lini shilingi milioni 28 zinalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama wiki mbili zilizopita tuliwaita *Pan African* na *Songas* na *TPDC* hapa Dodoma ili wakutane na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na kubaini ile miradi mingine lakini pia kwa kujadiliana na hili. Kwa hiyo, kwa majadiliano ya malipo ya hii shilingi milioni 28 bado inaendelea, lakini tunawahimiza kwamba walipe haraka iwezekanavyo.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *EWURA* wametangaza asilimia tano ya ongezeko la bei ya mafuta na siku zilizopita walisema wana mafuta ya kutosha kwa siku 48 mpaka 60 na kwa kisingizio kwamba shilingi imeporomoka. Je, hayo mafuta waliyoyapandisha ni haya yatakayokuja baadaye au haya yaliyoko ndani ya *stock?* Kwa nini yamepandishwa?

**SPIKA:** Hili swali lilikuwa *relevant* kwa hili swali lililotoka. Hili swali la pili halikuwa *relevant.* Tusiulize maswali kwa sababu tunapenda, eeh! Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa kawaida wa kisheria, zoezi la kupitia bei ya bidhaa ya petroli nchini hufanyika kila baada ya wiki mbili, yaani siku 14. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kilichofanyika jana ni mwendelezo wa zoezi ambalo lilikuwa likifanyika kabla hata ya juzi *formula* ya kukokotoa bei kwenye bidhaa hizi kufanywa.

Hili ni zoezi la kawaida. Wote tutakumbuka kwamba kuna kipindi ambapo kwa mfano kama hakuna ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia ama hakuna mabadiliko katika *exchange rate* ya fedha yetu wakati fulani tumekuwa tukisikia bei za mafuta zinashuka. Kwa hili zoezi lililofanyika jana limezingatia hilo. Lakini kikubwa kilichosababisha jambo hilo ni mambo mawili. La kwanza, bei katika Soko la Dunia imeongezeka, lakini pia *exchange rate* ya fedha yetu imebadilika kidogo.

Kuhusu suala la msingi ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba, je, kwa *stock* ambazo zipo hapa nchini ambazo hazijaathiriwa na bei kwa sababu katika hali ya kawaida haitarajiwi kwamba leo imetangazwa mabadiliko ya bidhaa, *stock* iliyoko hapa ndani haiwezi kuletwa *forward* ikatumika kwa bei ambayo imetangazwa leo. Hilo tutalifuatilia pamoja na *EWURA* kujua kwa sababu *stock* zilizoko hapa hazikuathiriwa na bei hii ambayo imetangazwa jana. Naamini kwamba *EWURA* watakuwa makini kusimamia hilo.

Na. 423

**Ahadi ya Kujenga Barabara za Mbinga Mjini**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais katika Kampeni za uchaguzi mwaka 2010, aliahidi ujenzi wa barabara za Nyoni – Maguu – Mkoha na ile ya Mbinga – Litembo kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya gharama za kazi hizo na ni lini ujenzi utaanza ili kutimiza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kuanza kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu Barabara za Unyoni – Maguu – Mkoha (Kilometa 30.4) na vile vile barabara ya Mbinga – Litembo (Kilometa 30) katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetenga jumla ya Shilingi milioni 80.4 kwa ajili ya kujenga mita 300 katika mlima wa Luwaita katika barabara ya Mbinga - Litembo kwa kutumia "*Otta Seal*" ili barabara hiyo iweze kupitika kwa urahisi majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa barabara hizo zitaanza baada ya kukamilika kwa usanifu na kupata fedha za kugharamia ujenzi huo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Lakini pia naipongeza Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanatutia matumaini sana kwa wananchi wa Vijiji vya Tanga, Miyangayanga, Kindimba, Mbuji, Litembo lakini pia Unyoni, Maguu, Mapela, Manjilo, Mikaranga na Mkoha. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Hii barabara ya Mbinga – Litembo haiishii pale, inakwenda mpaka Kitula, Mzuzu na kwa muda mrefu imekuwa haitengenezwi, ingawaje ni kweli kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais kuweka lami mpaka Litembo. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akawasaidia wananchi wa kutoka pale Litembo mpaka Kitula na Mzuzu kuhakikisha hii barabara ya kipande hiki ambacho hakijatengenezwa muda mrefu kitaanzwa kutengenezwa na kuwa imara zaidi?

La pili, pale Mbinga Mjini barabara nyingi zimewekwa lami na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na barabara ambayo haina lami kwa sasa ni hii ya kutoka Mbinga inaelekea Litembo na Serikali ya Mkoa ilikuwa imeahidi kuweka lami katika kipande hicho ili lile vumbi linaloathiri pale mjini kwa sababu tu hii barabara ni barabara kuu ya Serikali: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuangalia uwezekano wa angalau kuanza na hiki kipande cha Kilomita tano?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, rafiki yangu kwamba barabara hizi mbili alizoziongelea, barabara ya Unyoni – Maguu mpaka Mkoha na barabara ya Mbinga – Litembo mpaka Mkiri, hizi barabara zilikuwa za Wilaya. Ni miaka mitatu tu iliyopita tumezipandisha daraja kuwa barabara za Mkoa. Kwa hiyo, sisi tunahudumia Mbinga – Litembo mpaka Mkiri na barabara nyingine zinazoweza kuhudumiwa na Halmashauri. Lakini la pili, ni kuhusu kama tunaweza kuanza Kilomita tano katika barabara hiyo tuliyoizungumzia ya Mbinga – Litembo – Mkiri. Hatuwezi kufanya hivyo bila kufanya upembuzi yakinifu na vile vile usanifu wa kina. Huu ndiyo ujenzi wa kisayansi katika barabara hizo sasa hivi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais Mbinga Mashariki ni sawa kabisa na ile aliyoitoa mkoani Mara kwenye Kampeni za Uchaguzi mwaka 2010 ya ujenzi wa barabara ya Mika – Utegi – Shirati mpaka Mpakani mwa Kenya, sasa nilitaka kujua ni lini barabara hii itajengwa ili kutimiza ahadi ya Rais kuweza kuinua uchumi wa Mkoa wa Mara?

**SPIKA:** Kilicho sawa sawa tu ni ahadi. Lakini kwamba barabara ziko sawa sawa, siyo kweli. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunaelewa kabisa kuhusu barabara ya Mika – Utegi – Shirati kwamba ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na kama tulivyosema mara kwa mara Bungeni, hii ni bajeti ya kwanza tu, tunaomba Waheshimiwa Wabunge muwe wavumilivu, bajeti nyingine zinakuja na tunaendelea na ujenzi wa Kilomita zaidi ya 11,300 hatuwezi kuzifanya kwa mara moja.

Na. 424

**Samani kwa Maofisa wa Serikali Majumbani**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Maofisa wa Serikali wanaoishi kwenye nyumba za Serikali wanayo stahili ya kununuliwa samani. Je, Serikali inasemaje kwa Maofisa wanaoishi kwenye nyumba zao kuhusu stahili hiyo ya samani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Viongozi wa Serikali wanaoishi kwenye nyumba za Serikali wanayo stahili ya kununuliwa samani na Serikali. Samani zinazonunuliwa ni mali ya Serikali na zinabaki katika nyumba husika mara Kiongozi husika anapohama.

Mheshimiwa Spika, kwa Maofisa wanaoishi kwenye nyumba zao, hawanunuliwi samani na Serikali kwa mujibu wa taratibu zilizopo kwa vile nyumba wanazoishi hazisimamiwi wala kuratibiwa na Serikali.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye jibu lake amesema Maafisa wanaoishi katika nyumba zao binafsi hawapewi stahili zao za samani. Naomba nimpe taarifa kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikiwalipia posho Maafisa wake ya Sh. 119,373,000/=. Je, kwa maana hiyo, haijui *stock* ya mali zake?

Swali la pili, kwa kuwa nyumba za Serikali ziliuzwa na Maafisa hawa ambao wanaishi kwenye nyumba zao binafsi ni haki yao kupata samani: Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kurudisha nyumba zile ili na wao waweze kupata stahiki hizo kwa sababu ni haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pengine jibu langu lilikuwa fupi mno na la ujumla. Nifafanue kidogo tu kwamba ninapoongelea hapa viongozi wa Serikali ni makundi mawili. Kundi la kwanza ni Watendaji Waandamizi wa Serikali ambao wana stahili ya kupewa samani na kupewa nyumba za Serikali. Lakini pale ambapo mtu mwenye stahili ya kupewa nyumba ya Serikali, anapokaa kwenye nyumba yake mwenyewe, tunawalipa *housing allowances*. Kwa hiyo, siyo kitu cha ajabu kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii anachokiona.

Ninachozungumza ni *category* nyingine, kwa mfano, Viongozi wa Kisiasa, kwa mfano, Mawaziri na Manaibu wao ni msimamo wa Serikali kwamba waishi kwenye nyumba za Serikali na ndiyo maana Naibu Waziri au Waziri akiamua kukaa kwenye nyumba yake halipwi hata *housing*

*allowance* wala hawekewi samani kwa sababu tuna Wasukuma wote wahamie kwenye nyumba za Serikali. Changamoto ipo tu pale ambapo Waziri hajapewa hiyo nyumba na hilo tunalifanyia kazi.

**MHE. PAULINA G. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Samani nyingi zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, hazina ubora na siyo imara. Ni lini Serikali itaanza kutumia raslimali za nchini, misitu tuliyonayo kama miti ya mininga kutengeneza samani hizo badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kawaida kiutendaji siyo kwamba Serikali ndiyo inaagiza samani kutoka nchi za nje. Tunatumia Sheria Na. 21 ya mwaka 2004, kutangaza *tender* na wale wanaoshinda *tender* ndiyo wanaotuletea samani na bahati mbaya au nzuri wamekuwa wakituletea samani ambazo mara nyingi zimekuwa hazifai. Lakini Serikali baada ya kusikia kilio cha wadau wengi tumekuwa tunatoa *specifications* kwamba tunahitaji samani imara na tunaweza kukuhakikishia kwamba samani imara ni zile ambazo zinatokana na vifaa vya kwetu na zinatengenezwa hapa nchini.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Nawakumbusha wale Mawaziri wanaojibu maswali *page* mbili, wasivuke hapo na Wabunge wanaohutubia wenzao waache. Kwa hiyo, tuwe tunauliza maswali mafupi ili tupate waulizaji wengi.

Washimiwa Wabunge, nina matangazo ya wageni, siwezi kuwatangaza wageni ambao ni wa Wabunge binafsi, natangaza wageni wa makundi ambao ninao hapa. Kwanza kabisa, nina wageni wa Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka - Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Makamishna, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yake wakiongozwa na Mheshimiwa Patrick Rutabazibwa, Katibu Mkuu wa Wizara, pia amefuatana na Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Maria Bilia.

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye ambaye ni Mkewe mpendwa anaitwa Antonia Kalisti Lekule na familia yake. Lakini pia amekuja Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arumeru, Ndugu Joseph Saivoye Ole-Loning'o. Pia yupo na Katibu wa Chama cha Wapangaji Tanzania, ameongozana na Wajumbe wengine watatu wa chama hicho. Nina Madiwani 24 kutoka Halmashauri ya Wizala ya Tarime na Viongozi wanne kutoka CCM kutoka Tarime. Hii Wilaya ya Tarime ni ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine. Halafu nina wageni 50 kutoka Kata ya Manchali kutoka Jimbo la Chilonwa, ahsante sana tunawakaribisheni. Halafu nina wageni kutoka kwenye Jimbo la Mheshimiwa David Kafulila, ni Mwenyekiti wa Kijiji ambacho hakikutajwa jina kwa tikei ya *NCCR* Mageuzi na Mwenyekiti mwingine wa kijiji kingine ambacho hakikutajwa jina, karibuni sana. Naogopa kurudia utaratibu wa zamani wa kutaja kila mtu pamoja na watoto wadogo. Hili Bunge ni la wazi kwa kila mtu. Kwa hiyo, wageni wetu mliopo hapa mnakaribishwa. Leo sina tangazo la kazi, ila nina matangazo mawili. Kwanza Mheshimiwa Capt. John Komba, juzi nyumba yake imeungua na moto kule Jimboni kwake, wengine walikuwa wanafikiria ni Dar es Salaam labda Mbinga Mjini, lakini ni kule kule Jimboni kwake Lituhi. Sababu za moto huo bado hatujazifahamu. Lakini nina tangazo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, tukiwa humu ndani ya Bunge, tuko kazini na tunao Wabunge, tuna Mawaziri na tunaye Mheshimiwa Waziri Mkuu na mazungumzo yote humu yanaongozwa na meza hii. Sasa ipo tabia ambayo siyo njema na inaendelea mpaka sasa. Wabunge wanakwenda kuongea na Waziri Mkuu na picha itapigwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu wanaokuja kuongea na wewe. Sasa kama Waziri Mkuu *attention* yote itakuwa kwa Mbunge mmoja mmoja, basi naomba Waziri Mkuu akae Ofisini. Itakuwa rahisi kwa Waziri Mkuu akiwa ofisini kuongea. Hakuna sababu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akija hapa lakini Wabunge wote tunafoleni kwenda kuzungumza naye pale. Kwa hiyo, hakuna *attention.* Madhumuni ya kuwa Waziri Mkuu ambaye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali ni kusikiliza maswali, majibu maongezi yanayotokana na Wabunge wote.

Kwa hiyo basi, uamuzi wangu ni kwamba Wabunge wengine wote kama mnamtaka Waziri Mkuu ni kule ofisini kwake na Mawaziri watakaokwenda pale kwake wawe na swali linalohusu mambo tunayoendelea nayo hapa. Vinginevyo mna nafasi yenu kule ofini. Mnajua *incidences* mbalimbali zilizotokea, Waziri Mkuu yupo humu ndani lakini hayupo na sisi kwa sababu mtu anakaa pale dakika 15 anaongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Sasa nawaombeni kabisa, hii iwe utaratibu na tutaiingiza kwenye Kanuni, kwa sababu *otherwise* hakuna sababu ya kuwa na Kiongozi wa Serikali Bungeni kama itaendelea kuwa hivi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7) inasema: *"Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambako hakuna Mbunge mwingine anayasema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo kwa hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."*

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wangu unahusu Kanuni ya 46.

**SPIKA:** Hiyo ndiyo uisome.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, inahusu maswali kujibiwa kikamilifu.

*"Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama alivyoulizwa isipokuwa kama jibu linalohusu ni refu au lina takwimu nyingi. Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza kabla muda wa kujibu swali hilo haujafikiwa."*

Mheshimiwa Spika, nilivyokuwa nauliza maswali yangu ya nyongeza, swali langu la pili halikujibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ni sawa, lakini tunaomba tutumie muda huu vizuri zaidi. Kuna vipindi vingi, wewe unaweza kusema kwamba Waziri alipokuwa anajibu swali langu hakunijibu katika maeneo haya. Sasa tukisema tuanze sasa hivi, ni mimi tu ambaye nina mamlaka ya kumwambia Waziri jibu lako sijaridhika, ukarudie tena. Sasa hilo unaweza kulileta kwa utaratibu mwingine.

Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewane pia, wale wa maswali ya nyongeza afadhili Mheshimiwa Owenya alikuwa na swali lake la msingi. Wale wanaorushia maswali hapa mtapata majibu hafifu kwa sababu yeye hakujua kama nyie mtauliza hivyo. Kwa hiyo kwa swali la msingi ni vizuri Waziri akampa maelezo halafu atueleze kitu gani hakikuwa sahihi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Hapana! Kuhusu nini?

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Kuhusu maelezo uliyoeleza.

**SPIKA:** Ya nani?

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, ya kwako. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae kwanza. Nimemjibu yule aliyeomba mwongozo. Sasa haiwezi kuwa mwongozo juu ya mwongozo. Sasa tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Bunge lako lipokee na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi sote kuwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi chake cha pili na Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal kuwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa Katavi, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu.

Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamana kubwa aliyonipa kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sekta ambayo nilibahatika kuishughulikia kwa miaka ipatayo kumi nikiwa Katibu Msaidizi Mkuu *(UN Under-Secretary General)* na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi *(UN-Habitat).* Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi ya kutumia uzoefu nilioupata huko kutumikia nchi yangu. Naahidi kwamba kwa baraka za Mwenyenzi Mungu nitafanya kila linalowezekana kufikia matarajio yake na ya wananchi wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nakupongeza sana kwa kujenga historia ya nchi yetu kwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke wa Bunge hili Tukufu. Nakupongeza kwa umahiri na umakini ambao tayari umeonyesha katika kuongoza shughuli za Bunge. Hongera sana, na Mwenyezi Mungu aendelee kukuongoza na kukupa hekima. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai - Mbunge wa Kongwa, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Pia nawapongeza Waheshimiwa Jenista Joakim Mhagama - Mbunge wa Peramiho, Sylivester Massele Mabumba - Mbunge wa Dole, na George Boniface Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa kunichagua bila kupingwa kuwa Mbunge wao katika uchaguzi wa mkuu wa mwaka 2010 na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru ndugu, jamaa na marafiki walioshiriki katika kuniwezesha kurejea nyumbani kutoka Umoja wa Mataifa. Kipindi cha mpito kilikuwa kigumu kwangu na chenye hekaheka nyingi, lakini kwa msaada, imani na mapenzi waliyonipa mambo yamekwenda vizuri.

Nawashukuru wananchi na ninawahakikishia popote pale mlipo, iwe Tarafa ya Nshamba, Kimwani au Muleba yenyewe, kwamba tutajifunga kibwebwe kuliendeleza Jimbo la Muleba Kusini na Wilaya ya Muleba kwa ujumla kwa ari, nguvu na kasi zaidi. Pia, napenda kutoa salamu zangu kwa Watanzania wote na kuwashukuru kwa moyo wao wa kulinda amani na utulivu katika kuendeleza demokrasia. Ni sifa ambayo imeleta heshima kubwa kwa Taifa letu. Asiwadanganye mtu, kwani kote nilikopita duniani wakati nikitumikia Umoja wa Mataifa tulitambuliwa kwa sifa hiyo. Namwomba Mwenyezi Mungu amwezeshe kila mwananchi kulitambua hili na kuchangia katika nafasi yake na kadri ya uwezo wake ili hali hiyo iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na viongozi na Watendaji wa Serikali kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Kwa namna ya kipekee, natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli - Mbunge wa Kahama, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Natoa shukurani za pekee kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye - Mbunge wa Arumeru Magharibi; Katibu Mkuu - Bw. Patrick Rutabanzibwa; Naibu Katibu Mkuu - Bibi Maria Bilia; Watendaji katika Idara, Vitengo, Shirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushauri na mshikamano wao katika kupanga na kutekeleza mipango ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi ni idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na kijamii katika miji na vijiji nchini inayoongezeka kwa kasi kuliko uwezo wa Serikali wa kupanga, kulipa fidia, kupima na kugawa ardhi, na kusimamia uendelezaji wake. Kutokana na hali hii, Wizara katika kutekeleza majukumu yake, inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

(i) Kutokuwa na mfumo thabiti wa utunzaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi;

(ii) Ardhi kwa ajili ya uwekezaji na matumizi mbalimbali ya Serikali kutopatikana kwa urahisi mijini na vijijini;

(iii) Uelewa mdogo wa wananchi, Viongozi na Watendaji wengi kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za uendelezaji ardhi, nyumba na makazi;

(iv) Gharama kubwa za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, upangaji wa miji na upimaji wa ardhi nchini;

(v) Upungufu mkubwa wa nyumba bora mijini na vijijini na riba kubwa ya mikopo ya nyumba inayotolewa na mabenki;

(vi) Ujenzi holela Mijini na uvamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma za jamii kama vile maeneo ya wazi;

(vii) Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi na nyumba hasa kwa maeneo ya mijini na vijijini; na

(viii) Nakisi ya bajeti inayotengewa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo ambazo zimetukabili kwa kipindi kirefu, zimeendelea kuathiri maendeleo ya Sekta ya Ardhi. Hata hivyo, tunayo matumaini kwa kuwa ni Sekta mtambuka yenye wadau wengi, tukishirikiana kwa pamoja na kuwa wabunifu, tutaweza kuzipatia ufumbuzi wa kudumu kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeazimia kuendelea kukabiliana na changamoto hizo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuanza kujenga mfumo mmoja wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa njia ya kielektroniki *(Integrated Land Management Information System)* utakaounganisha mifumo yote ya utunzaji wa kumbukumbu za Sekta ya Ardhi;

(ii) Kuanzisha chombo kitakachosimamia Hazina ya Ardhi *(Land Bank)* ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miradi ya uwekezaji na kuunda Mfuko wa Kulipa

Fidia *(Land Compensation Fund)* kwa mujibu wa Sheria za Ardhi ili kuiwezesha Serikali kulipa fidia kwa wakati inapotwaa ardhi kwa maslahi ya umma;

(iii) Kutoa elimu kwa umma na kwa viongozi na Watendaji wa Serikali za Mitaa kuhusu Sera, Sheria na kanuni za ardhi, nyumba na makazi nchini;

(iv) Kukamilisha usimikaji wa alama za rejea za upimaji wa ardhi na kujenga kituo cha kupokea picha za *satellite* ili kurahisisha na kupunguza gharama za upimaji;

(v) Kuongeza kasi ya kueneza matokeo ya utafiti unaofanywa na Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Majengo *(NHBRA)* na kutoa mafunzo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi;

(vi) Kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa kuwa mwendelezaji mkuu wa nyumba na majengo mbalimbali;

(vii) Kuhamasisha makampuni binafsi kujenga nyumba za kuuza na kupangisha hususan za gharama nafuu;

(viii) Kuhamasisha wananchi kuanzisha Vyama vya Ushirika wa Nyumba *(Housing Cooperatives);*

(ix) Kuiwezesha kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)* kuyakopesha mabenki mikopo ya ujenzi wa nyumba yenye masharti nafuu ili mabenki nayo yatoe mikopo yenye riba kidogo;

(x) Kutekeleza Programu ya Taifa ya Kurasimisha na Kuzuia Makazi Holela Mijini kwa kushirikiana na Halmashauri;

(xi) Kurejesha kada ya Askari Ardhi *(Land Rangers)* katika Halmashauri ili kudhibiti uvamizi wa maeneo ya wazi na ujenzi holela. Utekelezaji wa mkakati huu tayari umeanza katika Jiji la Dar es Salaam;

(xii) Kuimarisha vyombo vya kusimamia maadili na weledi wa wataalam wa sekta ya ardhi katika ngazi zote; na

(xiii) Kuendelea kuunda Mabaraza mapya ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya hasa kwenye Wilaya zenye migogoro mingi na kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuyaimarisha Mabaraza ya Ardhi kwenye ngazi ya Vijiji na Kata.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Sh. 20,641,200,000/= kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato katika Sekta ya Ardhi. Hadi Juni, 2011 jumla ya Sh. 15,689,390,778/= ambazo ni sawa na asilimia 76 ya lengo zilikusanywa. Upungufu wa makusanyo ya maduhuli ulitokana na baadhi ya changamoto nilizozieleza hapo awali, hususan kutokuwa na mfumo thabiti wa usimamizi wa kumbukumbu za ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara imeweka lengo la kukusanya Sh. 20,665,000,000/=. Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

Kuimarisha ufuatiliaji wa kumbukumbu za ardhi; kupanga, kupima na kumilikisha maeneo mapya; kukamilisha upimaji na umilikishaji wa viwanja kwenye maeneo ambayo hayajakamilika; na kuhamasisha wananchi kulipa kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wamiliki wa ardhi nchini kulipa kodi ya pango la ardhi na ada nyingine kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuepuka usumbufu ikiwemo tozo na kunyang'anywa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011 Wizara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 53,362,742,663/=. Kati ya fedha hizo Sh. 7,573,264,663/=, sawa na asilimia 14 ya fedha zilizoidhinishwa, zilitengwa kwa ajili ya mishahara, Sh. 25,159,688,000/=, sawa na asilimia 47, zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh. 20,629,790,000/=, sawa na asilimia 39, zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Juni, 2011 jumla ya fedha zilizopatikana ni Sh. 31,769,391,298/=, sawa na asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopatikana, Sh.7,573,264,663/= zilitumika kwa ajili ya mishahara, Sh. 18,322,743,635/=, kwa ajili ya matumizi mengineyo, na Sh. 5,873,383,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za Maendeleo zilizopatikana zilikuwa sawa na asilimia 28 tu ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Hadi Juni, 2011 kiasi kilichotumika ni Sh. 31,423,143,942/= sawa na asilimia 99 ya fedha zilizopatikana.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni mhimili na raslimali muhimu katika kukuza uchumi wa nchi. Kwa kuzingatia umuhimu wake, Wizara yangu inaendelea kutoa huduma za utawala na usimamizi wa ardhi kwa lengo la kuimarisha usalama au uhakika wa milki. Huduma zinazotolewa ni pamoja na utoaji wa hatimiliki za ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, utwaaji ardhi kwa manufaa ya umma na ubatilishaji milki za wanaokiuka masharti ya milki zao. Vilevile, Wizara inatoa elimu na miongozo juu ya sera na Sheria za Ardhi, na inahamasisha uanzishwaji wa Masjala za Ardhi za Wilaya na Vijiji kwa lengo la kufanikisha utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Hati za Hakimiliki ya Kimila.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuandaa hatimilki za ardhi huanzia kwenye ngazi ya Halmashauri na huishia katika Ofisi za Ardhi za Kanda. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilitayarisha na kutoa hatimilki 19,648. Lengo lilikuwa ni kutoa hatimilki 20,000. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu inatarajia kutayarisha na kutoa hatimiliki 21,000. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha na kuboresha matumizi ya teknolojia ya kompyuta ili kuharakisha uandaaji wa hatimiliki na kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliahidi kufungua Ofisi ya Ardhi ya Kanda ya Magharibi Mjini Tabora itakayohudumia Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Kigoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa jengo kwa ajili ya ofisi hiyo limepatikana. Ofisi hiyo itatoa huduma za Sekta ya Ardhi ikiwa ni pamoja na huduma za mipango miji na vijiji, upimaji, umilikishaji, usajili, uthamini na ushauri kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba. Kwa mwaka 2011/2012 ukarabati utafanyika ili Ofisi hiyo ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliahidi kugatua mamlaka ya kuidhinisha upimaji wa ardhi katika Kanda sita za Sekta ya Ardhi ambazo ni Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kusini (Mtwara), Kusini Magharibi (Mbeya), Kati (Dodoma), Ziwa (Mwanza), na Kaskazini (Moshi). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya kugatua mamlaka hayo yamekamilika. Ofisi na vitendea kazi vimepatikana.

Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itawahamishia kwenye Kanda hizo watumishi watakaosimamia upimaji, ukaguzi na uidhinishaji wa ramani. Natoa wito kwa wananchi kuzitumia Ofisi za Kanda za Ardhi na Halmashauri nchini kupata huduma za ardhi, badala ya kufuata huduma hizo moja kwa moja kwenye Makao Makuu ya Wizara, kwani husababisha gharama na ucheleweshaji usio wa lazima katika kupata huduma hizo kwa mwananchi. Hata hivyo, ieleweke kwamba Wizara iko tayari kupokea rufaa pale ambapo mwananchi hakuridhika na maamuzi ya ofisi ya Kanda.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Wizara yangu ya mwaka jana, nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itahakiki milki 4,018 katika maeneo ya Tegeta, Mbezi, *Jangwani Beach*, Ununio na Boko, Jijini Dar es Salaam. Hadi Juni, 2011, jumla ya milki 3,535 (asilimia 88) zilihakikiwa. Kazi ya kuhakiki milki 483 zilizobaki itakamilika katika mwaka 2011/2012. Aidha, jumla ya migogoro 58 ilijitokeza kutokana na uhakiki huo. Kati ya migogoro hiyo, 46 (asilimia 79) ilitatuliwa kiutawala na migogoro 12 haikuweza kutatuliwa. Hivyo, wahusika walishauriwa kwenda Mahakamani. Natoa wito kwa wananchi walioko kwenye maeneo tajwa ambao hawajawasilisha nyaraka zao kwa ajili ya uhakiki waziwasilishe Wizarani. Vilevile natoa wito kwa wananchi kufuata taratibu sahihi za kisheria katika kupata ardhi ili kujiepusha na migogoro na hasara itokanayo na vitendo vya kujipatia ardhi kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 (Sura ya 113) kila mmiliki wa ardhi ana wajibu wa kulipa kodi ya pango la ardhi, kuiendeleza kwa wakati kwa matumizi yaliyopangwa na kulinda mipaka yake. Mmiliki anayekiuka masharti haya anapaswa kuchukuliwa hatua kwa kubatilisha milki yake na kurudisha ardhi husika mikononi mwa Mheshimiwa Rais.

Aidha, pale ambapo ardhi inahitajika kwa manufaa ya umma, inaweza kutwaliwa chini ya Sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya mwaka 1967 (Sura ya 118). Utaratibu wa utwaaji na ubatilishaji unaanzia ngazi ya Halmashauri hadi ngazi ya Taifa, na uhamisho wa milki unaanzia katika ngazi za Halmashauri na kuishia katika Ofisi ya Ardhi ya Kanda. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya milki 64 zilibatilishwa. Wizara yangu itaendelea kutwaa ardhi na kubatilisha milki kwa mujibu wa sheria. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuwasilisha Wizarani taarifa za viwanja na mashamba yaliyotelekezwa na kutumika kinyume na masharti ya milki ili hatua za kubatilisha milki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, uhamishaji wa milki ya ardhi hutokana na wananchi na makampuni kuuza au kurithisha mashamba na viwanja. Kwa mwaka 2010/2011 jumla ya milki 950 zilihamishwa kwa kufuata taratibu za kisheria. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu inatarajia kushughulikia maombi 1,000 ya uhamisho wa milki.

Mheshimiwa Spika, miradi maalum ya utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 (Sura ya 114) inaendelea katika Wilaya za majaribio kwa lengo la kujenga uwezo na kuandaa miongozo kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya ili ziweze kutekeleza sheria hiyo. Katika mwaka 2010/2011 miradi hiyo iliendelea katika Wilaya za Babati, Bariadi, Maswa, Bunda, Kilolo, Iringa na Mbarali. Kazi zilizofanyika katika Wilaya hizo ni kutoa elimu kwa wananchi na viongozi kuhusu sera na sheria za ardhi, upimaji na uhakiki wa mashamba, na utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Hati za Hakimilki za Kimila. Utoaji wa vyeti vya ardhi ya kijiji unaviwezesha vijiji kutambua maeneo yake kiutawala na kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi. Vilevile, utoaji wa hati za hakimilki za kimila unawezesha kuwepo kwa usalama wa milki kwa wananchi. Hivyo kuwawezesha kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu ilitoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 3,283 ikilinganishwa na lengo la vyeti 5,000, na kufanya jumla ya vyeti vilivyokwishasajiliwa nchini kufikia 7,510. Wizara iliandaa, kusajili na kutoa Hati za Hakimilki ya Kimila 46,063 na kufanya jumla ya Hati za Hakimilki ya Kimila zilizokwishatolewa nchini kote kufikia 157,968. Aidha, Ofisi za Masjala za Ardhi za vijiji 23 zilianzishwa na kufanya jumla ya masjala hizo nchini ifikie 408. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Ofisi ya Rais, na wadau wengine kupitia Mradi wa Mkakati wa Kurasimisha Raslimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), itanarajia kuandikisha na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 3,732 na Hati za Hakimilki ya Kimila 45,000 katika Wilaya mbalimbali nchini.

Napenda kuzipongeza Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Mpwapwa, Mufindi, Chato, Bukoba, Hanang, Karatu, Mbulu, Musoma, Kyela, Mvomero Misungwi na Mpanda kwa juhudi zao za kutoa hati hizo katika baadhi ya vijiji vyao. Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zote kuiga mfano huu kwa kutenga fedha kwa ajili ya kupima na kuhakiki mashamba ya wananchi na kuwamilikisha.

Vilevile, nazishauri Halmashauri za Wilaya kuwatuma viongozi na Watendaji wao kutembelea Wilaya za mfano kujionea faida kubwa ya upimaji na uhakiki wa ardhi vijijini. Naomba ieleweke kwamba uwezo wa Wizara yangu kutoa huduma hii katika Halmashauri kwa kasi inayotakiwa na wananchi ni mdogo sana ukilinganisha na mahitaji. Halmashauri zenyewe zijiwekee mikakati na mipango kazi ya kurasimisha ardhi ili Wizara ijikite katika kutunga sera, kutoa miongozo, kuwaendeleza wataalam wa Sekta ya Ardhi na kutoa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya, Ofisi ya Rais (kupitia MKURABITA) na wadau mbalimbali iliendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya sera na Sheria za Ardhi. Elimu hiyo ilitolewa katika semina zilizofanyika katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Wilaya zilizohusika ni Bunda, Kilolo, Maswa, Bariadi, Babati, Mbarali, Iringa

Vijijini, Kinondoni, Mafia, Mkinga, Simanjiro, Musoma, Serengeti, Njombe na Makete. Vilevile, elimu hiyo ilitolewa kupitia maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Saba Saba na Nane Nane.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha utayarishaji wa miongozo ya utekelezaji wa sheria za ardhi. Kwa mwaka 2011/2012 miongozo hiyo itasambazwa katika Halmashauri zote ili Watendaji waitumie katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yao. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu ilijiwekea lengo la kusajili hati za kumiliki ardhi na nyaraka nyingine za kisheria zipatazo 50,000. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Juni, 2011 jumla ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 59,544 zilisajiliwa. Kati ya nyaraka zilizosajiliwa, 22,923 ni hatimiliki, na 28,572 ni nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334). Vilevile, nyaraka 7,449 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) na nyaraka 600 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura ya 210). Kwa mwaka 2011/2012, Wizara ina lengo la kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria 60,000. Kati ya hizo, 25,000 zinatarajiwa kuwa hatimiliki na 35,000 nyaraka nyingine za kisheria.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011 Wizara yangu ilikusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Usajili wa Ardhi na Sheria ya Usajili wa Nyaraka za Kisheria ili ziendane na mabadiliko ya sera na sheria nyingine za sekta ya ardhi. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa rasimu za marekebisho ya sheria hizo zimetayarishwa. Kwa mwaka 2011/2012. Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria hizo baada ya kupata ridhaa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kufanya uthamini wa mali kwa ajili ya utozaji wa kodi ya pango la ardhi, ushuru wa Serikali kutokana na mauzo au uhamisho wa mali na mizania ya makampuni na asasi, na kwa ajili ya uwekaji mali rehani, mirathi na bima. Jumla ya uthamini 8,872 uliidhinishwa mwaka 2010/2011. Wizara yangu vilevile iliidhinisha taarifa za uthamini wa mali za wananchi walioguswa na miradi ya upanuzi wa barabara, uwekezaji katika migodi na misitu, na maeneo ya upimaji wa viwanja. Uthamini pia ulifanyika katika eneo huru la uwekezaji *(EPZ)* lililopo Bagamoyo, eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba Muhimbili huko Kwembe Mloganzila, Dar es Salaam na maeneo ya Mradi wa Mabasi yaendayo Kasi Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu imelenga kuthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali zipatazo 13,000 kwa madhumuni mbalimbali. Uthamini utafanyika kwa ajili ya fidia ili kupisha utekelezaji wa miradi ya kitaifa kama vile mradi wa Mji Mpya wa Kigamboni na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam katika eneo la Vijibweni, Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha rasimu ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini. Kwa mwaka 2011/2012 Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni baada ya kuridhiwa na Serikali. Kutungwa kwa sheria hiyo, pamoja na mambo mengine, kutaongeza uwazi katika shughuli za uthamini na kuongeza uwajibikaji wa wataalam wa uthamini nchini ili watekeleze kazi zao kwa weledi zaidi na kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya kisera, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu ilianza zoezi la kukusanya takwimu zitakazoiwezesha kukadiria vizuri zaidi thamani ya ardhi na mazao nchini kuanzia Mmkoa wa Dar es Salaam. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itahuisha viwango vya fidia nchini na kuanzisha mfumo wa kisasa wa Hazina ya Takwimu za Uthamini *(Valuation Data Bank)* ambao utawezesha uthamini wa mali kufanyika kwa uhakika na uwazi. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wathamini wa Mikoa na Halmashauri juu ya ukokotoaji wa viwango vya thamani ya ardhi, mazao na majengo.

Mheshimiwa Spika, tangu wazo la kuanzisha hazina ya ardhi libuniwe mwaka 2002, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mikoa na Halmashauri imefanya zoezi la kutambua ardhi inayofaa kuingizwa katika hazina hiyo ili itumike kwa ajili ya uwekezaji. Ili kutimiza lengo la kuwa na hazina ya ardhi, ardhi yake inatakiwa kuwa imepangwa, imepimwa na kusajiliwa, haina mgogoro kuhusu umiliki wala matumizi yake, iko karibu na huduma za msingi na miundombinu, au

kuna mipango ya kufikisha huduma hizo, na ina ukubwa wa kutosha kulingana na uwekezaji unaokusudiwa. Katika mwaka 2010/2011 mashamba 66 Mkoani Morogoro yaliainishwa kwa ajili ya kufutwa na kuingizwa kwenye Hazina ya Ardhi. Taratibu za ufutaji zinaendelea. Aidha, mashamba 112 Mkoani Arusha yalikaguliwa na kupendekezwa kuingizwa katika Hazina ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuanzisha Hazina ya Ardhi ili kupunguza urasimu katika utoaji wa ardhi kwa wawekezaji na kupunguza migogoro inayotokana na uwekezaji hususan vijijini, kwa mwaka 2011/2012 Wizara inatarajia kuanzisha chombo kitakachosimamia uanzishwaji wa Hazina ya Ardhi na utoaji ardhi ya hazina hiyo kwa wawekezaji kwa misingi ya kugawana hisa na wawekezaji hao, ambapo hisa zitatolewa kwa uwiano na thamani ya mtaji wa mwekezaji *(invested value method of land valuation)*. Lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika zaidi na ardhi katika maeneo yao, na kuongeza usalama wa miradi ya wawekezaji *(Sustainability of extensive land-based investments)*. Hisa na faida zitagawanywa kati ya Halmashauri, wawekezaji wa ndani na Serikali Kuu. Natoa wito kwa Bunge lako Tukufu kuunga mkono Muswada wa Sheria ya Kuunda Taasisi hiyo mara taratibu zitakapokamilika ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imetoa kipaumbele kwa uboreshaji wa mifumo yake ya kukusanya, kutunza na kutumia kumbukumbu za ardhi, na kuimarisha mawasiliano kati ya Makao Makuu yake na Ofisi za Ardhi za Kanda. Kuanzia mwaka 2005/2006 hadi Juni 2011, jumla ya Ofisi za Ardhi 32 za Halmashauri ziliwezeshwa kutumia mfumo wa kompyuta kutoa huduma za ardhi, kama vile kukadiria kodi ya pango la ardhi. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaziwekea Ofisi za Ardhi za Halmashauri 10 mifumo hiyo ya kompyuta. Halmashauri hizo ni za Manispaa ya Dodoma na Wilaya za Hanang, Njombe, Same, Hai, Kilosa, Mbeya, Masasi, Mpanda na Muheza. Pia, Ofisi za Ardhi za Kanda ya Kaskazini iliyoko Moshi na Kanda ya Ziwa iliyoko Mwanza zitaunganishwa kwenye mtandao wa kompyuta wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2010/2011, Bunge lako Tukufu lilielezwa juu ya azma ya Wizara ya kuweka mfumo mmoja wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi *(Integrated Land Information System)* ambao utaunganisha mifumo yote ya utunzaji wa kumbukumbu za Sekta ya Ardhi.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mchakato wa kumpata mtaalam mwelekezi wa kusanifu mfumo huo zinaendelea, na kazi ya kujenga mfumo inatarajiwa kuanza mwaka 2011/2012. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinatunza vizuri kumbukumbu zao za ardhi ili kuwezesha mfumo huu kujengwa kwa faida ya wananchi na Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu ilianza mchakato wa kuunda Mabaraza mapya matatu ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya za Nzega, Kilosa na Manyoni, kama sehemu ya mkakati wa kusogeza huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba karibu na wananchi. Idadi hii itafanya jumla ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya nchini kufikia 42. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu inakusudia kukamilisha taratibu za kuunda Mabaraza hayo matatu na itaanza mchakato wa kuunda Mabaraza mengine sita katika Wilaya za Ngorongoro, Mpanda, Karagwe, Tunduru, Kyela na Muleba. Vilevile itaimarisha utendaji kazi wa Mabaraza yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya iliendelea kushughulikia migogoro 13,203 ya ardhi na nyumba iliyokuwepo mwezi Juni, 2010 na mingine 12,643 iliyopokelewa hadi Juni, 2011. Mwaka 2010/2011 mashauri 10,092 yaliamuliwa, na mashauri 15,754 yanaendelea kusikilizwa.

Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kuimarisha Mabaraza kiutendaji ili kuondoa mlundikano wa mashauri katika Mabaraza hayo. Aidha, katika mwaka 2011/2012 Wizara itaanza mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba (Na. 2 ya mwaka 2002) ili kuongeza thamani ya mali inayohusika katika migogoro ya ardhi na nyumba inayoweza kusikilizwa katika Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuyaimarisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata kiutendaji ili kupunguza idadi ya mashauri yanayopelekwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa njia ya rufaa. Aidha, Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla wakumbuke kwamba Mabaraza ya Ardhi katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya yaliundwa baada ya mapendekezo ya Tume ya Ardhi iliyoundwa na Mheshimiwa Rais Mstaafu Alhaji Ali Hassan Mwinyi mwaka 1993/1994 chini ya Uenyekiti wa Profesa Issa Shivji. Lengo la kuunda Tume hiyo lilikuwa ni kupata mapendekezo ya kupunguza kero kubwa za ardhi kwa wananchi. Mlundikano wa kesi za ardhi katika Mahakama za kawaida ulikuwa mkubwa, hivyo ikaamuliwa Mabaraza yaundwe. Hata hivyo, hadi sasa Wizara haijaweza kupata fedha za kutosha kuweza kuunda Mabaraza katika kila Wilaya kama inavyotakiwa kisheria. Kwa hali hiyo, uchangiaji wa Halmashauri hususan majengo katika kuanzisha Mabaraza mapya utakuwa muhimu sana katika kukamilisha zoezi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kutekeleza jukumu la kusimamia upimaji ardhi nchini na utayarishaji wa ramani za msingi. Upimaji ardhi hutuwezesha kufahamu kipande cha ardhi kilipo, ukubwa wake na mipaka yake. Ramani za msingi ni nyenzo muhimu katika kupanga matumizi ya ardhi na kuandaa mipango ya maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa ramani una hatua kuu nne ambazo ni upigaji picha za anga au za *satellite*, upimaji picha *(photo control)* na uhakiki ardhini, urasimu ramani *(cartography),* na uchapishaji wa ramani. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliahidi kuhuisha ramani za msingi za uwiano wa *unit* moja kwa 2,500 (1:2,500) za miji kumi ya Kanda ya Magharibi.

Kazi hiyo ilifanyika kwa miji 13 ya Nzega, Bukene, Ndala, Igunga, Sikonge, Urambo, Kaliua, Ulyankhulu, Isikizya, Bwanga, Muganza, Buseresere na Katoro. Utayarishaji wa ramani za miji hiyo umekamilika. Utayarishaji wa ramani za Wilaya ya Nzega katika uwiano wa 1:350,000 na eneo la Mkoa wa Kagera katika uwiano wa 1:50,000 nao umekamilika. Wizara iliahidi kuboresha uchapishaji wa ramani kwa kununua mtambo mpya wa kisasa. Mchakato wa ununuzi wa mtambo huo unaendelea na utafungwa na kuanza kutumika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Wizara yangu ya mwaka 2010/2011, tuliahidi kuanza ujenzi wa kituo cha kupokea picha za *satellite (Satellite Receiving Station)* mjini Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mchakato wa ununuzi wa mitambo ya kituo hicho ulianza mwaka 2010/2011, na Wizara itaendelea kutoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa kituo hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuweka mtandao mpya wa alama za msingi za upimaji ardhi *(National Geodetic Control Network)*. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilikamilisha usimikaji na upimaji wa alama za msingi 300 katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Rukwa na Mbeya. Alama hizo zinaiwezesha Wizara kusimika na kupima alama za msingi 600 nchini kote.

Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu itapima mvuto wa dunia *(gravity)* kwa kutumia ndege katika Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Lindi, Iringa, Morogoro, Pwani, Rukwa, Tabora, Dodoma, Dar es salaam, Tanga, Manyara, Arusha, Kigoma na Kagera. Upimaji huo wa mvuto wa dunia utawezesha mahali alama za msingi mpya na 100 za zamani zilizopo juu ya ardhi kujulikana kwa uhakika na kuhusishwa katika mtandao mpya wa upimaji ardhi. Natoa wito kwa wananchi kuelewa kuwa alama hizo siyo za kutwaa ardhi yao, bali ni za kuwezesha upimaji wa ardhi. Nawaomba wananchi waisaidie Serikali kulinda alama hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 rasimu ya Sera ya Upimaji na Ramani ilikamilishwa. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu baada ya kupata maoni ya wadau itawasilisha rasimu hiyo Serikalini (Baraza la Mawaziri), na baada ya kuridhiwa itatayarisha mkakati wa kutekeleza sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, migogoro kuhusu mipaka ndani ya nchi imeendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo. Uzoefu unaonyesha kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya mipaka ni wananchi katika baadhi ya maeneo kutotambua mipaka iliyowekwa rasmi na kutolewa kwenye matangazo ya Serikali. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri

Mkuu - TAMISEMI ilitatua migogoro ya mipaka kati ya Wilaya za Korogwe na Lushoto na kati ya Wilaya ya Bariadi na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itahakiki mipaka baina ya Wilaya za Musoma Vijijini, Serengeti na Bunda.

Napenda kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine kuendelea kufanya Mikutano ya ujirani mwema na kufahamu na kutambua mipaka ya Wilaya zao. Wizara iko tayari kutoa ushirikiano inapohitajika. Aidha, Wizara itasisitiza kupatikana kwa maoni ya wananchi kabla ya mipaka ya Wilaya kubadilishwa ili kupunguza migogoro ambayo imekuwa inajitokeza.

Mheshimiwa Spika, alama za mipaka ya kimataifa ya nchi yetu huhakikiwa na kuimarishwa mara kwa mara kwa kushirikiana na nchi jirani. Katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliimarisha alama za mpaka wenye urefu wa Kilometa 51 kutoka Ziwa Nyasa hadi makutano ya Mto Misinje na Mto Ruvuma. Alama zote 26 zilizowekwa enzi za ukoloni zilikarabatiwa, na alama mpya 16 ziliwekwa katika maeneo ya makazi ya watu na machimbo ya madini.

Aidha, Wizara ilishiriki katika majadiliano na wataalamu wa nchi za Shelisheli, Comoro na Msumbiji kuhusu mipaka ya baharini baina ya nchi zote nne.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine husika ilifanya mazungumzo na Serikali ya Malawi mwezi Septemba, 2010 nchini Malawi kuhusu mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa. Mazungumzo bado yanaendelea katika ngazi ya Watendaji. Hivi sasa Wizara inasubiri upande wa Malawi uitikie mwaliko wa kuja Tanzania kuendelea na mazungumzo hayo.

Vilevile, ilikutana na wawakilishi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC),* kuhusu mpaka kati ya Tanzania na *DRC* katika Ziwa Tanganyika. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kuongoza majadiliano na nchi zote zinazohusika kwa lengo la kukamilisha makubaliano juu ya mipaka yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Burundi, kuna mgogoro uliojitokeza katika Kijiji cha Kasange Wilayani Ngara. Mgogoro huo ulitokana na wananchi wa Burundi kuvuka mpaka na kufanya shughuli za kilimo upande wa Tanzania. Wataalamu wetu na wenzao wa Burundi walifanya mikutano miwili, nchini Tanzania na baadaye Burundi, kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huo.

Katika Mkutano wa mwisho ilikubalika kuwa mkataba wa mwaka 1924 ulioweka mpaka kati ya nchi hizi mbili uheshimiwe. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu itahakiki mpaka kwa kurejea mkataba huo kwa kuishirikisha Serikali ya Burundi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa mipaka ya vijiji, kwa mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya vijiji vipya 300. Hadi kufikia Juni, 2011 vijiji 261 vilipimwa katika Wilaya za Bariadi (vijiji 99), Meatu (29), Maswa (52), Kishapu (46) na Korogwe (35). Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kupima mipaka ya vijiji ambavyo havijapimwa. Wizara itaendelea kupima vijiji kwa kadri vitakavyokuwa vikiongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upimaji wa ardhi chini ya maji, ni jukumu mojawapo la Wizara yangu kupima ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani za ardhi hiyo na kina chake. Ramani hizo hutumika katika kuongoza vyombo vya majini, kubaini maeneo yanayofaa kwa bandari na kufanya utafiti wa aina mbalimbali. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilihakiki vipimo vya alama za rejea za upimaji baharini zilizopo kwenye maeneo ya mwambao wa Tanzania. Kukamilika kwa uhakiki huo kutasaidia kupima kwa usahihi maeneo ya bahari ya nchi yetu ambayo inahusisha maji ya kina kifupi *(internal waters),* maji ya kina kirefu *(territorial sea)* na eneo la Ukanda wa Kiuchumi Baharini *(Exclusive Economic Zone).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza eneo nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini katika mwaka wa 2010/2011 Wizara yangu iliendelea na mchakato wa kukamilisha andiko litakalowasilishwa Umoja wa Mataifa ili nchi yetu iweze kuongezewa eneo la ziada nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini *(Extended Continental Shelf)*. Andiko hilo lilikuwa liwasilishwe kabla ya tarehe 13 Mei, 2011 lakini kutokana na tatizo la uharamia katika Bahari ya Hindi ukusanyaji wa takwimu za kijiolojia baharini kwa ajili ya andiko haukuweza kukamilika kwa wakati. Umoja wa Mataifa ulikubali kuongeza muda wa kuwasilisha andiko hadi tarehe 13 Novemba, 2011. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itakamilisha andiko na kujiandaa kulitetea mbele ya Tume ya Mipaka ya Baharini *(Commission on the Limits of the Continental Shelf).* Nachukua fursa hii kushukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa ushirikiano waliotupa na hivyo kuwezesha kukamilika kwa kazi bila athari yoyote huko baharini. Ninatarajia kuongoza utetezi huo muhimu na nyeti kwenye Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa viwanja na mashamba, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliratibu na kuidhinisha upimaji wa viwanja 26,788 na mashamba 606, ikilinganishwa na lengo la viwanja 50,000 na mashamba 100 Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu inatarajia kuidhinisha upimaji wa viwanja 35,000 na mashamba 800. Ili kurahisisha urejeaji wa kumbukumbu za viwanja vilivyopimwa, Wizara imeandaa ramani moja unganishi (*Cadastral Index Map)* ya eneo la Mkoa wa Dar es Salaam. Ramani ndogo *(survey plans)* 2,321 zenye viwanja 15,188 zimeunganishwa katika ramani hiyo kubwa na kuingizwa kwenye mfumo wa kielektroniki. Kwa mwaka 2011/2012 ramani unganishi zitaandaliwa kwa ajili ya Jiji la Mwanza na Manispaa ya Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kupima Viwanja *(Plot Development Revolving Fund)* unaendelea kuzisaidia Halmashauri mbalimbali nchini kupima viwanja kwa kuzipatia mikopo kwa ajili hiyo. Kuanzia Julai, 2000 hadi Juni, 2011 Wizara ilitoa mikopo ya jumla ya shilingi 1,101,353,518 kwa Halmashauri 42. Jumla ya shilingi 651,758,143 zimerejeshwa na shilingi 642,130,579 bado hazijarejeshwa kati ya fedha zilizorejeshwa, shilingi 267,151,348 zilirejeshwa mwaka 2010/2011 kutoka kwenye Halmashauri 12.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2005, kupitia Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara yangu ilizikopesha Halmashauri saba jumla ya shilingi bilioni 2.62. Halmashauri hizo ni za Manispaa ya Morogoro (shilingi milioni 200); Jiji la Mwanza (shilingi milioni 400); Mji wa Kibaha (shilingi milioni 220); Wilaya ya Bagamoyo (shilingi milioni 400); Manispaa ya Kinondoni (shilingi milioni 600); Manispaa ya Temeke (shilingi milioni 400) na Manispaa ya Ilala (shilingi milioni 400). Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya kuandaa michoro ya mipango miji, kulipa fidia, kupima na kumilikisha viwanja. Hadi Juni, 2011 fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itaweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Halmashauri zilizokopeshwa zinarejesha mikopo hiyo kwa wakati. Tunaendelea kushauriana na Wizara ya Fedha ili kuona uwezekano wa Halmashauri zinazodaiwa kurejesha mikopo hiyo moja kwa moja kutoka kwenye ruzuku zao zitakazotolewa na Wizara hiyo. Natoa wito kwa Halmashauri kutambua kwamba kushindwa kwao kurejesha mikopo hiyo kunaathiri utendaji kazi wa Wizara yangu na kuzinyima haki Halmashauri nyingine ambazo zingekopeshwa kama mikopo ingerejeshwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango ya miji na vijiji, katika kuhakikisha kuwa makazi ya wananchi yanakuwa yenye ustawi na endelevu, Wizara yangu imeendelea kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji nchini kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 na Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipango Miji na Vijiji ya mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uandaaji na utekelezaji wa mipango ya uendelezaji miji, katika kupanga miji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji huandaa mipango ya jumla *(General Planning Schemes)* ya aina mbili kwa ajili ya kusimamia ukuaji na uendelezaji miji. Mipango hiyo ni ya muda mrefu *(Master Plans)* ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji kwa miaka ishirini na ya muda mfupi *(Interim Land Use Plans)* ambayo ni ya miaka kumi. Wizara vilevile huandaa mipango ya uendelezaji upya wa maeneo mbalimbali ya miji

*(Redevelopment Schemes)*, kwa lengo la kuboresha mandhari, miundombinu na huduma katika maeneo husika. Uandaaji wa mipango hiyo hutegemea utayari wa Halmashauri husika na uwezo wa kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ilikamilisha uandaaji wa mpango wa muda mfupi wa mji wa Waso. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi ilianza maandalizi ya mpango wa muda mfupi wa mji wa Misenyi. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Misenyi na Njombe itakamilisha maandalizi ya mipango ya muda mfupi ya miji ya Misenyi na Makambako. Wizara vilevile itaanza maandalizi ya mpango wa muda mfupi wa mji wa Mafia, na itakamilisha mipango kabambe ya mji wa Bagamoyo na majiji ya Dar es Salaam na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Songea ilikamilisha mpango wa uendelezaji upya wa eneo la kati la Manispaa ya Songea na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilianza maandalizi ya kutangaza uendelezaji upya wa eneo la Manzese. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea na uandaaji wa mpango wa uendelezaji upya wa maeneo ya Manzese na Makongo Juu. Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Njombe Wizara, vilevile itaanza maandalizi ya mpango wa uendelezaji upya wa eneo la kati la Mji wa Njombe. Natoa wito kwa wananchi katika maeneo hayo kutoa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa maeneo ya kati ya miji unahitaji moyo wa uvumilivu na uelewa kwa wananchi wanaomiliki maeneo ambayo yatatwaliwa kupitisha miundombinu. Izingatiwe kwamba upangaji wa maeneo hayo na ujenzi wa miundombinu (kwa dhana ya *sites and services)* ni wa gharama kubwa. Kwa hiyo, Halmashauri zenye miradi hiyo zitalazimika kutafuta vyanzo vya ziada vya fedha, vikiwa ni pamoja na mikopo kutoka Hazina au kwenye mabenki, ili kukamilisha miradi hiyo. Hatimaye wenye maeneo hayo watalazimika kulipa kodi mpya ya ardhi ili waendelee kumiliki ardhi yao ambayo itakuwa imeboreshwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 (Kifungu cha 70) Wizara ina mamlaka ya kumtoza mwenye ardhi ada *(betterment fee)* inayotokana na kuboreshwa kwa hali ya eneo lake mjini. Natoa wito kwa wananchi kuelewa jambo hili na kuwa tayari kutoa ushirikiano wao ili uboreshaji wa makazi mijini utekelezwe kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ardhi inapoboreshwa thamani yake inapanda na wenye ardhi hiyo sharti walipie maboresho hayo kama wanataka kuepukana na kero ya ardhi yao kutwaliwa, wao kupewa fidia na viwanja kugawiwa upya. Utaratibu wa wenye ardhi kulipia maboresho utafanyiwa majaribio Makongo Juu, Dar es Salaam ambapo wakazi wa eneo hilo watachangia gharama na kuendelea kumiliki ardhi yao itakayoboreshwa. Endapo mwananchi atashindwa kulipa *betterment fee*, atakuwa na uhuru wa kuuza ardhi yake au kuacha itwaliwe ambapo atalipwa fidia stahiki na kuondoka. Utaratibu huu uliwahi kutekelezwa kwa mafanikio makubwa miaka ya nyuma, kwa mfano wakati wa kupanga na kuboresha eneo la Upanga, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kutenga maeneo ya kutosha kwa ajili ya shughuli za bandari ya Dar es Salaam, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Uendelezaji Upya Eneo la Kurasini ulioanza mwaka 2006. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilipima na kumilikisha viwanja kumi vyenye ukubwa wa ekari 13.7 kwa njia ya zabuni. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kufanya uthamini wa mali na kulipa fidia kwa wakazi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za bandari. Nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa eneo la mradi na maeneo mengine kwa uvumilivu na ushirikiano wao katika utekelezaji wa miradi ya kuendeleza upya maeneo ya mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu urasimishaji wa makazi holela, Wizara iliendelea na kazi ya kurasimisha maeneo yaliyojengwa kiholela kwa kutambua milki za wakazi wa maeneo hayo na kuyaendeleza upya kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Katika mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilitambua milki 7,698, ikapima viwanja 3,763 na kutoa hatimiliki 775 kwa wamiliki. Wizara imeandaa rasimu ya programu ya Taifa ya kurasimisha na kuzuia

makazi holela kwa kushirikiana na baadhi ya Halmashauri. Programu hiyo ni ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuboresha na kuzuia makazi holela mijini. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itakamilisha maandalizi ya programu hiyo na itazisaidia Halmashauri kujiandaa kuitekeleza kwa kutoa mafunzo katika miji ya Sumbawanga, Singida, Mbeya, Tanga, Tabora, Musoma na Iringa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza itaendelea kurasimisha makazi kwa kutambua maeneo na kuyapima. Kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam itahakiki mipango ya urasimishaji katika Kata ya Mbezi ili wananchi waweze kupimiwa maeneo yao kwa kuchangia gharama na kupata hatimiliki. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais kupitia mradi wa MKURABITA na wadau wengine kurasimisha na kuzuia makazi holela nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji miji mipya na vituo vya huduma, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam iliendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa shughuli, watu na magari katikati ya Jiji kwa kuanzisha vituo vya huduma katika maeneo ya pembezoni. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliandaa taratibu za kushirikisha sekta binafsi katika uendelezaji wa Kituo cha Huduma cha Luguruni katika Manispaa ya Kinondoni. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itakamilisha mkataba utakaoiwezesha kampuni binafsi kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya kituo hicho na kushirikiana na Wizara na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni katika uendelezaji wa kituo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke itaanzisha Kituo cha Huduma katika eneo la Kongowe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke iliendelea na maandalizi ya mpango kabambe wa kujenga Mji Mpya wa Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. Eneo hilo linahusisha Kata za Kigamboni, Tungi, Vijibweni, Mjimwema na Kibada, pamoja na Mitaa ya Kizani na Mbwamaji katika Kata ya Somangila. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilianza mchakato wa kuunda mamlaka maalum itakayosimamia uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, itakamilisha maandalizi ya mpango kabambe baada ya kuujadili katika mikutano ya hadhara itakayofanyika kwenye eneo la mpango huo. Wizara pia itakamilisha uundaji wa mamlaka itakayosimamia uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni *(Kigamboni New City Development Authority).* Mamlaka hiyo itaandaa mipango ya kina ya ujenzi wa miundombinu, itafanya uthamini wa mali na kutayarisha maeneo mbadala na makazi kwa ajili ya wananchi watakaolazimika kuhama maeneo yao ya sasa na kwenda mapya lakini ndani ya eneo hilohilo la Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia stahiki kwa wananchi. Aidha, mamlaka hiyo mpya itatumia mbinu za kisasa kupata fedha za kutosha kulipia fidia, kwa mfano kwa kutanganza *Municipal bond* ili wananchi wenye uwezo wachangie gharama hizo kwa kujipatia hisa katika eneo hilo litakalokuwa la kisasa. Nachukua fursa hii kwanza kuwashukuru wananchi wa Kigamboni na viongozi wao wakiongozwa na Mbunge wao Mheshimiwa Dkt. Faustine Engebert Ndugulile, kwa ushirikiano wao mkubwa. *(Makofi)*

Pili, nawaomba waendelee kuwa wavumilivu wakati jitihada zikiendelea kufanyika ili kukamilisha zoezi hili la kwanza na la kipekee katika nchi yetu. Aidha, napenda kuwakumbusha wananchi kuwa ni ukiukaji wa Sheria ya Mipangomiji kujenga katika eneo la Mpango Kabambe wa Mji Mpya Kigamboni bila kuwa na kibali halali cha ujenzi, kwani maendelezo yatakayofanyika kinyume cha sheria hayatatambulika wala kutolewa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi vijijini, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi na kutoa miongozo ya kuandaa mipango ya kina ya maeneo ya makazi katika vijiji. Mkakati wa kutekeleza jukumu hilo unahusisha kuziwezesha Halmashauri za Wilaya na Vijiji kupanga, kutekeleza na kufuatilia mipango yao. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilitafsiri mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya makazi

kwa lugha ya Kiswahili. Vilevile kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Babati na Bariadi ilisimamia utekelezaji wa mipango ya makazi ya vijiji iliyoandaliwa. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mipango iliyokwishaandaliwa ya vitovu vya vijiji na vituo vya biashara. Aidha, itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya mipango hiyo nchini. Kwa kushirikiana na Halmashauri, pia itaandaa mipango ya kina ya makazi ya vijiji vinavyozunguka hifadhi za misitu Mkoani Tabora, kama ilivyoombwa na Mkoa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na uendelezaji wa miji, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI hutoa kanuni na miongozo inayosaidia katika usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji nchini. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliandaa mapendekezo ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007, lengo kuu likiwa ni kukasimu madaraka ya kutoa huduma za mipangomiji kwa maofisa wa Ofisi za Ardhi za Kanda. Aidha, Wizara ilitafsiri Sheria ya Mipangomiji kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itachapisha tafsiri ya Kiswahili ya Sheria ya Mipangomiji na kusambaza kwa wadau mbalimbali. Wizara pia itaendelea na mchakato wa kuandaa kanuni za Sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu la usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji ni la Serikali za Mitaa. Mfumo wa kitaasisi na kiutendaji uliopo haujaweza kudhibiti ujenzi holela ambao unaendelea katika miji mingi bila kujali sheria na taratibu zilizowekwa. Hii imefanya sehemu kubwa ya miji yetu isiwe mahali nadhifu na salama pa kuishi. Kwa hali hiyo, Serikali imedhamiria kurejesha kada ya Askari Ardhi (*Land Rangers*) katika muundo wa Halmashauri zote nchini. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na Manispaa zote Jijini Dar es Salaam itaratibu kazi za Askari Ardhi wa muda ambao wameshaanza kazi Jijini Dar es Salaam ili kudhibiti ujenzi holela. Natoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa askari hawa ambao hakika sasa watawezesha Wizara na Halmashauri kudhibiti ujenzi holela na uvamizi wa maeneo ya umma.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maeneo ya kupumzikia na ya burudani na michezo. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa za Kinondoni na Ilala itaandaa mpango wa kuboresha eneo la Bonde la Msimbazi linalohusisha kata za Buguruni, Hannanasif, Jangwani, Kigogo, Kinondoni, Magomeni, Mchikichini, Tabata, Upanga Magharibi na Mashariki na Vingunguti ili litumike kama bustani ya Jiji *(Central City Park).* Eneo hilo litatumika kwa ajili ya shughuli za michezo, burudani na matumizi mengine ya umma. Natoa wito kwa mamlaka na taasisi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa wananchi wanahamasishwa kuhusu mpango huo kwa manufaa ya wakazi wa sasa na vizazi vijavyo. Aidha, waliovamia eneo hilo au kufanya maendelezo waelewe kuwa hakuna mustakabali katika shughuli zao ndani ya bonde hilo. Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007, mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam wa mwaka 1979 na agizo la Mheshimiwa Rais vinaelekeza kuwa bonde hilo lilindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango ya matumizi ya ardhi ni nyenzo muhimu katika kuendeleza ardhi na rasilimali zake kwa ufanisi, kuzuia migogoro baina ya watumiaji ardhi, kuimarisha milki ya ardhi hususani ya kimila, kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji, kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji na kuongeza ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi kwa watumiaji ardhi ambao wengi wao ni wananchi wa kawaida wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ilitoa mafunzo kuhusu Sheria za Ardhi. Mafunzo hayo yalijumuisha na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi yaliyojumuisha Wizara mbalimbali, Sekretarieti za Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Dodoma, Singida, Kagera, Mwanza, Morogoro, Pwani na Iringa, Halmashauri za Wilaya 45 za Tanzania Bara na wawakilishi kutoka sekta binafsi kumi. Lengo la mafunzo lilikuwa ni kujenga uwezo Kitaifa katika kutekeleza nguzo ya tano ya Kilimo Kwanza na yaliambatana na uhamasishaji juu ya Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Vilevile Wizara kupitia Tume ilisaidia kupatikana kwa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza ambapo jumla ya vijiji 106 katika Mikoa ya Tanga, Iringa, Pwani, Lindi na Morogoro vilifanyiwa ukaguzi na kubaini kuwa vina ardhi ya akiba na maeneo yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, asasi zisizo za Kiserikali na wadau mbalimbali katika kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na wilaya. Tume iliandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 158 katika Halmashauri za Kilosa, Kasulu, Songea, Nanyumbu, Mbarali, Mbozi, Ileje, Kisarawe, Mafia, Muleba, Njombe, Mufindi, Kilolo, Arusha, Kilindi, Handeni, Tanga, Kondoa, Babati, Rufiji, Kilwa, Bariadi na Maswa. Katika vijiji hivyo, maeneo kwa ajili ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yametengwa kwa kushirikisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Tume inakusudia kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi ya vijiji 160 vya mfano itatayarishwa. Tume itashirikiana na wadau wa maendeleo na Halmashauri za Wilaya katika kuandaa mipango hiyo ya vijiji katika Wilaya za Ukerewe, Bunda, Maswa, Musoma Vijijini, Muleba, Misenyi, Rorya, Meatu, Chato, Shinyanga Vijijini, Bukombe, Biharamulo, Ngara, Kishapu, Magu, Sengerema, Misungwi, Serengeti, Chunya, Ileje, Njombe, Mufindi, Mbinga na Songea Vijijini. Baadhi ya Wilaya hizo zimehusishwa ili kuwezesha utekelezaji wa programu ya *Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)* kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara kupitia Tume itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya tisa zitakazochaguliwa kutoka katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma, Kagera na Kigoma na itatoa mafunzo kwa watendaji wa ngazi ya Wilaya kuhusu sheria za ardhi na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Tume itaendelea kuwezesha utekelezaji wa programu za sekta za kilimo, maji na mifugo kwa kushirikiana na Wizara husika. Wizara itaendelea kufanya utafiti kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi, hasa kuhusu vyanzo vya migogoro ya ardhi, uhamiaji mijini kutoka vijijini, ushirikishwaji wa wananchi na matumizi ya ardhi mijini na vijijini. Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya nchini kutoa kipaumbele kwa maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya myumba, Wizara yangu inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta ya nyumba katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya nyumba nchini kunachangia ongezeko la nafasi za ajira, kunainua kipato cha watu na Pato la Taifa na kunaboresha mazingira ya kuishi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuweka mazingira mazuri ya uendelezaji wa sekta ya nyumba, upungufu wa nyumba nchini bado ni mkubwa. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wadau wengine kubuni na kuendeleza mikakati na mipango ya kukabiliana na uhaba huo.

Mheshimiwa Spika, ushirika wa nyumba ni njia muhimu ya kuwawezesha wananchi wenye kipato cha chini kupata nyumba bora kwa gharama nafuu na kuhakikisha uwepo wa usimamizi thabiti wa maeneo ya makazi. Kwa kutambua hilo, uendelezaji wa vyama vya ushirika wa nyumba utakuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara yangu katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Katika mwaka wa 2010/2011 Wizara ilikamilisha mwongozo wa kuanzisha na kusimamia vyama vya ushirika wa nyumba nchini. Kwa mwaka 2011/2012 mwongozo huo utachapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na waajiri kuunga mkono jitihada za Serikali za kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba katika maeneo yao. Vilevile wananchi wanashauriwa kuanzisha vikundi vya ushirika wa nyumba katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza kukusanya takwimu kuhusu hali ya nyumba nchini kwa lengo la kuboresha sera na mikakati ya kuongeza uwekezaji katika sekta ya nyumba. Katika mwaka 2010/2011 ukusanyaji wa takwimu ulifanyika katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Morogoro, Moshi, Tanga, Iringa, Mbeya na Mwanza. Kwa mwaka 2011/2012 ukusanyaji wa takwimu hizo utaendelea katika miji ya Shinyanga, Kibaha, Lindi, Mtwara, Kigoma, Musoma, Tabora, Bukoba, Sumbawanga, Babati, Njombe na Songea. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya

Taifa ya Takwimu, masuala ya nyumba yatapewa kipaumbele katika sensa ya mwaka 2012 (kupitia *housing survey module). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali tangu uanzishwe mwezi Julai, 1992 hadi Juni, 2011 ulitoa mikopo ya nyumba yenye jumla ya shilingi bilioni 7.6 kwa watumishi 1,480. Idadi ya watumishi waliokopeshwa ni ndogo ikilinganishwa na 2,853 walioomba mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 37.2. Mikopo iliyotolewa haikutosheleza mahitaji ya watumishi waliokopeshwa kutokana na mtaji mdogo wa mfuko. Wastani wa mikopo iliyotolewa ilikuwa shilingi milioni tano tu kwa kila mtumishi ikilinganishwa na wastani wa maombi ya shilingi milioni 13. Hadi Juni, 2011 kulikuwa waombaji 387 wa mkopo wanaohitaji jumla ya shilingi bilioni 10.2. Kati ya waombaji hao, 313 ni wapya na 74 wa nyongeza. Mahitaji yao ni makubwa na hayaendani na uwezo wa Mfuko ambao ni shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na taasisi za fedha itabadilisha mfumo wa Mfuko kwa kuweka taratibu mpya kwa kuufanya kuwa wa kuwapatia watumishi wa umma dhamana ili waweze kupata mikopo inayotosheleza mahitaji yao kutoka katika taasisi za fedha badala ya kutegemea mtaji wa Serikali pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Mikopo ya Nyumba ya mwaka 2008, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na wadau ili kuwezesha kupatikana kwa mtaji wa mikopo ya nyumba yenye masharti nafuu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imewezesha kuanzishwa kwa kampuni iitwayo *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)* ambayo itakuwa inatoa mikopo yenye riba nafuu kwa benki za biashara ili nazo ziwakopeshe wananchi kwa masharti nafuu kuliko ilivyo sasa. Hadi Juni, 2011 benki ambazo zilikuwa zimenunua hisa za *TMRC* ni Benki ya Rasilimali Tanzania, *Azania Bancorp, Exim Bank, National Microfinance Bank, CRDB Bank* na *Dar es Salaam Community Bank. TMRC* itaanza kukopesha benki hizo kabla ya mwisho wa mwaka 2011. Ili kulinda maslahi ya umma katika uendeshaji wa *TMRC,* Wizara imeelekeza Shirika la Nyumba la Taifa liwekeze kwenye kampuni hiyo ili liwe na hisa na hivyo kuwa jicho la Serikali katika chombo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya benki zilishaanza kutoa mikopo ya nyumba. Benki hizo ni *Commercial Bank of Africa*, *International Bank of Commerce*, *Azania Bancorp, Stanbic Bank* na *United Bank for Africa.* Ninatoa wito kwa benki nyingine zijitokeze kununua hisa za *TMRC* ili kuongeza mtaji wa kampuni hiyo na zianze kutoa mikopo ya nyumba yenye masharti nafuu ili wananchi walio wengi waweze kumudu kukopa kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu inakusudia kuboresha mazingira ya uendelezaji wa sekta ya nyumba kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu mfumo wa mikopo ya nyumba *(mortgage finance)* na utaratibu wa kumiliki sehemu ya jengo *(condominium housing);* kuandaa taarifa za nyumba nchini, kuhamasisha uundaji wa vyama vya ushirika wa nyumba na kuhamasisha waendelezaji nyumba *(Real Estate Developers)* kuwekeza katika sekta ya nyumba ili kuongeza upatikanaji wa nyumba bora zenye gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo *(NHBRA)* wanalo jukumu la kufanya utafiti kuhusu ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu na kueneza matokeo yake nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu kupitia Wakala iliendelea kufanya utafiti na kubuni mbinu za kujenga nyumba kwa gharama nafuu kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini. Vilevile Wakala waliendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vikundi vya ujenzi vilivyoanzishwa katika vijiji, kata na Wilaya. Aidha, Wakala ilieneza matokeo ya utafiti mbalimbali kama vile matofali yanayofungamana, vigae vya kuezekea vya nyuzi za mkonge na mashine za kutengeneza matofali na za vigae hivyo. Wakala ilitumia vyombo vya habari na maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kueneza matokeo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Utafiti wa Nyumba iliendesha semina za uhamasishaji na mafunzo kwa vitendo kwa wananchi, maafisa maendeleo ya jamii, madiwani, wahandisi na watendaji wengine katika Wilaya za Temeke, Ilala, Kilolo, Mvomero, Kilosa na Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wakala imejizatiti kuandaa mazingira endelevu ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini. Watahamasisha uanzishaji wa vikundi vya ujenzi na vikundi vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi kwa lengo la kuboresha hali ya nyumba zilizopo hasa vijijini. Vikundi hivi vitasaidiwa ili hatimaye vianzishe ushirika wa ujenzi wa nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 semina za uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu zitaendelea kufanyika katika Wilaya za Kilosa, Liwale na Kiteto. Vilevile Wakala itashirikiana na Halmashauri katika kueneza teknolojia za ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wananchi katika Halmashauri za Temeke, Ilala, Kilolo na Mvomero zilizohamasishwa mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala itaendelea kushiriki katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa, na wataboresha maabara yake ya utafiti kwa kufunga vifaa vipya. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini kushirikiana na Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Majengo na kutumia matokeo ya utafiti wake ili kuboresha makazi. Vilevile nashauri kuwa idara za Serikali na taasisi za umma zitoe kipaumbele kwa matumizi ya teknolojia iliyobuniwa na Wakala hii ili kupunguza gharama za usanifu na ujenzi wa nyumba na majengo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* liliandaa mpango mkakati kwa kipindi cha 2010/2011 - 2014/2015. Mpango huo utaliongoza shirika katika juhudi zake za kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake. Katika mwaka 2010/2011 Shirika liliweka muundo mpya wa uongozi, lilirekebisha mikataba kati yake na wadau mbalimbali, lilifuta mikataba 373 ya wapangaji waliokuwa wanapangisha wapangaji wengine kinyume cha taratibu, lilirekebisha miongozo mbalimbali ya Shirika ikiwa ni pamoja na ile ya upangishaji wa nyumba na uwekezaji, lilipunguza mrundikano wa kesi zake mahakamani na lilipunguza madeni sugu ya kodi za pango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 juu ya ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara, Shirika linatarajiwa kujenga nyumba zisizopungua 15,000 katika miaka mitano ijayo. Asilimia 70 ya nyumba zitakazojengwa zitauzwa kwa wananchi. Katika historia ya Shirika, kuanzia lilipoanzishwa mwaka 1962 hadi mwaka 1975 liliweza kujenga nyumba 14,462 ambazo ni sawa na wastani wa nyumba 1,112 kwa mwaka. Katika kipindi hicho Serikali ilichangia asilimia 47 ya gharama zote za ujenzi, wafadhili walichangia asilimia 40 na Shirika lenyewe lilichangia asilimia 13 tu. Kati ya mwaka 1975 na 2010 Shirika lilijenga jumla ya nyumba 2,319, sawa na wastani wa nyumba 66 kwa mwaka. Hivyo basi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo Shirika linatarajia kujenga nyumba kwa kasi kubwa kuliko ilivyowahi kutokea katika historia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba hivi sasa linamiliki majengo 2,310 yenye sehemu za nyumba 16,457. Kati ya sehemu hizo, nyumba za makazi ni 9,600 na za biashara ni 6,857. Lengo la kuuza asilimia 70 ya nyumba zitakazojengwa (sawa na nyumba 10,500) katika kipindi cha miaka mitano ijayo lina maana kwamba Shirika litajenga na kuuza nyumba nyingi zaidi ya zilizopo leo, hivyo kuchangia utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kuwawezesha wananchi wengi zaidi kuwa na makazi bora.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa viwango vya kodi za Shirika la Nyumba kwa wastani ni sawa na asilimia 24 ya bei ya soko. Wakati huo huo Shirika halipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini, lakini tumelipatia changamoto ya kujenga nyumba nyingi na kuboresha nyumba zake zilizopo kwa kuzifanyia matengenezo. Kwa hali hii viwango vya kodi ya pango la nyumba za Shirika havina budi kuongezwa ili kuliwezesha kutekeleza majukumu hayo makubwa. Kwa sasa Shirika linahudumia asilimia 0.45 tu ya wapangaji wote nchini na Serikali ingependa liwahudumie Watanzania wengi zaidi. Katika mipango yake Shirika limejiwekea lengo la kuongeza viwango vya kodi kwa awamu mpaka kufikia asilimia 85 ya viwango katika soko ifikapo mwaka 2015. Ninatoa wito kwa wapangaji wote wa Shirika la Nyumba la Taifa kuelewa kwamba ongezeko la kodi ya pango

haliepukiki ikizingatiwa kwamba Shirika lina jukumu zito la kuwahudumia Watanzania wengi zaidi. Hata hivyo, napenda kuwahakikishia kwamba viwango vya kodi vitaendelea kuwa chini ya viwango vya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Shirika lilijipanga kutekeleza miradi mikubwa kwa kuongeza akiba yake ya ardhi kwa ekari 7,967 katika miji ya Dodoma, Musoma, Arusha na Morogoro. Vilevile Shirika lilifanya maandalizi ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara zipatazo 4,000 katika Wilaya mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Shirika liliendelea na ujenzi wa nyumba za makazi Arusha (nyumba 52) na Dar es Salaam (34), pamoja na jengo la biashara mjini Kigoma. Kadhalika Shirika liliendelea na utekelezaji wa miradi ya ubia 75 yenye thamani ya shilingi bilioni 300 kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mchango mkubwa wa Shirika katika miradi hiyo ni ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Shirika lilikusanya shilingi bilioni 41.9 ambayo ni sawa na asilimia 108 ya lengo la mwaka huo. Ongezeko la makusanyo lilitokana na juhudi kubwa zilizofanyika za kukusanya malimbikizo ya kodi kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa Na. 2 ya 1990 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 ambazo zinalipa Shirika uwezo wa kufanya shughuli zake kwa misingi ya biashara. Kwa mwaka 2011/2012 Shirika limeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 43.1 kwa kuendelea kutekeleza mikakati ya kukusanya malimbikizo ya madeni na mapato yanayotokana na kodi za pango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Shirika liliendelea kutekeleza mkakati wa kutenga asilimia 20 ya Bajeti kwa ajili ya kuyafanyia matengenezo majengo yake 2,392. Katika kipindi husika Shirika lilitumia shilingi bilioni 5.06 kwa ajili hiyo. Kwa mwaka 2011/2012 Shirika limetenga shilingi bilioni 6.8 kwa ajili ya matengenezo ya majengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Shirika lilianza mazungumzo na benki 10 kwa lengo la kupata mikopo ya ujenzi wa nyumba na kuwapatia wanunuzi mikopo ya nyumba. Ni matarajio ya Wizara kuwa wananchi wataweza kupata mikopo kutoka kwenye benki hizo kwa ajili ya ununuzi wa nyumba zitakazojengwa na Shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Shirika linatarajia kuanza ujenzi wa nyumba za makazi 2,721 na majengo saba ya biashara katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tabora, Mbeya na Morogoro. Miradi hii itagharimu shilingi bilioni 311.5 na Shirika litatumia shilingi bilioni 164.1 kwa mwaka 2011/2012. Vilevile Shirika litaanza ujenzi wa nyumba nyingine 160 za makazi katika baadhi ya miji mikuu ya Mikoa na Wilaya mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za kisheria, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imefanikiwa kuwapata watumishi waandamizi wa kuendesha shughuli za Kitengo cha Huduma za Kisheria *(Legal Services Unit)* za kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara na Taasisi zake, kushiriki katika majadiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali wa sekta ya ardhi na kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kufuatilia mashauri yanayoihusu Wizara Mahakamani. Natoa shukrani kwa msaada na ushirikiano uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuiwezesha Wizara kuanzisha kitengo hiki.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano Serikalini, Wizara yangu iliendelea kuimarisha Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ambacho kina jukumu la kuwasiliana na wananchi na wadau na kuwapa habari kuhusu shughuli za Wizara. Katika mwaka 2010/2011 elimu kwa umma juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara pamoja na sera, mikakati na sheria za sekta ya ardhi ilitolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na mikutano ya wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kuimarisha Kitengo hiki kwa kuajiri wataalam wa mawasiliano ya umma na kuongeza vitendea kazi. Wizara itaboresha mkakati wake wa mawasiliano na kuzindua mkataba wa huduma kwa mteja. Mabadiliko ya mkakati yatalenga kujumuisha ipasavyo mipango muhimu inayotekelezwa na Wizara, ikiwa ni pamoja na mpango wa uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na wa kuzuia uvamizi wa maeneo ya wazi mijini. Elimu kwa umma itatolewa kupitia vyombo vya habari na majukwaa

mbalimbali, kwa mfano maonesho, maadhimisho ya Kkitaifa na mitandao ya jamii *(social media).* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za utawala na rasilimali watu, utendaji kazi katika Wizara uliendelea kuboreshwa kwa kusimamia rasilimali zilizopo. Kwa kutambua umuhimu wa rasilimali watu, Wizara iliendelea kutoa mafunzo, kuboresha mazingira ya kazi, kuwapatia watumishi stahili zinazoendana na ajira zao na kusisitiza utawala bora, kusimamia nidhamu ya watumishi na kupiga vita rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea kutekeleza mpango wa uendelezaji rasilimali watu kwa kubaini mahitaji halisi ya watumishi na sifa wanazotakiwa kuwa nazo katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara. Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 262 na kuwathibitisha kazini watumishi 76. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Wizara waliendelea kupata mafunzo ya aina mbalimbali. Katika mwaka 2010/2011 jumla ya watumishi 100 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu inatarajia kuwapatia mafunzo watumishi wapatao 110. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya kutoa huduma bora kwa mteja, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo mahususi kwa watumishi. Katika mwaka 2010/2011 waajiriwa wapya 84 walipata mafunzo ya awali kuhusu majukumu yao. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wateja kwa kuanzisha kituo maalum cha kuwahudumia *(Customer Service Centre)* kwenye makao makuu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuelimisha watumishi juu ya namna ya kujihadhari na UKIMWI. Watumishi 19 waliopima na kutoa taarifa kwa uongozi juu ya hali ya afya zao waliendelea kupatiwa huduma za dawa na lishe kila mwezi. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya kwa hiari na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Ardhi, Wizara yangu inasimamia Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya stashahada *(Ordinary Diploma)* katika fani za urasimu ramani na upimaji ardhi na Cheti katika fani za umiliki ardhi, uthamini na uchapaji ramani. Wataalam wanaosomea fani hizi wanahitajika kwa wingi katika Serikali Kuu, Taasisi za Umma na Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2010/2011 walihitimu wanafunzi 130. Kati yao 50 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na 80 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea kutekeleza mradi wa upanuzi wa Chuo cha Ardhi Tabora kwa kujenga mabweni, madarasa na maktaba ili kuongeza udahili wa wanafunzi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huo unaendelea. Ujenzi wa bweni unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2011. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea na ujenzi wa maktaba na ukarabati wa madarasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani, katika muda mfupi niliotekeleza majukumu yangu katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nimeona jinsi Wizara ilivyo na majukumu mazito yanayogusa nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa za nchi yetu. Ni mategemeo yangu kwamba Bunge litaendelea kuwa na mtizamo chanya na kuipa kipaumbele Wizara hii na sekta ya ardhi kwa ujumla kulingana na mchango wake katika kufanikisha juhudi za kuleta maendeleo ya haraka katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya ardhi katika mwaka 2010/2011 ni matokeo ya ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za Kiserikali, Mashirika ya Kidini na taasisi za fedha za Kimataifa. Wadau hao ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ);* Benki ya Dunia na Serikali za Denmark, Sweden, Uholanzi na Uingereza kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara *(Business Environment Strengthening for Tanzania);* Serikali za Finland na Norway na Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa *(UN-HABITAT).* *(Makofi)*

Kuhusu msaada wa *UN-HABITAT,* sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Kofi Annan, kwa kunipendekeza na nikachaguliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuwa Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Makazi Duniani *(UN-HABITAT)* kwa miaka kumi (Septemba, 2000 hadi Agosti, 2010). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho nilifanikiwa kujenga ushirikiano wa karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwezesha miradi kadhaa nchini kutekelezwa ambayo Shirika hilo linaendelea kuifadhili. Ushirikiano huo umezaa matunda mengi katika sekta mbalimbali. Kwa mfano, mchakato wa kuandaa Sheria ya Mikopo ya Nyumba na Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo ambazo zilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2008, ulitokana na ushauri wa *UN-HABITAT.* Sina budi kutambua ushirikiano mkubwa nilioupata katika kutekeleza majukumu yangu kama Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo kutoka kwa Mawaziri walionitangulia ambao walikuwa ni viongozi wa ujumbe wa Tanzania katika Baraza la *UN-HABITAT. (Makofi)*

Shukrani za kipekee nazitoa kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi na Mbunge wa Chato ambaye mwaka 2006 akiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kongamano la Maendeleo ya Miji la Umoja wa Mataifa *(World Urban Forum II)* lililofanyika Vancouver, Canada ambalo nililiandaa. Vilevile namshukuru Mheshimiwa John Chiligati, Naibu Katibu Mkuu, Tanzania Bara wa Chama cha Mapinduzi na Mbunge wa Manyoni ambaye alinisaidia sana kutekeleza majukumu yangu ya Kimataifa. Namshukuru kwa jinsi alivyonikaribisha, niliporejea nyumbani, kwa upendo na akanikabidhi Wizara na kwa jinsi anavyoendelea kunishauri katika utekelezaji wa majukumu yangu. Hakika aliniachia msingi mzuri ambao nitauendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa na Naibu Katibu Mkuu Bibi Maria Bilia kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi kifupi tangu niteuliwe kuwa Waziri wa Wizara hii. *(Makofi)*

Nawashukuru vilevile Wakuu wa Idara na Vitengo katika Wizara, viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa sekta ya ardhi kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu. Naomba waendelee kutekeleza majukumu yetu kwa kujielekeza katika kuchangia ipasavyo kuboresha mazingira ya kuondoa umaskini na kuendeleza biashara na uwekezaji. *(Makofi)*

Natambua kuwa Wizara yangu haina nyenzo na rasilimali zote tunazohitaji, lakini hata kwa rasilimali tulizonazo, zikisimamiwa kwa uangalifu tukapata thamani inayowiana na rasilimali hizo *(value for money),* zitazaa matunda makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu imeazimia kutekeleza mipango ya kuendeleza ardhi, nyumba na makazi ili kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika hotuba hii. Aidha, itahakikisha kuwa upangaji na ugawaji wa ardhi, upangaji wa miji unaendelea kwa kuzingatia sheria zilizopo kwa usimamizi wa karibu. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri tutawezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya wawekezaji kwa utaratibu mpya wa wananchi kutumia ardhi kama mtaji *(land for equity).* Hali kadhalika kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine Wizara itaendelea kutafuta ufumbuzi wa migogoro sugu ya ardhi na tutajielekeza katika kuziba mianya inayosababisha migogoro hiyo ili isiendelee kutokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo Wizara yangu imejipanga kuhakiki, kupanga matumizi ya ardhi, kupima, kusajili na kutoa hati katika maeneo hayo ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki na hivyo kuondoa migogoro kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote kwa lengo la kuwaondolea wananchi umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012 Wizara yangu imejipanga kutekeleza majukumu yake iliyojiwekea ili kufikia malengo ya MKUKUTA II, Dira ya Taifa ya 2025 na

Malengo ya Milenia. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

(i) Mapato - Mapato ya Serikali shilingi 20,645,006,000;

(ii) Matumizi ya Kawaida - Matumizi ya Mishahara shilingi 7,351,409,000; Matumizi Mengineyo *(OC)* shilingi 18,353,352,000; Jumla shilingi 25,884,761,000;

(iii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo - Matumizi ya Maendeleo Fedha za Ndani shilingi 6,000,000,000; Fedha za Nje shilingi 16,010,437,000; Jumla shilingi 22,010,437,000.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 47,895,198,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara yenye anuani ya *www.ardhi.go.tz*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Wizara hii, wakati natangaza wageni nilipitiwa kwa bahati mbaya wageni wa Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Halima Mdee nimewaruka kwa bahati mbaya. *(Makofi)*

Hawa ni wageni wake kutoka jimboni kwake Jimbo la Kawe yupo Ester Samanya, tena wamekaa kwenye *Speakers Gallery I am sorry*. Yupo Deusdedit Mtiro, Magesa Kazinyingi, Powell Mfinanga, Martha Charles, Milka Bulaza na Brighton Babile. *(Makofi)*

Halafu juzi tulikuwa na msanii mwingine wa shughuli za daladala leo tuna msanii mwingine wa nyimbo za Injili anaitwa Bibi Beatrice Muhone. Huyu ni mwimbaji wa Nyimbo wa Injili yupo hapa Dodoma kwa ajili ya kuzindua kanda yake. Kwa hiyo, kama ni hapa Dodoma basi mkisikia huko basi mwende tu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA – K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, afya njema na kuniwezesha kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Kabla sijawasilisha maoni ya Kamati naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sitawashukuru wapiga kura wangu wote wa Mkoa wa Mbeya na hasa Jumuiya ya Umoja wa CCM (UWT) wa Mkoa wa Mbeya kwa kunichagua kwa kishindo kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka mitano na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge. Ninawahakikishia nipo pamoja nao na pindi shughuli za Bunge zitakapomalizika nitarudi kuungana nao ili tuendelee kushirikiana kwa pamoja katika kuendelea kuuletea Mkoa wetu wa Mbeya maendeleo. Nawaahidi kamwe sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa familia yangu yote na hasa watoto wangu wapendwa Joseph na David. Ninawashukuru kwa uvumilivu

wao kwangu hasa ninapokuwa mbali nao kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Bunge na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza jukumu hilo la Kkikanuni tarehe 1 hadi 2 Juni, 2011, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikutana na watendaji wakuu wa Wizara wakiongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka katika ukumbi wa mikutano uliopo Ofisi ya Makamu wa Rais, jijini Dar es Salaam. Katika vikao hivyo, Kamati ilipitia yafuatayo:-

Kwanza taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012; pili, taarifa ya utekelezaji wa kazi za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* katika mwaka wa fedha 2010/2011 na Mpango wa Kazi za Shirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012; tatu, taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo katika mwaka wa fedha 2010/2011 na Mpango wa Kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012; nne, taarifa ya utekelezaji wa kKazi za Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Mpango wa Kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012; na tano, mpango wa kuendeleza eneo la Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri pia aliieleza Kamati kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina idara saba na vitengo tisa, Idara hizo ni Maendeleo ya Huduma ya Ardhi, Upimaji wa Ramani, Maendeleo ya Nyumba, Sera na Mipango, Utawala na Utumishi, Mifumo ya Habari na Mawasiliano na Idara ya Upangaji wa Miji na Vijiji. Aidha, Wizara inazo Taasisi na Mashirika yanayofanya shughuli zake chini ya uangalizi wa jumla wa Wizara ambayo ni Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Wakala wa Taifa wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA),* Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo cha Ardhi Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa majadiliano ya Bajeti kwa mwaka 2010/2011 katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Kamati ilitoa maagizo 15 kwa ajili ya utekelezaji, hasa katika maeneo yanayohusu muda wa upatikanaji wa hati miliki, suala la uwekaji mipaka kwenye maeneo ya Bahari na Ziwa, ukusanyaji wa mapato katika halmashauri na ulipaji kodi kwa wakati kutoka kwa wapangaji wa Shirika la Nyumba na kadhalika. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhika na baadhi ya utekelezaji wa maagizo hayo. Aidha, kwa upande ambao unaonekana haujatekelezwa vizuri, Kamati imeshauri ipasavyo na kutoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na kazi zilizopangwa kutekelezwa fedha zinazoombwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zimegawanywa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Hivyo basi, kiasi cha shilingi 47,895,198,000/= zinaombwa, kati ya fedha hizo, Wizara inakusudia itakusanya shilingi 20,645,006,000/= kama Mapato ya Serikali, katika Matumizi ya Kawaida Wizara inakusudia kutumia shilingi 25,884,761,000/= na katika Miradi ya Maendeleo Wizara imepanga kutumia jumla ya shilingi 22,010,437,000/= kati ya hizo fedha za ndani ya nchi ni shilingi 6,000,000,000/= na fedha za nje ya nchi ni shilingi 16,010,437,000/=. Fedha hizi zinaombwa kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza pamoja na kazi nyingine zikiwemo shughuli za msingi zifuatazo:-

Kwanza Idara ya Utawala wa Ardhi imepanga kuratibu uanzishwaji wa mfuko wa fidia ya ardhi *(The land Compersation Fund);* Pili, Kitengo cha Usajili wa Hati kimepanga kukamilisha marekebisho ya Sheria za Usajili wa Hati; (Sura ya 334), Sheria ya Usajili Nyaraka (Sura ya 117) na Sheria ya Usajili wa Mali zinazohamishika (Sura 210) ili ziendane na hali ya sasa ya usajili wa nyaraka hizo; tatu, Kitengo cha Uthamini wa Mali kimepanga kukamilisha uandaaji wa sheria ya uthamini; nne, Idara ya Upimaji na Ramani imepanga kutambua na kupima ardhi kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje; na tano, Kitengo cha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kimepanga kuanzisha na kuendeleza Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za Ngorongoro, Manyoni, Karagwe na Mkoa mpya wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, Idara ya Mipango Miji na vijiji imepanga kuratibu uanzishaji wa Askari Ardhi *(Land Rangers)* wa majaribio ambao wameshaanza kazi katika jiji la Dar es Salaam ili kudhibiti ujenzi holela mijini na kuandaa mamlaka itakayosimamia ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni; kuandaa na kutekeleza mipango ya kina ya miundombinu; saba, Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi imepanga kutekeleza mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi kwa kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ushirikishwaji katika vijiji 100 vya mfano; nane, Idara ya Nyumba imepanga kusimamia ukusanyaji wa marejesho ya mikopo ya nyumba kutoka kwa watumishi wa Serikali walionufaika na Mfuko wa Mikopo ya Nyumba; na kumi, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo umepanga kuandaa mazingira endelevu ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa kutumia vifaa vipatikanavyo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupitia mapitio ya Bajeti Fungu 48 kifungu kwa kifungu na mwelekeo wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, ardhi ni mtaji, ikiwa mwananchi anamiliki ardhi inayotambulika, iliyopimwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria, ardhi hiyo itamsaidia mwananchi huyu kufanya shughuli za maendeleo kama kilimo, malisho, ujenzi wa nyumba na kadhalika na kwa kadri mwananchi huyu anavyoendeleza ardhi hii kwa shughuli hizo mwananchi huyu anaongeza thamani ya ardhi anayoimiliki na kupata fursa ya kuitumia ardhi hiyo kama rehani ya kupata mtaji wa maendeleo katika vyombo na taasisi za fedha kama mabenki. Hivyo basi, sekta ya ardhi na ujenzi wa nyumba za makazi na biashara ni sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii katika mataifa mbalimbali kwa kuwa chachu ya sekta zingine za uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Kamati inaitaka Serikali itambue sekta ya ardhi kama sekta mtambuka ambayo kama haitakuwa inapewa fedha za kutosha kila mwaka kama ilivyo sasa. Sekta ya ardhi itakwamisha mipango ya sekta nyingine na kukwamisha maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kwa mfano, kama ardhi haikupimwa na kutengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo itaikwamisha Wizara ya Kilimo kutekeleza sera ya Kilimo Kwanza, vilevile kama ardhi haikupimwa na kutenga maeneo ya uwekezaji itakwamisha sekta ya viwanda na biashara ambayo inahitaji kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza nchini kwa kujenga viwanda na maeneo ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ardhi isipopimwa, isiposimamiwa vizuri na kupangiwa matumizi bora inaweza kusababisha migogoro na migongano. Migogoro hii inaweza kusababisha nchi isitawalike/isitawaliwe na kuleta maafa makubwa katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Wizara na Taasisi za Serikali zina namna ya kujiongezea mapato yanayotokana na shughuli zake za maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 20,645,006,000/=. Mapato hayo yatatokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo ada za ardhi, ada inayotozwa na Vyuo vya Ardhi, ada za upimaji wa ardhi, ada za uthamini, ada za usajili wa hati, ada zinazotozwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na ada zinginezo zinazotozwa katika sekta ya ardhi. Pesa inayopatikana inapelekwa Hazina na kisha sehemu ya fedha hizo inarudishwa Wizarani kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati inapitia Bajeti ya Wizara hii iligundua kwamba Serikali kupitia Hazina imepanga kuipatia Wizara kiasi cha asilimia 71 ya fedha hizo ambazo Wizara imekusudia kukusanya ikiwa ni pungufu ya asilimia tano ya *rentation* ya mwaka 2010/2011 ambayo Wizara hii ilipata asilimia 76. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *rentention* ni fedha za maduhuli ambazo Wizara imejipangia yenyewe kukusanya kwa ajili ya shughuli za maendeleo, Kamati inashauri Serikali iweze kuipatia Wizara hii *rentantion* ya asilimia 100 ili Wizara iweze kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Kwanza kuongeza gawio kwa asilimia 10 na kufika aslimia 30 badala ya gawio la sasa la asilimia 20 zinazotolewa kwenye Halmashauri ambazo zinafanya kazi ya kukusanya tozo ya ada mbalimbali kwa niaba ya Wizara. Fedha hizi zitasaidia kupunguza matatizo mengi yanayozikabili

ofisi za ardhi zilizopo kwenye Halmashauri. Aidha, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutoa ruzuku katika Idara ya Ardhi kwenye ngazi ya Halmashauri kama inavyotoa ruzuku kwa sekta ya elimu, afya na kadhalika. katika ngazi ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pili, Wizara itaweza kutoa mafunzo kwa Wapimaji wa Ardhi *(Surveyers)* na Wapanga Miji *(City Planners).* Mafunzo haya yatasaidia utumiaji wa vifaa vya kisasa vya upimaji na ramani. Utaalamu huu utasaidia kupunguza tatizo la ujenzi holela na ulazima wa wananchi kujenga maeneo yasiyopimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio la Arusha lilisema na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere alituasa kuwa ili tuendelee tunaitaji vitu vinne, ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Mwalimu alikuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa kwa dunia ya leo mtaji pia ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya nchi na watu wake. Mwalimu hakuishia hapo akatumia uzoefu wa nchi zingine ambazo raia wake ni maskini kwa vile tu ardhi yote inahodhiwa na mamwinyi na makabaila wachache ndio maana Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliona mbali sana tangu mwanzo wa Utaifa wetu na hata kabla ya Uhuru wetu. Akasema ardhi ya Tanzania ni ya Watanzania wote na atamilikishwa kwa muda maalum kila mwenye uwezo wa kutumia ardhi hiyo kwa manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi, Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha inafanya upembuzi yakinifu ili kuweza kubaini uwezo wa wawekezaji na kufanya utafiti kabla ya kummilikisha ardhi mwekezaji asiye na uwezo. Utaratibu huu utapunguza tatizo la kuwamilikisha maeneo wawekezaji wasio na uwezo wa kuyamiliki ambao wamekuwa wakishindwa kuendeleza maeneo waliyopewa badala yake kuwakodisha wananchi, mfano eneo la Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ndio rasilimali kuu kuliko zote katika uchumi wa nchi yetu. Nchi yetu imebarikiwa na Mwenyezi Mungu kwa kupewa ardhi ya kutosha, tena sehemu kubwa yenye rutuba. Uwekezaji kwenye sekta nyingine kama madini, viwanda, utalii, biashara miundombinu na kadhalika unaweza kuwanyanyua wachache wakaondokana na umaskini kwa ukubwa wa ardhi tuliyonayo tunaweza kuigeuza ardhi kuwa mtaji na kutuletea maendeleo kwa mtu binafsi na Taifa kwa ujumla. Ardhi pekee ndio yenye uwezo wa kumnyanyua kila Mtanzania aachane na umaskini. *(Makofi)*

Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara ianzishe kitengo cha elimu kwa umma na Wizara ikipatie kitengo hiki fedha za kutosha ili kiweze kuwa na vipindi maalum redioni na kwenye luninga vyenye lengo la kuwaelimisha wananchi ili watambue umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria na kuendeleza ardhi wanayomiliki kama rasilimali ya kuwaondolea umaskini na kuwaletea maendeleo. Lakini elimu hii lazima itolewe kwa uangalifu ili watu wasiweke ardhi au nyumba zao rehani kwa mambo yasiyofanyiwa uchambuzi wa kutosha, maana nia ni kuwawezesha kupata mikopo, nia ya Serikali si kwamba wananchi wapoteze ardhi yao au nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mfumo madhubuti, rahisi na wazi wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya ardhi kulingana na Sheria ya Ardhi (1999), ambapo ardhi vijijini inasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii inatoa utarartibu wa Halmashauri ya Kijiji kupata Cheti cha Ardhi ya Kijiji ili kuweza kutoa usajili wa Hatimiliki za Kimila kwa watu wenye haki za kumiliki ardhi katika maeneo ya kijiji. Wizara kupitia Tume ya Matumizi ya Ardhi imeweza kupima baadhi ya vijiji, baadhi ya vijiji vimepewa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Masijala ya Ardhi za Wilaya na Vijiji zimejengwa kwenye baadhi za maeneo ya Wilaya na Vijiji. *(Makofi)*

Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ishirikiane na Chuo cha Utumishi wa Umma (Magogoni), kwa kuandaa uratibu wa kuwaelimisha Maafisa Ardhi wa Wilaya namna bora ya utunzaji wa majalada katika masjala zote za ardhi. Vilevile masjala haya ya ardhi yatumie teknolojia ya kisasa ya kompyuta ambapo kumbukumbu ya mambo yote muhimu kuhusu mmiliki wa eneo, na ardhi yenyewe yaweze kuhifadhiwa sehemu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zinazoendelea zinategemea zaidi sekta ya nyumba katika kukuza uchumi, mchango wa sekta ya nyumba kwenye Pato la Taifa kwa nchi hizo ni kati ya asilimia 50 hadi 60 kwa mwaka. Nchini Tanzania, sekta ya nyumba huchangia chini ya asilimia 1.0 kwenye Pato la Taifa. Sekta hii ikisimamiwa vizuri itasaidia Serikali kutengeneza fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa watu wenye ujuzi na wasio na ujuzi; ongezeko katika makusanyo ya kodi mbalimbali kama vile Kodi za Ongezeko la Thamani *(VAT),* kodi za majengo, kodi za ardhi, kodi za mapato na kadhalika. Itaongeza kodi kutokana na kuwa na miji iliyopangika ambayo itarahisisha watoza ushuru kufika sehemu moja hadi nyingine kwa urahisi na kuwatambua walipa kodi na pia ukuaji wa sekta ya fedha kutokana na ongezeko la kipato, ongezeko la fidia na hata ukopeshaji kwa riba ndogo pamoja na kukua kwa sekta ya bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa sekta hii itatumika ipasavyo itaongeza vyanzo vipya vya mapato ya Serikali badala ya kuwa na vyanzo vilevile vya kodi za Selikali kama kupandisha bei za vitu kama bia, soda na sigara kila mwaka. Kutokana na umuhimu huu Kamati inashauri Serikali iitambue sekta ya nyumba kama moja ya sekta za kipaumbele cha Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mpango kabambe wa uendelezaji wa eneo la Mji Mpya wa Kigamboni. Kamati inaunga mkono mpango huu wa Serikali na kushauri kuwa Serikali ifanye tathimini ya uthamini wa mali za wananchi watakaohama ili kupisha mpango wa uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni, malipo ya fidia yatakayotokana na uthamini huo yaendane na viwango vya soko vya thamani ya ardhi, nyumba na mazao, kuwepo na uwazi wa kuhakikisha wananchi waishio eneo la mpango wanabaki kwenye eneo hilo na ikiwa Serikali ina nia ya dhati ya kutekeleza mradi huu, itenge fedha za kutosha ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa wakati. Ili mradi huu ukamilike utagharimu shilingi bilioni 13, wakati Wizara imetengewa shilingi bilioni tatu tu kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na majukumu mengine, Shirika hili linajukumu la kujenga nyumba au majengo kwa ajili ya kupangisha au/na kuuza kwa gharama nafuu. Jukumu hili kimsingi linalenga kumpunguzia mwananchi wa kipato cha chini na cha kati gharama kubwa za ujenzi ikiwa atajenga mtu binafsi. Vilevile jukumu hili litasaidia kuzuia ujenzi wa makazi holela katika maeneo mengi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Katika kutekeleza kwa vitendo jukumu hili Shirika la Nyumba la Taifa limeomba maeneo tofauti kutoka Halmashauri za Miji/Manispaa kwa mfano, Shirika lina mradi wa nyumba 290 zinazotegemewa kujengwa eneo la Medeli katika Manispaa ya Dodoma. Katika mradi huu na mingine mingi ya aina hii pamoja na kuwa Halmashauri za Miji/Manispaa zinatoa maeneo ya miradi ya aina hii, mamlaka zinazotoa huduma muhimu kama maji, umeme na miundombinu kama barabara, hazijafikisha huduma hizo kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Shirika limelazimika kugharamia huduma hizo, ambapo gharama hizi mara nyingi hubebwa na wanunuzi/wapangishaji, hivyo kuzifanya bei za nyumba za Shirika kuwa juu na hivyo Shirika kushindwa kutimiza azma yake ya kujenga nyumba za kuuza au kupangisha kwa gharama nafuu. Kamati inaishauri Serikali kuzingatia umuhimu wa *sites and services.* Aidha, Kamati inawakumbusha watoa huduma wengine kama *TANESCO,* Mamlaka za Maji na barabara kutimiza wajibu wao kwa kuhakikisha sehemu kubwa ya ardhi inawekewa huduma muhimu kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kutouza nyumba zilizopo kwenye maeneo yenye hadhi *(prime areas)* kama Upanga, Oysterbay na kadhalika. Kamati inaunga mkono azma hii ya Serikali na Shirika la Nyumba la Taifa ya kutaka kuboresha na kuyaendeleza maeneo hayo kwa madhumuni ya kutumia rasilimali ardhi vizuri na kwa manufaa ya Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango huu utasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa nyumba ambapo upungufu wa sasa wa nyumba unakadiriwa kufikia nyumba 200,000 kwa mwaka. Ikiwa mpango huu utatekelezwa kikamilifu utapunguza ukubwa wa tatizo hilo hasa ikizingatiwa kuwa

sehemu ambayo inaishi familia moja kwa sasa, ikiendelezwa vizuri zinaweza kuishi familia kati ya 100 hadi 150. Kamati inapenda kusisitiza kuwa baada ya maeneo hayo kuendelezwa, ni vyema kipaumbele cha kuuziwa au kupangishwa kikatolewa kwanza kwa watu/familia zilizokuwa zinaishi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho katika shukrani zangu, lakini kwa umuhimu mkubwa, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanakamati wenzangu napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Naibu Waziri Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Katibu Mkuu Ndugu Patrick Rutabanzibwa pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Taasisi na Mashirika yanayofanya kazi chini ya Wizara hii kwa maelezo ya ufafanuzi walioutoa mbele ya Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa ushirikiano wao walionipa wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha taarifa hii ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ali khamis Seif, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali na mimi mwenyewe Dkt. Mary Mwanjelwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Katibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru wewe kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wa Jimbo la Kawe kwa imani yao kwangu, makamanda wote (vijana, wazee na akina mama wa vyama vyote) walioshiriki katika harakati zangu zote za Kampeni na hatimaye kukesha na mgombea wao, Shule ya Msingi Oysterbay kulinda ushindi wetu. Mungu pekee ndiye anayejua shukrani yangu kwao! Ahadi yangu kwao ni kuwatumikia kwa uwezo wangu wote kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa aliyekuwa Mgombea Urais kupitia CHADEMA, Dkt. Wilbroad Peter Slaa. Hakika Wabunge wengi tuliofanikiwa kushinda, sehemu ya ushindi wetu ilipatikana kutokana na utumishi wake uliotukuka katika Taifa hili! Mungu akupe uhai,naamini ipo siku tutaifikia Nchi ya Ahadi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii. Shukrani pia ziende kwa wasaidizi wa Kiongozi wa Kambi, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Naibu Kiongozi wa Kambi na Mheshimiwa Tundu Lissu, Mnadhimu wa Kambi kwa kutuongoza vyema katika shughuli hii ngumu ya kuwatetea wanyonge. Shukrani pia ziwafikie Wabunge wenzangu wote wa Kambi kwa ushirikiano wao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi pia kuishukuru sana familia yangu yote, kwa upendo wao wa dhati na kwa upekee naishukuru timu yangu ya kampeni, wazazi wangu Profesa James Salehe Mdee na Theresia Kisenga Ngowi kwa upendo wao na kwa upekee nimshukuru kaka yangu Joseph James Mdee, ambaye alikuwa sambaba na mimi na timu yangu ya kampeni iliyoongozwa na uongozi wa Jimbo la Kawe usiku na mchana mpaka kikaeleweka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kaka yangu na rafiki yangu mkubwa Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini. Kwa yeyote anayemuona Halima Mdee na mafanikio yake, afahamu kwamba safari yangu ya mafanikio ya kisiasa yalianzia mbali sana! Na katika safari hii, tokea hatua za awali kabisa, kaka yangu huyu alikuwa mhimili mkubwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ya Tanzania ina ukubwa wa kilomita za mraba 942,600 sawa na hekta milioni 94.26, kati yake kilomita za mraba 888,200 sawa na hekta milioni 88.82 ni eneo la nchi kavu. Ili ardhi hii iwe na maana katika kuleta maendeleo ni lazima kila kipande kitambuliwe, kipimwe, kimilikishwe na kipangiwe matumizi, lakini hadi sasa ardhi iliyopimwa na kumilikishwa inakadiriwa kuwa ni asilimia moja tu. Jambo hili ndilo limepelekea migogoro isiyoisha baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi.

Aidha, Serikali kwa makusudi wanapindisha matumizi ya ardhi kwa kuwamilikisha viongozi wa nchi na wafanyabiashara wakubwa kama itakavyojionyesha katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia hii finyu ya utambuzi wa ardhi haina maana kuwa ardhi iliyobaki haitumiki au haina mwenyewe, kwani wananchi kwa miaka mingi wamekuwa wakiitumia katika kuendesha maisha yao, hivyo utaratibu wowote unaofanywa na Serikali kuimilikisha kwa mtu yeyote bila kwanza kuhusisha wale watumizi wa awali ni chanzo na kichocheo cha migogoro. Hivyo ardhi isikodishwe kabla ya kuwafikiria watumiaji wa ardhi hiyo kwenye maeneo husika (wakulima na wafugaji). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mamlaka ya usimamizi wa ardhi, Wizara ya Ardhi ni Wizara mtambuka, chini ya Taasisi yake ya Tume ya Taifa ya Mipango Wizara ina wajibu wa kuratibu utayarishaji na utekelezaji wa mipango na matumizi ya ardhi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya uwekezaji, kilimo ikiwa ni pamoja na kusaidia kupatikana kwa kwa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza, makazi, malisho (ufugaji), wanyamapori, misitu, vyanzo vya maji na shughuli zote zinazotumia ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ndio nchi, ardhi ndio msingi wa maendeleo. Kwa hiyo, hakuna amani, ustawi wala maendeleo kwa wanadamu bila matumizi bora na endelevu ya ardhi. Kwa bahati mbaya, baada ya kukumbatia sera ya uchumi huria ambalo limegeuzwa kuwa holela, uongozi wa nchi yetu umetelekeza kabisa wajibu wa kusimamia matumizi yenye tija ya ardhi kwa nchi yetu na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kushindwa huko kumejidhihirisha katika maeneo makuu mawili. Moja, masuala ya usimamizi wa ardhi yamewekwa chini ya Wizara zaidi ya moja hivyo hivyo kuleta mkanganyiko kwenye suala la uwajibikaji. Kuna muingiliano mkubwa sana wa majukumu baina

ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). *(Makofi)*

Pili, usimamizi wa maafisa za ngazi za kati na za juu umedhoofika kwa sababu ya kuwajibika kwa zaidi ya mamlaka moja. Mfano halisi ni maafisa ardhi wa halmashauri ya miji na wilaya ambao wanategemewa kuwa chini ya wakurugenzi wa halmashauri na wakati huo huo kuwajibika kwa Kamishna wa Ardhi na Waziri wa Ardhi. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kutokana na kukosekana kwa usimamizi thabiti wa Maafisa Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu za Serikali zinaonyesha kuwa halmashauri za wilaya zina upungufu mkubwa wa wataalam wa ardhi kwa asilimia 74, ikiwa ni sababu mojawapo ya kukua kwa kasi ya ajabu kwa vyombo visivyo na mamlaka kisheria kushiriki katika usimamizi, utawala na kutengeneza matumizi bora ya ardhi ya vijiji kama vile Mkuu wa Wilaya, Mbunge, Kamati za Ulinzi na Usalama na Mkuu wa Mkoa. Kwa mujibu wa Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 na ile ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 1982, hawa hawahusiki na usimamizi wa ardhi za vijiji. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mkakati ilionao wa kuviimarisha Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ili viweze kutoa wahitimu wengi ili kupambana na upungufu uliopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kila Taasisi/Idara/Wizara kujifanyia mambo yake, tumeshuhudia kutupiana mpira baina ya Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Wizara ya Nishati na Madini juu ya mgogoro wa ardhi unaowahusisha wakulima wa kijiji cha Nzasa wakipinga kuondolewa katika makazi yao halali. Katika mgogoro huu Wizara ya Maliasili na utalii wanataka kuwaondoa wananchi katika ardhi yao halali kwa madai kwamba wanaishi ndani ya hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Msitu ya wa Kazimzumbwi ilianzishwa na Gavana E. F. Twining kwa Tangazo la Serikali Na. 306/1954 la tarehe 24/9/1954. Tangazo hili liliweka mipaka ya Hifadhi ya Misitu wa Kazimzumbwi. Kwa mujibu wa mipaka husika, eneo lililo katika mgogoro halimo katika hifadhi hiyo na hata kama lingekuwepo, kwa mujibu wa hukumu za Mahakama utaratibu wa kisheria wa kutangaza eneo kugeuzwa kuwa na hifadhi haukufuatwa hivyo kubatilisha zoezi zima!

Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko hayo Ikulu ilimwandikia barua Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi barua yenye Kumb. Na. CEA 110/302/IV/01 ya tarehe 10/6/2008 ikitaka Wizara ikapime eneo la Nzasa - Chanika kujiridhisha kama kweli wakulima hao walikuwa ndani ya msitu wa Kazimzumbwi au la, barua ambayo haijapatiwa majibu mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara iliambie Bunge hili Tukufu ni kwa namna gani walifanyia kazi barua toka Ikulu zenye kumbukumbu namba CEA 110 /302/IV/01 ya tarehe 10 Juni, 2008 na barua yenye kumbukumbu namba CEA 110/302/IV/01 ya tarehe 18 Septemba, 2009 hasa ikizingatiwa kwamba kuna tuhuma kutoka kwa wanakijiji kwenda kuwa viongozi wa Serikali ya CCM wanatumia Idara ya Maliasili kama Gamba kutaka kunyang'anya ardhi ya kijiji kwa manufaa yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi hapa nchini hivi sasa imekithiri kufikia hatua ya uvunjifu wa amani na kufikia hadi umwagaji damu na pengine vifo kutokea katika maeneo kadhaa. Hali hii imeondoa utamaduni wetu wa asili wa kuvumiliana na kumaliza matatizo yetu kwa njia muafaka za mazungumzo. Ni muhimu Serikali ikaelewa kwamba kupuuza migogoro hii ya ardhi nchini ni sawa na kuatamia bomu, hivyo ni lazima hatua za haraka zichukuliwe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji, ubinafsishaji na hatma ya ardhi ya Tanzania, migogoro hasa ya wananchi na wawekezaji inakua kwa kasi na kuchukua sura mpya. Anapokuja mgeni kwa jina la mwekezaji matendo ya Serikali yetu yanapingana na usemi usemao mgeni njoo mwenyeji apone, bali imekuwa mgeni njoo mwenyeji asulubike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inawapa matumaini makubwa wakulima wa Tanzania kwa mipango kabambe ya kilimo cha kisasa, pamoja na uwekezaji mkubwa wa kilimo

utakaogharimu mabilioni za dola la Kimarekani kutoka kwa wanaoitwa wafadhili, hoja za msingi ni kama kilimo hicho kina malengo ya kumnuufaisha mkulima wa Tanzania au malengo yake ni kupokonya ardhi ya wazawa na kisha kuwageuza vibarua/manamba ndani ya ardhi yao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanya na HakiArdhi juu ya hali ya maeneo yaliyokuwa ya *Nafco, NARCO* na mashamba yaliyotelekezwa wamebainisha yafuatayo:-

(i) Ubinafsishwaji wa mashamba ulitawaliwa na utata na udanganyifu mkubwa hali iliyopelekea uadui baina ya wawekezaji na wakulima wadogo wadogo kwa upande mmoja na mgogoro kati ya wakulima wadogo na wafugaji kwa upande mwingine. Katika maeneo yaliyokuwa mashamba ya ngano, Hanang *(Hanang Wheat Complex (HWC)* na *Dakawa Ranch* iligundulika kwamba wakati wananchi wanaozunguka mashamba hayo wana mahitaji makubwa sana ya ardhi wawekezaji na vigogo wenye fedha wamejilimbikizia maeneo makubwa ambayo hawayaendelezi kwa ukamilifu. Kambi ya upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu na Watanzania kwa ujumla nini kilichojiri katika ugawaji wa ardhi ya iliyokuwa *Dakawa Ranch* na ni wanakijiji wangapi walinufaika na mgao huo!

(ii) Wawekezaji kuwakodisha wananchi wenyeji mashamba kwa ajili ya kilimo na kuwatoza fedha. Haya yalitokea katika mashamba yanayomilikiwa na *Rai Group* ambapo wananchi walikuwa wanakodisha $ 10 kwa ekari. Hali kama hii pia inafanyika katika shamba la mpunga Mbarali na Kapunga, yote yakiwa wilaya ya Mbarali.

(iii) Mashamba yaliyotakiwa kurejeshwa kwa wananchi lakini hayajarejeshwa, kati ya mashamba hayo ni Shamba la Gawal na Warret, lililopo Hanang lenye ukubwa wa hekta 4,000. Maamuzi ya kuyarejesha mashamba kwa wananchi yalifanyika toka mwaka 2004/2005. Kambi ya Upinzani inataka kauli ya Serikali kuhusiana na mustakabali wa mashamba haya! Kambi ya Upinzani inaitaka pia Serikali itoe tamko juu ya mustakabali wa shamba la Bassotu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kijiji cha Chasimba, Boko Dar es Salaam, hivi karibuni kumekuwa na matamko mbalimbali kutoka kwa Kampuni ya Saruji *(Tanzania Portland Cement Co. Ltd.),* ikitishia kufunga kiwanda kwa madai kwamba hawana eneo la kutosha. Hoja yao kubwa ni kwamba wananchi wa kijiji cha Chasimba wamevamia eneo lao na kwamba wanashindwa kujipanua kama kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nilizungumze hili ili kuondoa upotoshwaji unaotaka kufanywa na kiwanda husika. Ni muhimu Bunge hili Tukufu likafahamu kwamba Chasimba ipo ndani ya Kijiji cha Boko, kijiji ambacho kiliandikishwa kama kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Kuandikisha Vijiji, kutambuliwa kwa Vijiji vya Ujamaa na Uongozi wa Vijiji, 1975 na hati kutolewa 25/2/1976 na hakuna mazingira yoyote yanayoonyesha kwamba kijiji hicho kilifutwa ama kubatilishwa. Lakini kama ilivyo kawaida yetu, kuendekeza wawekezaji dhidi ya wenyeji, wanakijiji waliuzwa wakiwa ndani ya ardhi yao, ndipo likaja suala la kujalidiana kuhusu fidia, zoezi ambalo liliendeshwa kihuni hasa ikizingatiwa kwamba mwekezaji alikuwa na hati tayari! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwekezaji akidai anamiliki eneo lote la viwanja 1, 4 na 7 kuna nyaraka za Serikali zinazoonyesha kwamba mwekezaji husika hakupewa umiliki wa eneo lote, kuna eneo ambalo lilibaki Serikalini na mchakato wa kutengeneza hati mbili ulikuwa umefanyika na kufikia hatua za mwisho kabisa na nyaraka zipo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kiwanda kushindwa kujitanua kwa sababu haina eneo la kutosha hazina mashiko hata kidogo. Kwa mujibu wa barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni ya tarehe 30/5/2002 kwenda kwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Barua husika inaelezea ombi ambalo Manispaa ya Kinondoni ililipata kutoka kwa *M/S Tanzania Portland Cement Company Ltd.* la kutaka kugawanywa kiwanja na 1,4 na 7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barua husika inabainisha kwamba Kikao cha Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kilichofanyika tarehe 22/5/2002 kililijadili suala hilo na kulikubali kutokana na wawekezaji katika kiwanda hicho kutokuwa tayari kulipia eneo ambalo si la uzalishaji na wala si

la malighafi! Kwa ujumla eneo lote lina ukubwa wa hekta 922.22, eneo linalohusika na uzalishaji na malighafi lina ukubwa wa hekta 685. Eneo ambalo halitumiki na mwekezaji ni hekta 236.63. Ni eneo hili ambalo ndilo lina makazi ya wananchi ambao wengi wao walidhulumiwa kwa kulazimishwa kumpisha mwekezaji pasipo utaratibu wa kisheria kufuatwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunaishauri Serikali ambayo inataka kuwaondoa wananchi kwa nguvu kuliangalia suala hili kwa busara ya hali ya juu. Tofauti na maeneo mengine ambayo kuna uvamizi wa maeneo ya watu, wananchi eneo hili, wengi wao ni watu wazima ambao wana kila ushahidi wa kuonyesha kwamba pale ni asili yao na kilichofanyika ni dhuluma dhidi yao kupisha wenye fedha na hawapo tayari kuacha makazi yao, wakiungwa mkono na Mbunge wao na Madiwani wao wa Kata za Wazo na Bunju (CCM)! Tumeweka itikadi pembeni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufisadi wa ardhi na mustakabali wa Mtanzania maskini mkoa wa Mbeya, katika Wilaya ya Mbarali, shamba la mpunga la Mbarali *(Mbarali Rice Farm* - ekari 14437) na shamba la mpunga la Kapunga (ukubwa ekari 18425) yalikuwa ndio chanzo cha mapato cha wananchi wa eneo husika. Mashamba haya yalikuwa yanahudumia watu zaidi ya 30,000 na vijiji kumi. Ardhi hiyo pia ilikuwa inahudumia watu wa Iringa na Wilaya nyingine za Mbeya. Mipango ya awali ya Serikali, mwaka 2003/2004 kama ilivyobainishwa na aliyekuwa Waziri wa Kilimo ilikuwa ni kuyabinafsisha mashamba hayo kwa wakulima wadogo wadogo, mpango ambao ungejumuisha mashamba ya Ruvu na Dakawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na nguvu ya mafisadi kuizidi hekima ya Serikali na licha ya kilio cha aliyekuwa Mbunge wa Mbarali kipindi hicho Mheshimiwa Esterina Kilasi, Serikali iliamua kuuza eneo husika kwa Kampuni ya *Highland Estates Ltd*. Mmiliki wa sasa Bwana Nawab Mulla ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa wa Mbeya. Wananchi wamegeuka wapangaji kwa kukodisha maeneo ili waweze kulima na kujipatia kipato! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Shamba la Mbarali akipewa kwa bei ya kutupa Mwenyekiti wa CCM, shamba la Kapunga lilibinafsishwa na kukabidhiwa kwa Kampuni ya *Export Co. Ltd.* kwa bei ya kutupa ya shilingi bilioni 2.3, mmiliki akiwa bwana Jeetu Patel (Jina halisi Jayantkumar Chandubhai Patel). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ndio Tanzania ambayo wazawa wananyang'anywa ardhi, maeneo yote muhimu na ya kimkakati na kukabidhiwa wageni au watu wenye mamlaka na fedha huku ikiwaacha wazawa kubaki vibarua au wakulima wadogo wanaotegemea hisani ya mabeberu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado mustakabali wa shamba la mahindi Mbozi haujajulikana, serikali inataka kumpa mwekezaji, wakati wananchi wana uhaba wa ardhi kwa matumizi yao! Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe majibu kuhusiana na hatma ya shamba la mahindi mbozi. Halikadhalika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iliambie Bunge hili Tukufu, ni vigezo gani vilivyotumika kupata wanunuzi wa shamba la mpunga la Mbarali, shamba la Kapunga na mashamba husika yaligawiwa kwa maslahi ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara, Musoma Mjini kumekuwa na mtafaruku mkubwa kati Jeshi la Wananchi (JWTZ) na wananchi wa Bukanga na Buhare (Mgaranjabo) kutokana na jeshi kujimilikisha maeneo yao ya asili, waliyokuwa wakitumia kwa ajili ya matambiko kwa kabila ya Wakwaya. Hivi sasa wananchi hao hawaruhusiwi kuingia katika eneo hilo, jambo hilo limezusha chuki kubwa sana kati ya Jeshi na jamii ya Wakwaya wakazi wa Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro na matatizo ya ardhi, kwa wakubwa kunyang'anya wanyonge ardhi imeikumba pia Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Mgogoro huu unahusu shamba namba 299 (iliyokuwa *NARCO Ranches*),lenye ukubwa wa hekta 49,981. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika shamba hili taarifa zinaonyesha kwamba hekta 30,007 walipewa *Mtibwa Sugar* licha ya malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba eneo walilopewa ni

kubwa sana. Taarifa za kiuchunguzi zinaonyesha kwamba maeneo ambayo yalikuwa yamepangwa kugawiwa wanakijiji wa kijiji cha Wami, yamegawiwa wananchi wafuatao: -

(i) Bwana Philip Mangula, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, ndio anaongoza kwa kuwa mwanakijiji mwenye eneo kubwa, alipewa hekta 2000;

(ii) Bwana John Malecela, Waziri Mkuu Mstaafu na Makamu Mwenyekiti wa CCM alipewa hekta 100;

(iii) Jenerali Mstaafu Ngwilizi, ambaye pia alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa Awamu ya Tatu alipewa hekta 100 kati ya hekta 5000, zilizosemwa wamepewa wakulima wadogo wadogo wa kijiji;

(iv) Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, anamiliki hekta 2000, ambazo hazijaendelezwa;

(v) Waziri Mkuu Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Frederick Sumaye hekta 500; na
(vi) Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, hekta 1000 (ila tofauti na wengine shamba hili limeendelezwa).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inahoji kama hawa watajwa hapo juu ni wakazi wa kijiji cha Wami - Dakawa? Na ni vigezo gani vilitumika kuwanyima ardhi wanakijiji na kuwapa wakubwa hawa? Serikali haioni kwamba mgao huu wa ardhi uliojaaa dhuluma na upendeleo unahatarisha maisha ya Watanzania na usalama wa nchi kwa ujumla? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo haya wana hasira na Serikali yao kwa kuwa wameshaambiwa hakuna tena eneo la kugawa wakati walitozwa shilingi 20,000 kila mmoja kwa madai kwamba wangepewa hekta tano. Ahadi ya hekta 10,019 kwa wakulima na wafugaji, imegeuka hewa! Tunakwenda wapi kama nchi? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya zoezi la ugawaji wa ardhi katika maeneo yote yenye utata ambayo yalitawaliwa na rushwa, ubabe na udanganyifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Pwani, *Simba Motors Vs* wakakijiji katika Kitongoji cha Undindivu, Mapinga – Bagamoyo wananchi wa Kijiji hicho chenye idadi ya watu zaidi 1,400 wamekuwa wakimiliki eneo la Undindivu kwa ajili ya kilimo na ufugaji toka mwaka 1960. Kama ilivyo kawaida yetu, Kampuni ya *Simba Motors (T) Ltd.* ilimilikishwa eneo lote la kitongoji cha Undindivu bila wananchi au Serikali ya kitongoji na kijiji kujulishwa. Kampuni hiyo ilipima kwa kutumia mpimaji binafsi na ilimilikishwa shamba hilo lenye hekta 322. Baada ya kampuni husika kupima na kumilikishwa bila kufuata sheria takriban miaka 17 imepita kampuni hiyo haijawahi kuendeleza shamba hilo, kampuni haijawahi kuliendeleza eneo hilo, si kwa kilimo au ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kuna mgogoro mkubwa baina ya *Simba Motors* na wananchi wa kitongoji cha Undindivu na kutokana na shamba husika kumilikishwa kwa tajiri mmoja, wakati wakazi wa maeneo hayo wamekosa maeneo kwa ajili ya huduma muhimu za jamii na maeneo kwa ajili ya kupanua makazi yao ya kuishi, kwa sababu robo tatu ya eneo la kijiji limamilikiwa na tajiri huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuutafutia mgogoro huu ufumbuzi wa kudumu. Hatuwezi kuendelea kukaa kimya na kuacha wananchi wetu maskini wakipokonywa maeneo yao kwa faida ya matajiri wachache! Kambi ya Upinzani inajua kwamba ofisi yako ilishaletewa taarifa kwa barua ya tarehe 15/12/2010, hakuna kilichofanyika mpaka sasa. Tunataka majibu!

Mheshimiwa Spika, suala la mkoa wa Rukwa, *Agrisol,* Kilimo Kwanza na hatma ya Tanzania, nchi yetu imefika hapa ilipo kutokana na watu wenye dhamana kuingia mikataba mibovu ambayo badala ya kuisaidia nchi imekuwa ni msalaba mkubwa na kuwaacha Watanzania katika dimbwi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Kampuni ya *Agri-Sol Energy LLC* na Kampuni ya *Serengeti Advisors Ltd.,* inayoongozwa na Bwana Iddi Simba (aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Awamu ya Tatu) na Betram Eyakuze kwa pamoja wameunda Kampuni ya *Agrisol Energy Tanzania,* wameingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Mkataba ambao unatarajia kuipa kampuni husika miliki ya miaka 99 ya maeneo ya lugufu hekta 80,317 na Mishamo hekta 219,800. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masharti ya msingi katika makubaliano baina ya Halmashauri husika na wawekezaji ni yafuatayo:-

(a) Kodi ya Ardhi *(Land rent)* ambayo ni shilingi 200 kwa hekta;

(b) Ushuru wa Kisheria wa Halmashauri;

(c) Ada itakayolipwa Halmashauri ni shilingi 500 kwa hekta; na

(d) Na sharti la mwisho, kama mgogoro utatokea baina ya pande zote mbili, busara itatumika kutatua mgogoro, ikishindikana Chemba ya Biashara ya Kimataifa *(ICC)* ndio atakuwa msuluhishi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda wapi? Umaskini ndio utufanye tuwe mambumbu wa kufikiri? Hivi kwa nini hatujifunzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua za awali, Madiwani wa Halmashauri husika walikataa kutoa maeneo yote mawili, waliagiza mwekezaji apewe eneo moja na kwa kipindi cha miaka 20. Kama ataonekana kufanya vizuri, wangefikiria kumwongezea muda na eneo! Kama kawaida walioonekana kuwa wakali wakapelekwa Marekani, kwa siku nne! Baada ya kurejea, nchi ikaingizwa kwenye mkataba mwingine ambao utaigharimu nchi miaka mingine 99 kuweza kujinasua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si dhamira ya Kambi ya Upinzani kudhihaki ama kukatisha tamaa uwekezaji, tunafahamu kwamba Serikali inaichukulia *Agri-Sol Energy* kama sehemu ya mkakati wake wa Kilimo Kwanza, lakini hawa wawekezaji ambao wanaitwa wakubwa, mashamba ambayo wanayaendesha haswa yale yaliyoko Marekani na yaliyotembelewa na maafisa wa Serikali wakiongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu yana ukubwa wa ekari 17,900, (ambapo ekari 13,195 ni za mahindi na ekari 4705 ni maharage). Na shamba hilo limeajiri watu 13, hivi hawa ni wakulima kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba kulikuwa na mkakati uliokuwa ukiendeshwa kwa usiri mkubwa na kwa kasi ya hali ya juu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI wa kuwasambaza wakimbizi wanaokadiriwa kufikia 162,000 nchi nzima, katika mikoa mbalimbali, mchakato ambao ulipata upinzani mkubwa hapa Bungeni na kutoka mikoa husika. Huu ulikuwa ni mkakati wa makusudi ili maeneo husika yawe wazi kwa wawekezaji hao kukabidhiwa na mbaya zaidi wakimbizi waliambiwa bayana kwamba sharti la kupewa uraia wa Tanzania ni kuondoka maeneo hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu ikaeleweka kwamba huu mtindo wa kuwageuzwa Watanzania manamba ndani ya nchi yao kwa kutoa ardhi kwa wageni utakuja kusababisha machafuko hapo baadae. Ieleweke hoja hapa sio kulisha Taifa na kupata ziada kusafirisha nje ya nchi, hoja hapa ni kumnufaisha Mtanzania katika mipango yote endelevu ya matumizi ya ardhi! Na kama ni suala la chakula na kusafirisha nje ya nchi chakula hicho kipo tatizo ni kukitoa kwa wakulima na kufikisha sokoni, ushahidi huo upo kuwa mahindi ni mengi kuliko uwezo wa wananuni (Rukwa, Songea, Iringa - Ludewa na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya mwaka 1999, vifungu vya 19(2), 20(1), 20(2), 20(3) na 20(4) vya Sheria ya Ardhi vinatoa masharti ya umiliki wa ardhi kwa watu ambao sio Watanzania. Kwa ujumla wake vifungu husika vinapiga marufuku ardhi kupewa kwa wageni isipokuwa tu kwa madhumuni ya uwekezaji chini ya Sheria ya uwekezaji Na. 26 ya mwaka

1997. Na ili ardhi husika iweze kupatikana lazima kwanza itambuliwe, itangazwe kwenye Gazeti la Serikali na iwe *allocated* kwa Kituo cha Uwekezaji ambacho ndicho kitakuwa na jukumu la kumpatia mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, haya yote hayajafanyika na kinachotaka kufanyika kwa kutumia vibaraka wa kitanzani , ni kuhakikisha kwamba wabia (vibaraka) wa Kitanzania wanakuwa na hisa nyingi katika umiliki wa ardhi ili kuepuka kikwazo cha kupitia katika Kituo cha Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mamlaka ya kuingia ubia *(joint venture)* na mwekezaji ambaye si Mtanzania kama ambavyo inaonekana ni kamchezo ambako kanataka kuchezwa na *Serengeti Advisers Limited*, mabadiliko ya Sheria ya Ardhi yaliyofanyika mwaka 2004, Sheria Na. 2/2004 *The Land (Amendment ) Act 2004* Kifungu cha 19(1), (2)(c) kinasema ili kufanikisha masharti ya uendelezaji wa ardhi, raia wa Tanzania anayemiliki ardhi anaweza kuingia *joint venture* na mwekezaji ambaye si raia wa Tanzania kwa madhumuni ya uwekezaji chini ya Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38. Kwa mujibu wa Kifungu hicho ubia unafanywa na mzawa na mgeni. Kwa mujibu wa Sheria ya Uraia *(The Tanzanian Citizenship Act, Cap 357)*. Shirika la Umma au Kampuni au Halmashauri haiwezi kuwa na sifa za kuwa raia. Hivyo kwa mujibu wa kifungu 19(2)(c) si Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda wala Kampuni ya *Serengeti Advisers* yenye uwezo wa kutoa ardhi yake kwa mtu ambaye si raia ili kuwekeza kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo ya vifungu nilivyovitaja hapo juu (isipokuwa kama kuna mabadiliko ya sheria ambayo hadi sasa haifahamiki), Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na Kampuni ya *Serengeti Advisers* haina uwezo wa kuwekeza kwa pamoja *(joint venture)* na wawekezaji ambao si Watanzania mpaka hapo sheria zitakapofanyiwa marekebisho. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ituambie, ilitumia utaratibu gani wa kisheria kuingia mkataba huo wa kifedhuli na usio na maslahi hata kidogo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na Taifa kwa ujumla? Nani aliwatuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, kilimo na ufugaji ni ya sekta zinazoongoza kwa kutoa mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa, halikadhalika ndizo zinazoongoza kwa kutoa ajira kwani zaidi ya 80% ya Watanzania wamejiajiri katika sekta hii hasa vijijini. Hivyo basi kuboresha hizi sekta mbili maana yake ni kwamba tutakuwa tumeboresha 80% ya maisha ya Watanzania kwa kuwa na uhakika wa kipato, usalama wa chakula na kuongezeka kwa Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kwa nchi yetu kutokea kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji, chanzo cha migogoro hiyo ni kutokana na kutokuwa na mipango thabiti ya Serikali ili kubainisha/kutenganisha maeneo maalum kwa ajili ya wakulima, halikadhalika wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria yetu ya Ardhi, Na. 4 na Na. 5 ya mwaka 1999 imeainisha utaratibu ambao miliki ya ardhi ya mtu mmoja mmoja ama kikundi inavyotambulika kisheria mijini na vijijini kisheria ama kimila. Hata hivyo utaratibu wa utwaaji na umiliki ardhi hasa vijijini kwa matumizi ya wafugaji, wachungaji na wawindaji haujaainishwa ipasavyo! Mikakati ya kutenga ardhi hasa ya wafugaji imekuwa finyu mno kiasi kwamba wakulima na wawekezaji wameendelea kuhodhi/kuvamia ardhi ya wafugaji kwa msaada wa mawakala wa Serikali. Na wakati mwingine wafugaji wamekuwa wakivamia maeneo ya wakulima kutokana na kukosa maeneo muafaka kwa ajili ya malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafiti pia zimeonyesha kwamba ardhi ya wafugaji imekuwa ikichukuliwa kwa ajili ya matumizi ya wawekezaji, kugeuzwa kuwa Hifadhi za Taifa au *Game Reserves!* Matokeo yake wafugaji wanageuka watu wa kutangatanga! Wakati Serikali imekuwa ikiwataka wafugaji waondokane na njia za kizamani za kufuga, bado haijaonyesha njia mbadala za ufugaji wa kisasa!

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze ina mikakati gani katika kuhakikisha kwamba maeneo rasmi ya wafugaji yanabainishwa ili kuepusha umwagaji damu na

migogoro isiyo na tiba huko mbeleni. Halikadhalika Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko juu ya tatizo la mpaka na mgogoro wa wakulima na wafugaji wa jamii ya Wamasai katika eneo la vijiji vya Izava (Chamwino) na Chitego (Kongwa), mgogoro ambao kwa kiasi kikubwa ulisababishwa na maamuzi ya kibabe yaliyofanywa na wakuu wa wilaya hizi mbili (mwaka 2006), wakishirikiana na Mwenyekiti wa Halmashauri kipindi hicho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wa maeneo haya wanalalamikia wafugaji ambao waliingizwa kibabe katika maeneo yao bila kuwashirikisha kwa nguvu za kigogo mmoja, matokeo yake mashamba yao ndio yamegeuka malisho ya mifugo hiyo! Kumekuwa na tuhuma ya ushiriki wa askari wa Kongwa katika zoezi hili kandamizi!

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifuatilie mgogoro huu ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea hasa ikizingatiwa kwamba matukio ya kushambuliana, kujeruhi na kutishia maisha imekuwa ni jambo la kawaida baina ya pande mbili.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya tathmini na malipo ya fidia, imekuwa ni jambo la kawaida kwa wananchi kulalamika kupunjwa ama kutokulipwa kabisa fidia pale ambapo wanatakiwa na Serikali kuhama maeneo yao ili kupisha matumizi mapya ya ardhi. Sheria zetu zinatamka bayana kwamba pale ambapo mwananchi anapochukuliwa eneo lake na Serikali kwa matumizi mengine na hivyo kutakiwa kuhama anatakiwa kulipwa fidia inayojumuisha, thamani ya ardhi, usumbufu, usafiri na hasara ambayo muathirika ataipata kutokana na kuchukuliwa eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kumekuwa na malalamiko kila pahala ambapo wananchi wanatakiwa wasimamishe shughuli zao kupisha matumizi mapya ya ardhi. Serikali hailipi fidia ya kutosha na hata wananchi wakilalamika Serikali inaendelea na miradi, badala ya fidia kumwacha mwananchi awe katika hali aliyokuwa mwanzo, mfumo wa fidia wa nchi yetu, haswa maeneo yanapochukuliwa na Serikali (ambayo ndio hiyo hiyo inafanya tathmini na kuamua kiasi gani kilipwe) unamwacha muathirika fukara zaidi! *(Makofi)*

(a) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo juu ya hatma ya wananchi wa Kurasini Mabwawani ambao tangu nyumba zao zifanyiwe tathmini miaka miwili iliyopita ili kupisha upanuzi wa bandari, kumekuwa na kimya kingi na wakiuliza kuhusu hatma yao, hawajibiwi kitu! Kuna kundi ambalo limelipwa, kuna kundi lingine halielewi nini kinachoendelea na wanashindwa kuendeleza maeneo yao.

(b) Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Ardhi itoe maelezo juu ya hatma ya wananchi wa kijiji cha Mabwepande, kata ya Mabwepande Jimbo la Kawe ambao miaka minne iliyopita Serikali ilikwenda kufanya tahmini na kuwaagiza wananchi kutokufanya maendeleo yoyote ili kupisha upanuzi wa Chuo cha *IFM.* Hakuna kilichofanyika mpaka sasa, wananchi waliokuwa wanategemea kilimo wamezidi kufukarishwa, Serikali ikiulizwa haina majibu. Matokeo yake maeneo ambayo waliambiwa wayaache sasa yamevamiwa na genge la wavamizi, si Wizara, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ama vyombo vya usalama vinavyochukua hatua licha ya kupewa taarifa ya uvamizi huu! *(Makofi)*

(c) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hatma ya wananchi wa Kigamboni (ambao wengi walikuwa wanafanya kazi za kilimo) ambao wanalalamikia zoezi la kuchukua maeneo yao kupisha ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni kutawaliwa na rushwa, maeneo kuthaminishwa bei ndogo, wakati huo huo Serikali baada ya kulipa fidia kiduchu wanauza maeneo husika kwa bei ya kutupwa, bei ambayo mwananchi wa kawaida hawezi kuimudu! *(Makofi)*

(d) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hatma ya wananchi wa 1,600 wa Wilaya ya Mbarali waliotakiwa waondoke maeneo yao ili kupisha upanuzi mbuga ya Taifa ya Ruaha? Serikali ilitoa shilingi bilioni 6.5 tu kwa wakazi wote. Kwa tathmini ya kawaida kila mwananchi alipewa shilingi milioni 4.5. Hivi kwa maisha ya sasa kuna nyumba inayoweza kujengwa na kukamilika kwa kiasi hicho cha fedha? Huu ni unyonyaji na udhalimu ulio dhahiri. *(Makofi)*

(e) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hatma ya fidia ya wananchi wa Jimbo la Ubungo Kata ya Kwembe wanaopaswa kuhama kupitisha ujenzi wa majengo wa Chuo Kikuu cha

Sayansi ya Tiba ya Afya *(MUHAS)* Mloganzila. Wakati wa kuhitimishwa kwa Bajeti ya Waziri Mkuu katika mkutano huu wa Bunge, Serikali ilieleza kwamba tathmini ya fidia inaendelea na kwamba wapo wananchi ambao tayari wamelipwa fidia na wengine bado hawajalipwa mpaka sasa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia kwamba fidia iliyolipwa kwa wananchi wachache ni ya mali na mazao; hata hivyo wananchi hawajalipwa fidia ya ardhi. Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa maelekezo kwa Wizara zinazohusika kuhakikisha fidia stahiki inalipwa. Mwaka 2010 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ilifanya mkutano na wananchi na kuwaahidi kulipa fidia ya ardhi kwa mujibu wa sheria, Kambi ya Upinzani inataka Serikali ieleze malipo hayo yatatoka kwenye fungu lipi na yatalipwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malalamiko dhidi ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA),* mwaka 2004, Serikali kupitia wakala wa majengo mkoani Dodoma, waliwauzia wananchi nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na lililokuwa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. Malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi hawa wa Tambukareli ni kunyimwa hati za nyumba zao na *CDA* ilhali wameshalipia nyumba hizo kwa ukamilifu. Sababu zinazotolewa na *CDA*, zisizo na mashiko ni kwamba eti Serikali ilitoa uamuzi wa kuuza nyumba bila kuwahusisha *CDA*, hivyo hawatambui uuzwaji wa nyumba hizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelekezo kwa *CDA* kutoa hati husika, ni suala la kiburi na jeuri kwa taasisi ya Serikali kuhoji maamuzi ya Serikali au leo tuelezwe kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano inafanya kazi chini ya *CDA?* Kama kulikuwa na uzembe ndani ya Serikali, kwa nini wananchi hawa maskini waliodunduliza vihela vyao wapate makazi waumizwe? Kambi ya Upinzani inataka kauli thabiti ya Serikali kuhusiana na hili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria Na. 5 ya Ardhi ya Vijiji na mustakabali wa Taifa, Sheria ya Ardhi ya Kijiji inatoa mamlaka kwa Halmashauri ya kijiji kusimamia ardhi yote ya kijiji. Halikadhalika Halmashauri ya kijiji imepewa mamlaka ya kugawa ardhi baada ya kuruhusiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Uzoefu umeonyesha kwamba kutokana na kutokuwa na ufahamu mpana wa sheria, watu wenye fedha wamekuwa wakitumia fursa hii ya kisheria vibaya kwa kuwarubuni viongozi wa vijiji na hatimaye kugawa maeneo ya kijiji kwa wageni wenye fedha wachache, huku ikiwaacha wanakijiji bila ardhi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali inakuwa mbaya zaidi pale ambapo watu ambao sio Watanzania wanatumia upenyo huu wa kisheria na kumilikishwa maeneo makubwa ya kijiji kinyemela! Kambi ya Upinzani imepata malalamiko kutoka kwa wanakijiji wa kijiji cha Orngadida, Kata ya Qash, Babati (taarifa ambayo Waziri wa Ardhi, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wanayo). Wanakijiji hao wanawatuhumu viongozi wa Serikali ya Kijiji wakishirikiana na Diwani kuuza ardhi kwa wageni pasipo kuwashirikisha, wanakijiji wamemwandikia Mkuu wa Wilaya ya Babati barua mbili ambazo nazo hazijajibiwa!

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba kuna wageni wengi waliopata maeneo ya vijiji kinyemela kwa kutumia upenyo huo wakati Sheria ya Ardhi Na. 4 , kifungu cha 20 kinakataza wageni kumiliki ardhi nchini isipokuwa kwa malengo ya uwekezaji tu na ambao umiliki wake lazima upitie Kituo cha Uwekezaji Tanzania na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iliambie Bunge lako Tukufu, ni lini imefanya tathmini katika vijiji vyetu ili kuweza kubainisha ardhi zilizotolewa na Halmashauri za Kijiji na uhalali wake. Ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba sheria hii isipoangaliwa kwa umakini itasababisha umwagaji damu mkubwa hasa pale wananchi watakapohisi kunyang'anywa ardhi yao kifisadi au vinginevyo na mbaya zaidi zoezi hili linafanywa hata mijini na Serikali za Mitaa ambazo hazina mamlaka ya kugawa ardhi. Mchezo ambao wanafanya kwa kushirikiana na watendaji wa manispaa na baadhi ya Maafisa wa Wizara! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvamizi wa maeneo ya wazi mkoa wa Dar es Salaam, kutokana na malalamiko ya wananchi mbalimbali kuhusu uvamizi wa maeneo ya wazi ya umma katika mkoa wa Dar es Salaam, Serikali iliunda Kamati ya kufanya uchunguzi kuhusu uvamizi katika maeneo husika. Kamati ilikamilisha kazi yake tarehe 13 Julai, 2010.

Pamoja na majibu ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi aliyoyatoa tarehe 1 Julai, 2011 wakati akijibu maswali Bungeni kuhusu hatua ambazo Serikali imechukua toka mamlaka husika zilipokabidhiwa ripoti husika, Kambi ya Upinzani inataka maelezo zaidi kutoka kwa Serikali kwa kuwa mwaka mmoja umepita toka uchunguzi huo ufanyike na sehemu kubwa ya viwanja bado vipo mikononi mwa wavamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze, ni viwanja vingapi vimerudishwa na vingapi bado vipo mikononi mwa wavamizi? Ni lini Serikali itarejesha viwanja vyote vilivyobaki kwenye matumizi yake kwa mujibu wa sheria kwa kurejea mapendekezo ya Kamati? Ni hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika Wizarani na kwenye halmashauri walioshiriki kusababisha hali hiyo ukiondoa maafisa wachache ambao wamefikishwa mahakamani kutokana na kesi ya kiwanja kimoja hivi karibuni? Kwa kuwa sasa Wizara ina kada ya askari *(land rangers)* ni lini askari hao watatembelea maeneo yote yaliyotajwa kuvamiwa kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari za uvamizi wa viwanja vya wazi ni kubwa katika mipango miji na maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Mathalani katika Manispaa ya Kinondoni kwenye kiwanja Na. 856 *Msasani beach* ambacho kwa mujibu wa ramani ya upimaji iliyosajiliwa namba 29331 ilikuwa ni kwa matumzi ya wazi, lakini baadae kilimilikishwa kwa mtu binafsi. Athari yake ni kuzibwa kwa njia ya mkondo kuelekea baharini yamezibwa na hivyo kuleta mafuriko katika barabara na makazi ya watu wa eneo husika, hali hiyo ipo pia katika majengo ya *May Fair* na Markham. Kambi ya Upinzani inataka Serikali ieleze hatua zipi itachukua ili kuepusha wananchi wa maeneo ya Msasani, Mikocheni na maeneo mengine katika Jiji la Dar es Salaam yaliyojengwa majengo kinyume cha sheria na mipango miji na hivyo kuleta athari kubwa kwa maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya nyumba, sekta hii ni sekta pekee inayoweza kuleta na kutekelezwa kwa dhana nzima ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Nchi yetu na Watanzania kwa ujumla bado tuna matatizo makubwa ya nyumba bora na za bei nafuu kutokana na bei kubwa ya *cement* na bati bidhaa muhimu katika kutimiza azma ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulisema na tunasema kuwa bei ya simenti na bati inaweza kuwa chini ya shilingi 7,000/=, kama Serikali itakuwa na utashi wa kuwahudumia wananchi kwa dhati, wakati ukinunua simenti Uturuki na Pakistan ukinunua tani 600,000 bei ya tani moja ni dola za Marekani 70 hadi bandarini. Guangzhou, China tani moja ni dola za Marekani 26. Kwa hesabu za kawaida kwa mfuko mmoja ni dola 3.5 sawa na shilingi 5,250 kama ukinunua Pakstan au Uturuki, ukinunua China bei itakuwa dola 1.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani bado inasisitiza kuwa kama Serikali inadhamira ya kweli mfuko wa simenti hauwezi kuuzwa zaidi ya shilingi 7,500. Hivyo basi tunaitaka Serikali itueleze kwa nini bei ya simenti inauzwa zaidi ya shilingi 14,000 kwa Dar es Salaam na kwa nje ya Dar es Salaam bei ni zaidi ya hapo, wakati malighafi zinapatikana hapa hapa nchini na kiwanda kikubwa cha simenti kinatumia gesi asili ili kupunguza gharama za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama hizi na ni faida kiasi katika kodi tunayopata kwa kuwalangua Watanzania? Serikali haioni kwamba ina wajibu wa kuondoa hizi kero wananchi wajenge nyumba bora na kwa bei nafuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* lilipoanzishwa mwaka 1962, moja kati malengo yake ilikuwa ni kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya Watanzania wafanyao kazi mijini. Hata hivyo kwa kadri siku zilivyosonga mbele, shirika hili liligeuka kutoka kuwahudumia masikini na watu wenye kipato cha kati na badala yake kuwahudumia watu wa kipato cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linahudumia asilimia 0.5 tu ya Watanzania wote wa nchi hii, swali la msingi ni je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kuwa shirika hili linahudumia Watanzania wengi zaidi kwa kuwapatia nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari, mwezi Juni, 2010 Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, akikerwa na hali ilivyokuwa katika Shirika la Nyumba alisema kwa sasa *NHC* ndilo Shirika la Umma linaloongozwa kwa rushwa nchini Tanzania na kwamba baadhi ya watumishi waandamizi wameligeuza shirika hilo kuwa ni ng'ombe wao wa kukamua fedha chafu! Katibu Mkuu alikwenda mbele zaidi, kwa kutolea mfano wa nyumba iitwayo *Victoria House* iliyopo kando ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi ambayo pesa ya pango ilikuwa ikiingia kwenye akaunti ya mtumishi wa shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko pia ya kutokuwa na uaminifu baina ya wapangaji, wakishirikiana na washirika wao waliopo kwenye utumishi wa shirika kulikopelekea shirika kupata hasara ya mabilioni ya shilingi kwa kuingia mikataba tata! Kwa mujibu wa vyanzo vya taarifa hizi, mikataba tata imekuwa ikifanyika huku ikiwashirikisha wapangaji wa asili ya kihindi kwa kiasi kikubwa ambao wanatuhumiwa kuligeuza shirika hilo kama mali yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, mwaka mmoja ukiwa umepita tangu kauli hii nzito toka kwa mtendaji wa ngazi ya juu wa Wizara, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watumishi hawa na ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wapangaji wasio waaminifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali na taasisi zake kutolipa kodi za pango kwa wakati, katika kipindi cha Julai, 2011 Shirika lilikusanya kodi za pango pamoja na malimbikizo kiasi cha shilingi bilioni 31. Pamoja na jitihada za kukusanya kodi na malimbikizo na hasa yale yanayodaiwa Serikali na taasisi zake, malimbikizo bado ni makubwa. Hadi Machi, 2011 Serikali na taasisi zake ilikuwa ikidaiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.543, baada ya kupunguza malimbikizo kwa kiasi cha shilingi milioni 115, sawa na asilimia 8 tu! Kambi ya Upinzani inataka Serikali ieleze ni kwa nini imekuwa ni mdaiwa sugu na kwa nini hailipi madeni ya Shirika la Nyumba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya ununuzi na ujenzi wa nyumba, pamoja na kuwepo kwa Sheria ya Mikopo ya Nyumba *(Mortgage Financing Act)* ya mwaka 2008 na Sheria ya Umiliki wa sehemu ya majengo *(Unit Titles Act)* ya mwaka 2008, masharti ya mikopo hii bado ni magumu. Mfano kwa sasa benki zinazotoa mikopo ya nyumba masharti yake ni pamoja na muda wa marejesho ya kati ya miaka sita mpaka 15 na riba kati ya asilimia 17 mpaka 22 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iwapo hali hii haitabadilika, itakuwa vigumu kwa wananchi, halikadhalika Shirika letu la Nyumba kujenga nyumba za gharama nafuu na kwa wananchi walio wengi kuweza kumudu mikopo ya ununuzi wa nyumba. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itueleze ni kwa namna gani imejipanga kuweza kutatua tatizo hili! Lazima Serikali iweke mazingira ya kuziwezesha benki kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wawekezaji na wanunuzi wa nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na Ongezeko la Mtaji *(Capital Gain Tax)* kwenye mauzo ya nyumba zinazojengwa na Shirika. Changamoto kubwa inayowakabili Watanzania wengi ni kuweza kupata nyumba za bei nafuu. Kwa sheria zetu za kodi, nyumba mpya iliyojengwa kwa ajili ya kuuzwa inapaswa kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* pale inapouzwa na anayelipa kodi hiyo ni mnunuzi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la msingi ni kuwa nyumba hiyo wakati inajengwa vifaa vyote vya ujenzi ulipiwa kodi hiyo, hivyo kitendo cha mnunuzi kulipa kodi ya *VAT* wakati wa kununua nyumba hiyo ni kulipia kodi mara mbili *(Double Taxation)*. Je, Serikali haioni kama haimsaidii mwananchi kuweza kuishi kwenye nyumba nzuri na kwa gharama iliyo nafuu? *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya mkakati wake wa kuwanyang'anya Watanzania hata kile kidogo walichonacho badala ya kuwaongezea umaskini iwe ni kuwapa maisha bora kama kauli mbiu yenu inavyosema. Mfano dhahiri, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 shirika lilitarajia kujenga nyumba 49 zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 4.08 kwa gharama iliyotumika, wastani wa nyumba moja ililigharimu shirika shilingi milioni 83.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Shirika la Nyumba la Taifa kuanzia Julai, 2010 hadi Mei, 2011 wanatarajia kupata shilingi bilioni 6.3 kutokana na mauzo ya nyumba hizo yaani faida ya shilingi bilioni 1.9 kwa tafsiri nyingine nyumba moja itauzwa na Shirika la Nyumba kwa shilingi milioni 129.2, wakati gharama halisi za ujenzi ni shilingi milioni 83. Kwa kila nyumba iliyounzwa shirika limepata faida ya shilingi milioni 46.

Mheshimiwa Spika, mustakabali wa nyumba za Shirika la Nyumba, hivi karibuni kumekuwa na sintofahamu nyingi kuhusiana na nyumba za shirika. Wapangaji (hususan katika maeneo ya katikati ya miji) wamekuwa wakilitaka shirika liwauzie nyumba. Kambi ya upinzani inaitaka serikali itoe kauli, nini msimamo wake kuhusiana na suala hili, lakini sisi tunaona kuwa hakuna haja yoyote ya shirika hili kuuza nyumba hizo na badala yake iweke mkazo katika kujenga nyumba ambazo zitapangishwa kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo yaani *Government Loans, Guarantees and Grants Act 1974 and amendments 2003* inalifanya Shirika la Nyumba la Taifa kulazimika kupata kibali kutoka Wizara ya Fedha hata pale ambapo halihitaji kupata dhamana ya Serikali na pia hata kwa mikopo ya ndani ya nchi; wote tunafahamu rasilimali ambazo shirika hili linazo. Pamoja na kufahamu yote, bado tumeamua kuliweka shirika hili katika urasimu mkubwa wa Kiserikali wa kupata vibali kutoka Wizara ya Fedha bila ya sababu za lazima. Je, Serikali imedhamiria ya kutekeleza ahadi zake katika ujenzi wa nyumba na kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara kama sheria yake inavyolitaka? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi ni lini inatarajia kuanzisha mchakato wa kurekebisha sheria hiyo?

Mheshimiwa Spika, mpango wa uendelezaji eneo la Kigamboni, tangu mwaka 2007, Wizara ilianza hatua za awali za kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni. Mradi huu unahusisha hekta 6500 linaloshirikisha kata tano za Kigamboni, Tungi, Mjimwema, Vijibweni, Kibada na mitaa miwili ya Mbwamaji na Kizani kwenye Kata ya Somangila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka minne imepita, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ibainishe ni lini hasa mradi huu utaanza na michakato ya fidia kwa wananchi imefikia wapi na ni utaratibu upi unaotumika kulipa fidia husika. Halikadhalika Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwepo kwa utaratibu ulio wa uwazi pasi na upendeleo kuhakikisha kwamba wananchi waishio ndani ya eneo la mpango yaani wakazi wa kata zote tano wanabaki kwenye eneo hilo kama ambavyo madhumuni ya mpango unavyoainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina taarifa juu ya mchakato unaofanyika baina ya Serikali na Shirika la Nyumba la Taifa unaohusiana na uendelezaji wa eneo la *Tanganyika Packers* Kawe kama ilivyobainishwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara wakati akijibu swali namba 246, ambapo pamoja na mambo mengine alikiri kwamba katika eneo la Kawe kuna heka 180 ambalo ni eneo la makazi na ambalo halikuuzwa na Serikali kwa mwekezaji. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifahamu kwamba eneo husika bado lina wakazi ambao walikuwa ni wafanyakazi wa Kiwanda cha *Tanganyika Packers* na hatua zozote za kuliendeleza eneo husika lazima uhakikishe unawahusisha kikamilifu wananchi hao ambao wameishi eneo hilo maisha yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya/wakala wa kuratibu bei za pango la nyumba, kutokana na ongezeko kubwa la watu mijini, mahitaji ya nyumba za kupanga yamekuwa ni makubwa sana. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa wenye nyumba kujipangia bei za kodi ya nyumba kwa kadri wanavyoona inafaa wao, kwa kuwa hakuna chombo cha kuwadhibiti. Matokeo yake kodi ya nyumba imegeuka mzigo mkubwa sana kwa wananchi wa kawaida. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke utaratibu utakaotambulika kisheria utakaoweka mwongozo na kuweza kudhibiti gharama za kodi za nyumba kwa ujumla wake. Kwa maana nyingine ni kuanzisha mamlaka ya udhibiti itakayoitwa *Real Estate Regulatory Authority. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA)*, jukumu la Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(National Housing and Building Research Agency - NHBRA)* ni kufanya tafiti, kuelimisha, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora na za

gharama nafuu. Lengo la Wakala ni kuinua na kuboresha viwango vya nyumba kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa na vipatikanavyo hapa hapa nchini jambo ambalo litaongeza ubora wa maisha ya wananchi mijini na vijijini ili kutimiza malengo ya MKUKUTA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka ipewe taarifa ni kwa namna na kiasi gani wakala huu umefanikiwa kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake kwani ujenzi wa nyumba za matope, fito na nyasi bado upo pale pale jambo ambalo linasababisha maisha bora kwa kila Mtanzania kuwa ni kitendawili kwa miaka mingi ijayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu muhtasari wa matumizi ya fedha za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 53,848,061,000; kati ya fedha hizo shilingi 6,423,295,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 25,159,688,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 22,265,078,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2011 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 27,787,178,679 (bilioni 27.7) sawa na asilimia 51.5 ya tengeo la Bajeti kwa mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi 25,658,017,495 sawa na asilimia 92.5 ya fedha zilizopokelewa shilingi 13,226,897,075 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 8,499,539,334 zilitumika kulipa mishahara na shilingi 3,931,581,086 zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze ni kwa sababu gani kati fedha za maendeleo zilizotengwa shilingi 22,265,078,000/= zilizoweza kutumika ni shilingi bilioni 3.9 tu? Ni miradi mingapi iliyokuwa itekelezwe katika mwaka wa fedha 2010/2011 imeshindwa kutekelezwa kutokana na kukosekana huko kwa fedha?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tulikuja na hoja ya kuitaka Serikali iangalie upya mfumo wake wa ulipaji posho na marupurupu lengo likiwa na kuisaidia Serikali kuokoa matumizi yasiyo ya lazima na hatimaye fedha ambazo tunazitumia kulipana posho tuzielekeze kwenye matumizi yenye tija kwa wananchi. Tunashukuru kwamba hatimaye tulichokuwa tukikipigia kelele na kubezwa kimeanza kutekelezwa na Serikali hii hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akiliomba Bunge kuahirisha hoja ya Wizara ya Nishati na Madini ili waende kujipanga upya alitamka yafuatayo naomba kunukuu: "Mheshimiwa Spika, ushauri mlioutoa ni wa msingi sana. Moja mmesema Serikali nunueni mtambo na tusitafute visingizio vya fedha. Kwamba tafuteni kila mbinu huko, tafuteni, kateni posho zenu, kateni vitu gani, nendeni mkatazame magari mnayotumia haya, punguza huko. Tazameni *OC* yenu kikamilifu, mtaona kule ndani yako matumizi mengine ambayo mkiamua kwa dhati mnaweza kabisa mkayaondoa huko, yakaenda yakanunua mitambo ya uhakika, yakawasaidia hata kuongeza uwezo wa mafuta kwa ajili ya mitambo inayotumia mafuta." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumbe inawezekana! Tukiamua kupunguza anasa na starehe na kuwekeza kwa wananchi wetu, inawezekana! Hakika inawezekana! Katika Wizara hii zaidi ya shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya posho (wakati ni bilioni 3.9 tu zilitumika kwa shughuli za maendeleo). Cha kusikitisha zaidi hadi karne hii, kuna posho zinatengwa kwa ajili ya kuwalipia baadhi ya maafisa bili za maji na umeme kwa maofisa wanaostahili. Mfumo huu umesambaa mpaka kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuangalia upya mfumo huu wa kimwinyi na kuacha huduma hizi binafsi zigharamiwe kwa viongozi wa waandamizi (wakuu) tu wa mihimili mitatu ya dola! Tatizo kubwa linalotukumba kama nchi, ni kuendesha mambo kwa mazoea. Lazima tubadilike! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwashukuru tena Wasemaji wa awali katika hoja yetu hii kuanzia Waziri, Mwenyekiti na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Sasa kwa muda nilionao huu maana ni mpaka saa 7.15 mchana naweza kupata watu wanne tu. Atakayeanza ni Mheshimiwa John Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Dunstan Kitandula. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuzungumzia juu ya jambo hili ambalo ni muhimu kabisa, ardhi. Ardhi sio tu ni mali, ardhi ndio pale Watanzania tunapoishi na ninatumaini katika dhana yetu, ardhi ni ya kutumia, labda kule tunakoenda inafaa tuanze kufikiria kama dhana hii inatufaa kwa miaka inayokuja zaidi tukizingatia kwamba ulimwengu wote sasa hivi unaelekea kwenye kupata mali, kumiliki mali. Je, ardhi ni mali, kama tumekubali ardhi ni mali *then* labda tusijiwekeze tu kwa fikra za kiujamaa kwamba ardhi ni ya kutumia lakini ni ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na jambo hili linanielekeza kufikiria kwamba labda pia tuifikishe mahali zaidi unapozungumzia juu ya Katiba mpya, labda tufikirie pia Mamlaka ambayo tumeipa Serikali juu ya kutawala ardhi yetu. Inavyoonekana hata ukisikiliza maoni ya Kambi ya Upinzani hata ukisikiliza changamoto ambazo Waziri amezieleza, ukiangalia migogoro mingi ambayo inatendeka sasa hivi kwa sababu ya ardhi, unaanza kujiuliza je, hivi Serikali kweli ina uwezo wa kuweza kuwagawia na kuwahakikishia Watanzania wote kwamba ardhi yao itabakia kuwa yao na kwamba wale ambao wanataka kuja Tanzania hawatatumia fursa ya udhaifu wa Serikali na taasisi zake, kuwanyang'anya Watanzania ardhi yao! Mimi nafikiri tunakoenda, jambo hili tuanze kulifikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sisi ambao tunatoka Kanda ya Ziwa, ardhi kwetu ndio msingi wa kuondoa umaskini na ndio maana juzi hapa wengi wetu mlituona tunakasirika sana juu ya hatua ya Serikali ya kutangaza bei ya pamba shilingi 1,100/= halafu ikaiteremsha baadaye ikawa shilingi 800/=. Kwa sababu, tunajua ardhi ili upate pamba ni lazima uinunue sasa, watu wanafikiri kwamba ardhi unapewa na Serikali! Ardhi sasa tunanunua, tunakodisha. Kuna watu ambao wanakodisha ardhi, kupata heka moja unalipa mpaka shilingi 40,000/=. Kwa hiyo, kama uwekezaji, hao wanaolima pamba ni wawekezaji wakubwa katika Taifa hili na ndio maana tulikasirika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa mimi kwa niaba ya wananchi wa Bariadi na watu wote wanaolima pamba, bado nafikiri kwamba Serikali haijafanya wanalopaswa kufanya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bei ambayo wanastahili na makosa makubwa ambayo Serikali imefanya, ni kujiingiza na kusema bei itakuwa hivi! Na hawana uwezo wa kuweza kuhakikisha kwamba mambo yote katika soko yatakuwa kama vile wanavyotaka, hili ndio kosa *number one.*

Mheshimiwa Spika, kosa la pili, ni kuwa na Bodi ambayo yenyewe inafuata zaidi matakwa ya wanunuzi! Matakwa ya watu walio na viwanda na ukiangalia kwa ndani zaidi, *i think* kuna ufisadi wa aina fulani fulani ambao unafanywa ambao ningependa Serikali iuangalie kwa ukaribu zaidi na ndio baadhi yetu tunasema kwamba Bodi iache kuwaambia wanaochambua pamba, kuuza mbegu yao kwa shilingi 300/=, hii haina maana! Mtu ananunua pamba kwa shilingi 1,000/= halafu unaambiwa uuze mbegu ambayo ni 60% ya hilo zao kwa shilingi 350/=!

Mheshimiwa Spika, mimi nmechelewa kuja hapa Bungeni, kwa sababu ilinibidi nitafute masoko mpaka Uganda, mbegu inauzwa shilingi 800/=. Mpaka leo naamini kabisa kwamba ukiwa na mbegu ya shilingi 800/=, halafu na pamba hata kama ikienda kwa bei ya chini ikiwa pamba nyuzi, bado mkulima anaweza kupata shilingi 1,100/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru wanunuzi wengi ambao wameanza kunisikia kauli yangu, akina Njalu ambao wapo Bariadi, nawashukuru sana, akina Malongo nawashukuru sana, akina *Alliance* nawashukuru sana, leo bei ya pamba inaelekea kwenda kwenye shilingi 1,000/=.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kueleza kwamba tunahitaji kujua kwamba cha kwanza kabisa ardhi ni mali, ardhi ina gharama na ardhi ndio inakuwa gharama ya kwanza kwa kununua pamba, kwa hiyo, msichezee chezee mambo haya ya pamba! Na kama kwa siasa mimi ni Mwenyekiti wa Chama, mimi ninawashangaa sana watu wa Chama cha Mapinduzi, kuchezea chezea kwa kutumia Bodi, hili jambo la pamba! Hapa kuna kura zaidi ya milioni 14. Kama unataka kuwa na Rais anayetoka Chama cha Mapinduzi, basi Rais huyo awe makini kabisa katika

kuhakikisha kwamba wanaochezea chezea pamba anawafukuza kazi. Wanaochezea chezea pamba kama Bodi, anaifukuza Bodi. Wanaochezea chezea pamba kama vile Mkurugenzi, anamfukuza ili kuhakikisha kwamba kweli yupo makini katika kuhakikisha kwamba anawasaidia watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee, utawala huu wa ardhi bado haujatumalizia migogoro, migogoro ipo kibao. Na siku hizi kwa sababu ardhi watu wengi wanakimbilia kutafuta maeneo ambayo sasa hivi yamekuwa haba na maeneo yamekuwa haba kwa sababu watu tumeongezeka. Tulipoanza Taifa hili tulikuwa watu 8,000,000 leo akinamama, akina baba wamefanya kazi nzuri, tuna zaidi ya watu 40,000,000 sasa hivi. Lakini kila wakati Serikali, inawanyang'anya watu ardhi yao! Aidha, inafanya mapori, au inafanya hifadhi, sasa hivi tumeelezwa na Kambi ya Upinzani, uwekezaji mkubwa wa ardhi kubwa na mambo kama hayo. Sasa sisi hatuna mahali pa kwenda! Sisi kule *Sukuma land* sasa hivi watu tumebanana hivi! Tunatafuta twende tukalime wapi? Na Serikali hii inatuhimiza Kilimo Kwanza, tulime wapi? Ukienda kugusa hapa, mwekezaji! Ukienda ukigusa hapa, mhifadhi! Ukienda ukigusa hapa, hujapata kibali! Twende wapi? Tanzania hii ndio tumepewa na Mwenyezi Mungu tuitumie sisi kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimefurahishwa na dhana moja ambayo Waziri amesema, *Land Bank* (Hazina ya Ardhi), labda sasa wakati umefika, tupime ardhi yetu, tupime vijiji vipya na tumwambie kwamba wewe ukienda kijiji hiki maalum utapata heka kumi, utapata heka 20 na tuziweke ambazo hizi ni za Watanzania tu na tuweke mahali kwamba kama ni mwekezaji aje hapa lakini usimpe bure! Hii biashara ya kumpa bure mtu anayetoka nje, imetoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ardhi kijijini, nina hakika thamani yake siyo chini ya shilingi 5,000 kwa kile eka. Sasa mtu unampa eka 40,000, umempa mtaji wa bure. Huyo mtu akichukua ile hati ya *99 years* anaingia ndani ya Benki, yule Mzungu anakuja hapa na ndala, unampa hiyo hati, anaingia pale ana mtaji wake wa kuanzia, tuuze! Mimi nilipokuwa mwekezaji Swaziland, nilinunua ardhi na nikaweka kiwanda, kwa nini mtu aje hapa apewe tu, hii kupewa tu imetoka wapi? Hii ndiyo inaleta ufisadi na rushwa. Mimi naona imefika wakati sasa tuiangalie ardhi kama mali ili iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuiangalie Sheria upya, Sheria ya sasa ya kutenganisha kati ya Sheria ya *general land* yaani Sheria Na.4 na Sheria Na.5, mimi naona hii inaleta mchanganyiko mkubwa sana. Siku moja nilikuwa nazungumza na Jaji wa Mahakama wa Ardhi, nikamuuliza hivi tatizo ni nini, mbona migogoro imejaa kila mahali. Akasema mojawapo ya tatizo ni Sheria. Nafikiri kuna haja ya kuangalia Sheria hii. Mimi sasa hivi nina mfano mkubwa sana wa ndugu yangu mmoja anaitwa Mwanachene Ikanda, ambaye mtu mmoja alikuwa nje ya kijiji cha Lagangabidili, huyu bwana kuna baba yake alifia pale, kaja kajenga kaburi, kesho yake yuko Mahakamani anasema hapa ni ardhi yangu na maskini huyu sasa amekaa pale miaka na miaka, ana zaidi ya wajukuu 30 lakini kwa kutumia Sheria tuliyonayo sasa anafukuzwa na leo kama Mungu asiponisaidia kumsaidia, nyumba zake zote zinavunjwa, kwa sababu mtu ametumia Sheria tulizonazo ambazo hazikidhi mahitaji ya Taifa letu. Nafikiri kuna haja kubwa sana ya kuangalia hizi Sheria zetu upya na kwa huyu mwananchi Mheshimiwa Waziri kama anaweza kunisaidia akaweza kunihakikisha kwamba atasaidiwa angalau familia yake pale, naomba ndugu yangu afanye hivyo kwa sababu anapenda watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka kuzungumzia juu ya Shirika la Nyumba. Shirika la Nyumba kwa maoni yangu kama kuna kitu ambacho Mwalimu alikabidhi nchi hii ni utajiri mkubwa wa nyumba, pamoja na kwamba Serikali ya Awamu nyingine ilianza kuuza nyumba za Serikali, hiyo tutaishia hapo. Mimi sijaona Shirika ukiliangalia kithamani lililo na pesa nyingi kama Shirika la Nyumba, labda tuliangalie kwa mtazamo huo tusiliangalie kama Shirika ambalo linatoa *service* tu, mambo ya kutoa huduma dunia hii yamekwisha, Mr. Bure alishakufa siku nyingi, siku hizi lazima tuangalie kilicho na thamani lazima ukinunue na ukinunue kwa bei ya soko. Kwa hiyo, mimi naona mtazamo wake lazima sasa hivi tuanze kuufikiria upya. Mimi nafikiri kama Shirika la Nyumba linataka kutujengea nyumba, lina uwezo huo, lina uwezo wa kukopa kwa sababu dhamana ipo. Ukiangalia Upanga yote hiyo ni mabilioni ya shilingi, ni benki gani itakayoifungia mlango Shirika la Nyumba? Kwa hiyo, likielekezwa katika mtazamo huo, nafikiri litaweza kutujengea nyumba nyingi na iuze kwa bei ya soko, mambo ya burebure haya yameshapitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Mwanza kuna magofu mengi sana pale Nyerere Road, kama hawana uwezo wa kujenga, basi wasiwe wachoyo, sisi tunataka Mji wa Mwanza ulio mpya wauze, sisemi watoe bure, wauze baadhi ya magofu pale ili Nyerere Road ile iwe maghorofa, twende juu na tujenga mahoteli ya kufaa, kwa sababu tungependa watalii wengi waanzie Mwanza, kuja Serengeti, badala ya kila wakati kuanzia Arusha kwenda Mwanza. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri ana uwezo kabisa wa kusaidia kwa vile naye anatoka Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, sisi tuna Wilaya mpya ya Itilima, tupeleke sasa wapimaji na wale wapimaji wasitupimie tu nyumba ya Mkuu wa Mkoa, wasitupimie tu mahali ambapo sijui kutakuwa na Halmashauri, watupimie Mji wa Itilima, Lagangabidili pale, ambao utakidhi mahitaji ya miaka 100 inayokuja. Huu ndio udhaifu wetu, tunatanguliwa na watu baadaye ndio tunakuja kurekebisha, ndiyo maana kuna makazi holela. Sasa *with his experience* Mheshimiwa Waziri hebu afanye hivyo sasa Serikali itangulie, wapime ili watu wakae katika makazi ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Katika ambao hawajachangia mara moja leo alikuwa peke yake. Sasa nakuja kundi la waliochangia angalau mara moja, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na kwa muda tulionao, nafikiri Dunstan Kitandula atakuwa wa mwisho.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuionyesha tangu wameteuliwa kuwa Mawaziri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wote tumekuwa mashahidi, wameingia kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya, pale ambapo walianza Dar es Salaam kwa kushughulikia maeneo yale ya wazi ambayo yalikuwa yamevamiwa na baadhi ya wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpongeze sana Waziri na nimtie moyo kwamba aendeleze juhudi hizo ambazo ameanza nazo. Pamoja na vikwazo ambavyo ameanza kukutana navyo, lakini tupo nyuma yake ahakikishe kwamba maeneo yote ya wazi ambayo yalichukuliwa na baadhi ya watu yaweze kurejeshwa kwa misingi ya maendeleo yale yaliyokuwa yamekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hasa katika Kitengo cha Mipango Miji. Maafisa Ardhi katika Halmashauri na Miji yetu pamoja na hawa wenzetu wa Mipango Miji, ni vyanzo vya migogoro na matatizo makubwa katika Halmashauri na Miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Watu wa Mipango Miji wanaelewa kabisa kwamba baadhi ya maeneo ilikuwepo *master plan* toka zamani, lakini ukienda kuangalia sasa unakuta maeneo yale yote ambayo yalikuwa ya wazi, yaliyokuwa yametengwa kwa shughuli maalum, ama ni kwa ajili ya michezo ya watoto, ama ni kwa ajili ya shughuli maalum ambazo zitatokana na shughuli za Kiserikali, hawa Maafisa Mipango Miji wao ndiyo wamekuwa vyanzo vya kwenda kugawa maeneo hayo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara ya Ardhi, hususan Waziri wetu ambaye ni mwanamke, ameanza kazi vizuri, niombe maeneo yote hayo ambayo yalikuwa ni ya wazi, basi yaweze kuchukuliwa hatua na kuhakikisha kwamba yanarejeshwa, hata kama kulikuwa na nyumba zilizoota kama uyoga, zibomolewe ili maeneo hayo yaweze kutumika kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutochukua hatua au kusema kwamba labda hayo maeneo tayari wameshachukua, wamejenga majengo yanaonekana yana gharama kubwa, tutaendelea kuwapa nafasi watu hawa wenye uwezo mkubwa wa kifedha, wanaokwenda kuwarubuni hawa

Mipango Miji, kuendeleza uovu wao maana mtu mwingine wa kawaida ambaye huna uwezo wa fedha huwezi kumwendea Afisa Mipango Miji akakupa eneo ambalo ni la wazi. Wanaofanya hivyo ni wale watu ambao wana uwezo wa kifedha. Sasa ili kuwaonyesha kwamba Serikali iko imara basi tuhakikishe kwamba maeneo yale yote yanachukuliwa na kurejeshwa na kuhakikisha kwamba yanafanya shughuli zile zilizokuwa zimepangwa au zimekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niendelee kuzungumzia suala hilohilo la upande wa Mipango Miji. Ukiangalia kwenye Miji yetu, hizi nyumba ambazo zimejengwa za watu wa kawaida, sasa hivi unakuta vichochoro vyote vimezibwa, vimegeuka ni nyumba za biashara bila kujali kwamba vichochoro hivyo vinavyozibwa endapo itatokea janga la moto, nyumba zote zitaungua. Hawa watu wa Mipango Miji wanalijua tatizo hilo, inapofika kipindi cha uchaguzi, hata sisi viongozi wa kisiasa ni matatizo, badala ya kuwasaidia wenzetu wa Mipango Miji wale ambao wanakuja kufanya kazi yao na wamepewa maelekezo kwamba hebu mkahakikishe vichochoro vyote vile vinaachwa wazi, tunaanza kusema jamani mnajua sasa hivi kipindi cha uchaguzi, tukifanya hivyo tutakuwa tunaharibu. Ndugu zangu, naomba kama kweli sisi Serikali ya CCM tunataka kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuhakikishe kwamba maeneo yote yale ambayo hayaruhusiwi, hayashughulikiwi kwa namna nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitolee mfano wa pale Morogoro. Nimekaa pale Morogoro kama Katibu wa CCM wa Mkoa, karibu vichochoro vyote vimekuwa na maduka. Sasa nikuombe Waziri, kwa Miji yote, wale waliofanya vichohoro maduka, yabomolewe ili vichochoro vile vifanye kazi yake kama vilivyokuwa vimekusudiwa. Najua watu wanafunga vichochoro labda wanasema majambazi wanapita, wewe umepangiwa kila siku kwamba jambazi atakuja nyumbani kwako? Niombe vichochoro vyote vifunguliwe ili kusudi maeneo yale yawe wazi, Mji haujulikani umekaa vipi, ni mchafu kutokana na kuziba vile vichochoro.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la ardhi. Ni ukweli usiofichika, mwanamke ndiye ambaye analiongezea pato Taifa hili. Sasa niiombe Serikali angalau basi iweze kuweka mpango vizuri wa kuhakikisha kwamba unawapatia vipaumbele wanawake kwa kuwapatia sehemu ya ardhi kwa maana ya kupima ardhi na kuwapa mashamba ili waweze kumilikishwa. Ziko mila na desturi za baadhi ya makabila hawataki wanawake wamiliki ardhi na kwa bahati mbaya itokee mwanamke huyo mwanaume wake amefariki, basi hiyo ardhi inachukuliwa na ndugu wa mwanaume. Sasa niombe ndugu zangu iwepo Sheria ambayo itahakikisha kwamba mumewe akifariki ardhi ile iwe ni yake badala ya ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niombe Serikali iangalie utaratibu wa kuweza kuwasaidia wanawake wale ambao wanaweza kuitumia ardhi kwa kuwa dhamana kwa ajili ya kupatia mikopo ili iweze kuwasaidia kujiinua kiuchumi. Kama tunavyozungumza kwamba ardhi ni mali, kama ardhi ni mali, basi tuwasaidie wanawake hawa ili wapate dhamana ya ardhi waweze kupata mikopo ambayo itawasaidia katika kuendesha shughuli zao ili waweze kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la hawa wawekezaji. Ni kweli tunahitaji wawekezaji lakini sasa imefika kipindi ambacho inabidi tuwe na ukomo wa kuwapa hawa wawekezaji ardhi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu walio wengi mpaka sasa hivi bado hawajawa na ardhi ya kutosha, sasa sisi kama Serikali tujitahidi katika hili kuhakikisha kwamba hatuwapi wawekezaji ardhi kubwa, kwa maana ya maekari kwa maekari. Hasa tukizingatia hili suala la Afrika Mashariki na Kati, watu wameanza kuingia huku kwetu, basi wenzetu watakachokimbilia zaidi ni ardhi, tuwaelimishe wenzetu kwenye vijiji kuhakikisha kwamba hawaitoi hiyo ardhi kwa wawekezaji maekari na maekari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba wawekezaji hawa ni vizuri kukawa na utaratibu, wengi wao huwa wanakwenda moja kwa moja kupitia kwenye Wizara ya Ardhi, sasa inatakiwa tuagize kule maana anakuja na vijinoti tu anawaendea wa Serikali wa Vijiji au Mtendaji wa Kata, wanamueleza kwamba sisi tumetoka kule, kinoti hiki hapa, tunahitaji ekari 2,000, 3,000. Sasa Mtendaji wa Kijiji au Mtendaji wa Kata au Serikali ya Kijiji wakishaona ki-*note* kutoka juu Taifani hawana pingamizi zaidi ya kusema wanawapimia eneo hilo. Sasa niombe na ninyi tuachane na

tabia ya kuandika vijinoti kutoka juu kuagiza na kuwaelekeza viongozi wa Serikali za Vijiji kwamba wawagawie ama wawapimie maeneo hayo na hatimaye kuwamilikisha ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba maadamu nimegongewa hiyo kengele ya kwanza, niseme haya niliyokuwa nayo yanatosha, niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumzia maeneo mawili, Nishati na Madini na Wizara ya Ardhi. Jioni nilipata simu kutoka kwa mama mzazi anaitwa Bi. Siti Kilungo Mwihiyawe.

**SPIKA**: Yaani mama yako wewe?

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Eeh! Mama mzazi, akaniambia mwanangu mbona umechangia kwa sauti kubwa sana, mimi sikujielewa, akaniambia angekuwa hai baba yako, asingependa, angependa uchangie kwa sauti ya taratibu lakini watu waelewe, kwa hiyo sauti yangu leo itabadilika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana wapigakura wangu wa TMK kwa imani kubwa na mapenzi makubwa kwangu. Wamekuwa wakipata tabu siku hizi, sasa nisiposema kidogo wanaweza wasielewe. Wamesikia mambo mengi ya *DDC*, niwahakikishie huko sipo, mwaka 2009 mwenye dhamana, Mama Celina Kombani aliunda Tume ambayo ina taarifa zote za *DDC*. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi sipo, hizo ni kelele za mlango ambazo hazimzuii mwenye nyumba kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja Kurasini. Nilichangia wakati wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri anakumbuka, ndugu zangu wa Kurasini wana matatizo kwelikweli na Waziri amezungumza kwamba ule mpango wa Kurasini ulianza toka mwaka 2006. Waheshimiwa Wabunge hebu tuangalie wananchi hawa wanavyopata tabu toka mwaka 2006 leo mwaka 2011 watu hawajalipwa fidia, wanazuiwa nyumba zao kutengeneza hata choo!

Mheshimiwa Spika, nilipata taarifa jana zimenisikitisha kweli, Bwana Afya anapita Kurasini, wale ambao vyoo vyao vibovu anawatoza faini ya shilingi 40,000 mpaka shilingi 50,000, nimesikitika kwelikweli. Nilitamani yule Bwana Afya nimfukuze kazi, nikasema taratibu na sheria haziniruhusu, nisije nikafukuza kazi watu barabarani kumbe taratibu haziniruhusu, nikamuomba Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kweli lakini kilichonisikitisha zaidi ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 25 naomba ninukuu, inasema:-

"Nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa eneo la mradi, ana maana Kurasini, kwa uvumilivu na ushirikiano wao katika utekelezaji wa miradi ..."

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kuelewa hawa watu wanasubiri pesa zao ili waweze kuondoka lakini Mheshimiwa Waziri anasema anawashukuru kwa uvumilivu. Mimi kwa sababu nilichangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilitarajia leo Mheshimiwa Waziri angesimama hapa angesema Bunge likiisha anakwenda kuwalipa hawa watu lakini uvumilivu gani usiokuwa na mwisho? Wale watu wanateseka, hebu tujifikirie tungekuwa sisi, ni bora kama ule mradi hatuuwezi tuwaambie wananchi wajenge nyumba zao, waendelee kuishi kuliko kuendelea kuwatesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napata wasiwasi sana tunapozungumzia mradi wa Kigamboni na tukionyeshwa picha nzuri. Kama wananchi wa Kurasini, mradi wa kuendeleza bandari toka mwaka 2006 mpaka leo wananchi wale hawajalipwa, wanapata taabu kwelikweli na cha kusikitisha zaidi, mimi Temeke nimeshinda kwa kura nyingi 58, lakini Kurasini sikushinda na sababu ni hiyohiyo ya ule mradi.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda na Waziri Mkuu tarehe 14/3/2009, Waziri Mkuu akaagiza na anayo haki ya kuagiza kwamba jamani eeh, walipeni hawa wananchi haraka na jamaa wa Mabwawani pale ambao mwanzo walilipwa ukiondoa hawa ambao hawajalipwa kabisa lakini ukiambiwa malipo yenyewe ni vichekesho kwani mtu mwenye msingi kalipwa shilingi 300,000/=, mwenye nyumba kalipwa shilingi 1,800,000/= mpaka shilingi 4,000,000/= ambayo kwa kweli siyo haki, hazitoshi. Rais aliagiza tarehe 27/10/2010 kwamba walipeni wananchi wa Kurasini lakini mpaka leo wananchi wale hawajalipwa. Waziri mhusika alikwenda akakutana na wananchi na akasikitika sana na akawaambia anaharakisha kuwalipa lakini mimi nataka kusema ukweli kabisa kwamba Waziri hana tatizo wala Naibu Waziri hana tatizo lakini kilio cha wananchi wa Kurasini ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, hata lile eneo la mradi hajafika, tofauti na Mama Salome Sijaona. Ni tatizo kwelikweli, si vema kusema watu lakini niseme ukweli Katibu Mkuu, huyu Bwana Mkubwa kama ataendelea na Mama Tibaijuka kazi yote nzuri anayofanya Mama Tibaijuka itakuwa ni bure.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa mpango mzuri wa *National Housing,* kwanza nipongeze uongozi wa *National Housing.* Vijana wana uwezo na ni wachapakazi ukiondoa wale wazee wa zamani akina Komba, Malisa na Zedieli, lakini ndiyo waliofanya mambo yote makubwa. Yale maghorofa mazuri tunayoona Dar es Salaam, walikuwa wazee hawa nao walikuwa wachapakazi, wana nguvu na uwezo kwa hiyo wanashindana.

Mheshimiwa Spika, nachosema ni lazima maamuzi ya Bunge yaheshimike, tuliamua kwenye Bunge hilihili mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011 na kitabu kiko hapa kwamba baadhi ya nyumba za *National Housing* mfano nyumba za Keko, Chang'ombe mafleti na mimi ni mkazi wa pale, *Block No.1,* niseme mapema Mheshimiwa Spika usikie, Tandika Maghorofani, Ilala Kota, Mafleti ya *Breweries, Flats* za Ubungo na nyingine nyingi Tanzania tulisema tutawauzia wananchi walioishi mle kwa muda mrefu ili na wao waweze kujikimu. Mambo ya kushangaza leo mpango ule umekufa kabisa lakini sasa sijui kama Mheshimiwa Waziri wamepitia vitabu vya nyuma wakaona maamuzi ya Bunge au wameisikiliza tu *Management* na *Board* ya *National Housing*? Mimi nawaomba sana wapitie vitabu vya nyuma waangalie maamuzi ya Bunge, leo tulikuwa tunatarajia nyumba zile tutakuwa tumeshawakabidhi wananchi.

Mheshimiwa Spika, kengele ya pili inaweza ikanililia basi niseme tu mapema bajeti hii mimi siiungi mkono mpaka niambiwe wananchi wa Kurasini wanalipwa lini na wananchi wa Maghorofani na nyumba zote za *National Tanzania* tulizosema na tusione haya katika hili, mbona yale majumba mazuri tuliuziana? Kuwauzia hawa wananchi tunasita nini?

Mheshimiwa Spika, naamini leo nimeongea sauti ya chini na Mama mahali alipo moyo hautakwenda juu, siungi mkono hoja hii mpaka nipate majibu ya watu wa Kurasini na watu wa Maghorofa na wale wengine wenye nyumba ndogondogo. Haiwezekani Mheshimiwa Waziri, akisimama hapa atamke kwamba mradi huu hauwezekani, wananchi waendelee kujenga nyumba zao. Hata wale watu walionunua vile viwanja wako akina *Camel Oil* na *Oil Com,* vile viwanja vya mwanzo hamjawapa hati zao wala hamjawakabidhi mali yao, sasa sijui vipi. Hawa waliouza hamjawapa pesa zao wale walionunua hamjawapa hati zao, sasa sijui tunakwendaje?

Mheshimiwa Spika, leo mmeleta bajeti nzuri, kitabu hiki kidogo, tulikuwa tunauliza kitabu kidogodogo hiki ndiyo kimejaa mambo yote ya shida za ardhi ya nchi hii? Tunasema kinatosheleza, kina maneno mazuri lakini hofu yangu pamoja na kwamba asili yangu ni Temeke lakini asili yangu ni Ilala pia Kigamboni kunanihusu. Yule Bi. Siti, Baba yake Chekimea alipotoka Tunduru alifikia Tuangoma ndipo alipomkuta yule Mama wa Kizaramo, Mama yao Bi. Siti. Kwa hiyo, napata hofu sana na huu mradi wa Kigamboni kama utafanikiwa. Kama hawawezi tusiwasumbue wananchi tena. Hofu yangu tunaweza sasa hivi tukauchangamkia ikiisha Awamu ya Nne na mradi huu umeondoka. Kwa hiyo, tuwaambie wananchi ukweli.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nisije nikapigiwa kengele ya pili lakini siungi mkono mpaka nipate majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wa kumshukuru sana ni Mama yako maana umesema kwa utaratibu, tumekuelewa lakini kubwa ni kwamba kama akina Bibi hao wanasikiliza basi mjue mnaposema semeni kwa makini. Tunaendelea na Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Mkinga kwa imani ambayo wanaendelea kunionyesha kila uchao, niwaahidi tu kwamba nitawapa utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Prof. Tibaijuka kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara yake lakini vilevile niwapongeze vijana wenzangu wa Shirika la Nyumba, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi kifupi ambacho wamepewa dhamana ya kusimamia Shirika lile. Tumeanza kuiona tofauti, tumeanza kuona mabadiliko chanya katika Shirika lile. Utendaji wao mzuri ni uthibitisho tosha kwamba vijana wanaweza, tunachoomba tupewe nafasi ili tuweze kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya sana na kwa masikitiko makubwa pamoja na pongezi hizi nilizozisema, kwa moyo mzito sana niseme nasikitika kwamba sitaiunga mkono hoja hii. Sitaiunga mkono hoja hii kwa sababu watu wa Mkinga wameniambia nisiunge mkono. Kwa nini watu wa Mkinga hatuiunga mkono hoja hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga umekuwa ukisifika kwa muda mrefu kwa zao la Mkonge, tumeingiza mapato makubwa sana katika nchi yetu kupitia zao la Mkonge katika miaka ile ya 1960 lakini wakati tukipata sifa ile, tulikuwa tunapata maumivu makubwa kwa sababu 60% ya *arable land* ya Mkoa wa Tanga ilikuwa inatumika kwa kilimo cha Mkonge na Chai. Wakati ule maumivu hayakuwa makubwa kwetu kwa sababu ajira ilikuwa inapatikana, zao la Mkonge lilikuwa linaingiza mapato kwa nchi yetu kwa hiyo maumivu hayakuwa makubwa. Leo hii Mkonge umeshuka, mashamba yamekuwa mapori, bandari yetu haifanyi kazi, reli imekuwa historia, inafikia mahali ndugu zangu Wagosi wa Kaya wanauliza Tanga kunani? Uchumi umeporomoka, ni kwa sababu hiyo hatuungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hatuungi mkono hoja hii kwa sababu sasa tuna maumivu mengine yanakuja mbele yetu, Wizara imeamua kugawa hekta 25,000 za Wilaya ya Mkinga kwa mwekezaji mmoja akalime Jiotrofa. Hii haikubaliki hata kidogo! Haikubaliki kwa sababu sisi wenyewe wananchi wa Mkinga tuna *pressure* ya ardhi, eneo la Mkinga ni hekta karibu 250,000. Tayari sasa hivi tuna wawekezaji takribani 11 waliogawiwa ardhi katika Wilaya ya Mkinga ambao hawa wanachukua takribani hekta 25,000 lakini kama hiyo haitoshi leo tunaongezewa mwekezaji mwingine ambaye peke yake anapewa hekta 25,000. Nasema hii si haki na hatukubaliani nayo. Wakati haya yanafanyika si viongozi wa Wilaya wala uongozi wa Mkoa ambao tumeshirikishwa kwa kina katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, ninayo barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara yake, inayoidhinisha ugawaji wa hekta elfu ishirini na tano, mia moja na sitini na zaidi lakini wakati barua hii ikiagiza hivyo, ipo barua nyingine kutoka kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI inayozuia ugawaji huo. Hawa ni Watendaji Wakuu wa Serikali, wako katika Serikali moja ya Chama cha Mapinduzi lakini wanatoa maamuzi yanayogongana. Ushauri uliotolewa na Katibu Mkuu wa TAMISEMI ulikuwa ni mzuri sana, naomba nisome baadhi ya maeneo, anasema:-

“Ili kuwezesha Kampuni ya Arkadia kupatiwa ardhi iliyoombwa, maelekezo yafuatayo yatolewe kwa ajili ya utekelezaji huo kwamba Kijiji cha Daluni Kibaoni kiliganyika mwaka jana na kuanzisha vijiji vingine viwili. Vijiji hivyo bado vina mgogoro wa mpaka, shughulikieni migogoro hiyo. Mara baada ya kutatua migogoro ya mipaka hiyo, tayarisha matumizi bora ya ardhi hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kisha kampuni ya Arkadia ielekezwe kupeleka upya maombi kwenye Vijiji hivyo. Kwa sababu za kiusalama, sitisha maombi ya ardhi kutoka kwa wawekezaji wa kigeni walioomba ardhi katika Vijiji vya Mwakijembe na Mbuta ambavyo vipo katika mpaka na Kenya. Ardhi iliyoombwa na Kampuni ya Arkadia haiwezi kutolewa yote kwa mara moja kutokana

na maombi ya kampuni hiyo kuwa katika hatua tofauti za kushughulikiwa katika Vijiji mbalimbali. Hivyo, ardhi iwe inatolewa kwa jinsi itakavyokuwa inapatikana baada ya kupanga mpango mzuri wa matumizi ya ardhi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni ushauri na ni agizo kutoka kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI akimuagiza Mkurugenzi wangu na anauelekeza uongozi wa Mkoa wa Tanga. Wakati sisi tunajiandaa kutekeleza haya, tayari linakuja agizo hili kwamba wawekezaji hao wa Kampuni ya Arkadia wameshapewa ardhi hekta 25,000. Hatutakubaliana na hili! Hatusemi hivi kwa sababu hatutaki wawekezaji, la hasha!

Mheshimiwa Spika, watu wa Mkinga tuna uzoefu wa kukaa na wawekezaji. Tunayo mashamba 10 ya wawekezaji mbalimbali. JKT Maramba wana hekta 2,416, *Mwele Seed Farm* wana hekta 954, *Lugongo Sisal Estate* wana hekta 3,831, Mtapwa wana hekta 476, Kauzeni wana hekta 190, Mjesani wana hekta 9,081, *Mavovo Farm* wana hekta 1,503, Kwamtili wana hekta 700, *Manza Estate* wana hekta 386 na Mkomazi au *Moa East* wana hekta 6,292. Kwa hiyo, huu ni ushahidi tosha kwamba tunawapenda wawekezaji na tumekuwa tukiishi vizuri na wawekezaji hawa lakini sasa hili la mwekezaji mmoja kumpa hekta 25,000 bila maridhiano na wanavijiji husika na uongozi wa Wilaya si sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kinachouma zaidi, wapo wafugaji Wamasai ambao wamekuwa wakiomba maeneo waliyonyang'anywa yakaitwa ni maeneo ya hifadhi, wamewekeza kwenye maeneo yale, wamechimba visima na malambo kwa nguvu zao wenyewe, wamepoteza karibu shilingi milioni 10, suala lao ni la miaka mitano iliyopita. Yupo mwekezaji Magodi ambaye ni Mmasai ameomba ekari 3,000 amenyimwa na kijiji kwa sababu kijiji hicho hakina ardhi lakini anapokuja mwekezaji Muitaliano anapewa ardhi ile bila ya Serikali ya Kijiji kushirikishwa. Hii si sahihi!

Mheshimiwa Spika, hivi tunaitakia mema nchi yetu? Vijiji viwili kati ya hivi vinavyotajwa viko kwenye mpaka na Kenya? Hivi ni nani Serikalini asiyejua kwamba Wilaya ya Mkinga ina *porous border* kwamba tuna tatizo la watu kuingia hovyo kwenye nchi yetu katika ukanda ule? Tuna tatizo la Wasomali na Waethiopia kwa kupitia maeneo ya Bahari na kupitia maeneo haya ya Kenya wanapita kila uchao bila matatizo? Kama hiyo haitoshi leo tunakwenda kumpa mwekezaji maeneo hayo ya mpakani. *Are we serious?* Watu wa Mkinga wameniambia nisiunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maeneo tunayopigiwa kelele kwa njaa ndiyo maeneo haya leo ambayo watu hawa wanaporwa ardhi hii. Kichekesho zaidi ni kwamba wapo watu katika Wizara wanampotosha Mheshimiwa Rais. Wanataka kumfanya Mheshimiwa Rais achukiwe na watu wa Mkinga, watu wa Mkinga wanaipenda Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo maana siku zote tumekuwa tukiiunga mkono Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hatutakuwa tayari kuona watu wachache wanavuruga sifa hii ya watu wa Mkinga. Tunaomba alishughulikie suala hili ili watu wale waendelee kuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja hii kwa sababu haya ndiyo matakwa ya wananchi wa Mkinga, wananchi wa Tarafa ya Maramba ambao leo hii ni miongoni mwa watu ambao tunawaambia tunawapokonya ardhi, leo hii wanaishi kwa shida. Walikuwa wanalima kwenye mashamba ya JKT, tumewazuia. Serikali ya Wilaya inajipanga sasa kuwahamishia wananchi hawa na kuwawezesha walime katika maeneo ambayo leo yanachukuliwa anapewa mwekezaji, tunakwenda wapi? Kwa nini Serikali haizungumzi kwa kauli moja? Kwa nini Watendaji Wakuu wa Serikali hiyohiyo wanatofautiana? Naomba mlishughulikie suala hili ili tusije tukaleta matatizo. Tunaomba uamuzi ule wa kwanza wa kusema kwamba matumizi bora ya ardhi yafanywe halafu Serikali ya Wilaya na Mkoa viangalie ni kwa jinsi gani inaweza kumgawia mwekezaji huyu ardhi yafuatwe. Hatutakuwa tayari kuona tunaendelea na maumivu ya kupokonywa ardhi wakati sisi wenyewe hatuna ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Rais alipokuja katika Wilaya yetu alitoa agizo akasema, sasa watu wa Mkinga anzeni kuingia kwenye kuzalisha zao la Kakao. Maeneo ambayo tumeyapanga kwamba tuwashawishi watu wetu wawekeze katika kilimo cha Kakao ndiyo maeneo hayo ambayo Wizara yake wanayapora. Hivi ni nani huyu anayeweza kukinzana

na kauli ya Mheshimiwa Rais? Mheshimiwa Rais ameagiza sisi tunajipanga kutekeleza, watu ndani ya Wizara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninyi nyote ni mahodari wa kuzungumza, kuna dakika kumi ambazo hazitoshi kwa mtu mmoja kuzungumza kwa hiyo itabidi nisitishe shughuli hizi mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja iliyo mbele yetu. Msemaji wetu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Antony Mbassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Modestus Kilufi.

**MHE. ANTONY G. MBASSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu, kati ya vitu ambavyo vinasumbua wananchi kimojawapo ni ardhi. Ardhi imekuwa ikileta kero kubwa sana kwa wananchi kwa sababu kubwa mbili. Moja ni kwa Serikali kupitia Watendaji wake kutofanya kazi inavyostahili kwa maana ya kutambua ardhi, kuipima, kuibinafsisha au kuimilikisha na hatimaye kuipangia matumizi husika. Kwa upande wa pili ni kwa wananchi husika kutokupewa elimu sahihi kuhusu matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi migogoro hii imekuwa ikisumbua sana wananchi. Kati ya vitu ambavyo mwananchi wa kawaida anaweza akajivunia ni suala zima la ardhi lakini ardhi hii bado mwananchi huyu hajui matumizi yake kwa maana ya kwamba hajapewa elimu sahihi kuhusiana na matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja hii, mimi naomba niongelee suala zima la kuendeleza makazi tuliyonayo. Leo hii tukiangalia sehemu nyingi katika nchi yetu tunapata migogoro mingi ya ardhi kutokana na miradi ambayo inakuja kuanzishwa katika maeneo ambayo tayari yana wananchi. Miradi hii inamkuta mwananchi huyu akiwa eneo husika, matokeo yake inapoanza wahusika hawajali kwamba huyu mwananchi alikuwepo hapa na kwa sababu mradi huu unakuja basi anastahili fidia halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi ardhi waliyokuwa nayo haipimwi na kama ardhi haijapimwa haiwezi kuwa na thamani yoyote ile. Wananchi wetu wanahangaika kwa umaskini lakini kwa kweli hawapaswi kuwa maskini. Watu wameshindwa kupata mikopo kwa sababu wana vitu ambavyo haviwezi kuwekewa dhamana. Ardhi hii ingekuwa imepimwa mwananchi huyu angeweza kujikomboa kutokana na umaskini huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi tunayoipata ni kutokana na wataalamu wetu kutotambua ardhi hii ina thamani gani. Leo hii Jimboni kwangu wananchi wana mgogoro na Halmashauri kwa sababu ya ardhi. Wananchi wamepewa eneo la kujenga vibanda wakati watu hawa walikuwepo mahali pale siku nyingi. Wameanza kujenga vibanda kwa kutumia bati, lakini Halmashauri ilipokuja kupima bado mkataba uliosainiwa ambao waliingia na Halmashauri, hauoneshi kwamba ipo siku vibanda hivyo vitarudi kwa Halmashauri. Halmashauri ilipokuja kudai ushuru wananchi wanayo haki ya kuonesha zile hati zao zinazoonesha kwamba viwanja vile walivyopewa ni vyao. Sasa hapa tunayemlaumu ni nani? Je, ni huyu Mtendaji wa Serikali au huyu mwananchi aliyekutwa mahali pale na akagaiwa kiwanja kile? Sasa tuiombe Serikali ifanye mbinu

endelevu kutambua maeneo haya na kupanga mipango ya baadaye ya maendeleo, kwa kutambua kwamba wananchi hawa ipo siku watahitaji kulipwa fidia inayostahi na kama ndivyo basi mikataba iwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi sasa hivi tuna Miji au *centers* zinazokua lakini hazipimwi ingawa wataalamu hao wapo. Idadi ya watu katika *centers* hizi inaongezeka, tunapohitaji kuboresha miudombinu katika *centers* hizi inakuwa ni tatizo la msingi na ni kubwa sana na ndiyo tunaanza miradi ya bomoabomoa. Sasa tutawezaje kuepuka adha hii kama hatuwezi kufanya matumizi endelevu ya ardhi mapema iwezekanavyo kwa kuipima na kuwapa wahusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu, ninazo *centers* zinazokua mfano, *center* ya Kabindi, sasa hivi kuna mwingiliano mkubwa sana, wafanyabiashara ni wengi, watu wengi wanajenga lakini pale hakuna chochote, hakuna hata kipande ambacho kimepimwa. Sasa niiombe Serikali iweke msukumo ili kusudi watu hawa wapimiwe maeneo na yatambuliwe ni yapi yatakuwa maeneo ya wazi, maeneo ya kujenga na maeneo ya viwanda. Si hapo tu, kuna *center* kama Nyakanazi, Nyakahula ambazo ni *centers* zinazoinukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee migogoro ya wakulima na wafugaji. Hii imekuwa ni migogoro ya mara kwa mara lakini tunaipata kwa sababu wananchi hawa hawaoneshwi maeneo yao, hawapimiwi eneo la kufugia, hawapimiwi eneo la kulima na matokeo yake wanaingiliana na hapo ndiyo unapotokea ugomvi mkubwa sana na mbaya zaidi maeneo mengine yanapakana na hifadhi. Ni wazi kwamba mchungaji anahitaji eneo lililo na nyasi lakini kwa sababu hakuna mpaka aliooneshwa, atafugia popote pale na siku ya siku atakuja kukamatwa, atatozwa faini na faini nyingine hazifiki ndani ya Halmashauri zinaishia kwenye mifuko ya watu. Sasa namna hii tunawasababishia wananchi wetu mateso ambayo hawastahili kuyapata. Tukitenga maeneo haya, naamini ardhi yetu tutaitunza vizuri, itakuwa ya thamani na itaweza kuzalisha kile kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo haya kutokea, tumeeleza mara nyingi lakini hakuna juhudi zozote zinazochukuliwa, sasa sijui tutaboreshaje? Tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa karibu sana na atupe majibu, hususani wale wote tunaotokea Mkoa wa Kagera ambao tunazungukwa na ile Hifadhi ya Burigi. Matatizo ya wafugaji yameelezwa siku nyingi, ni matatizo ambayo yamekuwepo siku nyingi sana, wamekuja wafugaji wanaotoka nchi za nje, wamefugia mle, maeneo yale yote yameshaharibiwa sasa na mwananchi huyu wa kawaida akijichanganya mle na yeye anapata shida ileile, sasa tufanyeje? Tunaomba Serikali itusaidie hili tafadhali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi katika nchi yetu yamejaliwa sana kuwa na madini na sehemu nyingi tumeongea suala zima la wawezekaji ambao wamekuwa wakichimba madini haya, ambao wamegeuka kuwa sasa ni adui wa mwananchi wanayemkuta kwenye maeneo haya. Ukitafuta hapa chanzo ni nini, hawa watu wanapokuja na kutengewa maeneo huyu mwananchi anakuwa hapewi eneo lake la kuchimba, hapewi eneo lake la kufanyia shughuli zake na matokeo yake Vijiji vingi vimekosa huduma za hawa wawekezaji kwa sababu havina hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa nimeuliza swali kuhusu mgawanyo wa Kata, Vijiji na Tarafa lakini bado Vijiji hivyo vilivyogawanywa havina hatimiliki. Sasa huyu mwananchi anakuwa ni mtu wa kufukuzwa tu muda wote kwa sababu hana kitu kitakachomlinda na atakachoweza kusimamia katika mazingira yale aliyomo. Suala hili kwa kweli ni kero kubwa sana, tuombe Waziri anayehusika aje na mpango mkakati wa dhati, kuhakikisha kwamba Vijiji hivi vinapata hatimiliki ili wananchi waweze kuishi maisha yaliyo bora, siyo ya kufukuzwa tu kana kwamba wao ni wakimbizi ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tunaloliongelea kuna watu huko sasa hivi wanapata shida sana. Kutokana na mwingiliano wa watu, watu hawa wanashindwa kueleweka wao wanapatikana katika Halmashauri ipi au Kata zipi kwa sababu wako mpakani na sehemu walizomo hazijapimwa vizuri. Hili linapelekea hata Wakuu wa Wilaya wanapokwenda kwenye

maeneo husika na kutoa amri husika, zinashindwa kutekelezeka na ndiyo maana tunapata hii migogoro ya watu. Utasikia eneo fulani wamegoma, sijui imekuwaje, lakini suala hili lingewekwa wazi nafikiri lingeweza kuwasaidia wananchi wakaishi vizuri na kila mmoja akatimiza wajibu wake na kutii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba Wizara husika iangalie suala hili kwa sababu sekta ya ardhi ni mtambuka, ijaribu kushirikiana na Wizara nyingine zilizopo, wafanye kazi kwa pamoja, wawaondolee wananchi wetu hawa matatizo haya ya kila siku. Iwapo haya niliyoyasema yatafanyiwa kazi, ninaamini haya yanayotokea huko kote ambayo tunayasikia hapa Bungeni, hayatakaa yajitokeze kwa sababu kila mmoja atajua eneo lake likoje, atajua thamani ya shamba lake ikoje na hata akienda kuuza atajua auze kwa shilingi ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Antony Mbassa, na kwa kweli sauti yako ulivyokuwa unatoa *message* ya kuchangia, ni kama mtumishi wa Mungu kabisa. Nakushukuru sana.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mbarali, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuwa sikivu kwa kilio cha wananchi wa Mbarali, hasa kupitia Waziri Mkuu alipotangaza kwamba wale wananchi hawatasumbuliwa tena na uhamisho ambao kwa kweli ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Mbarali na mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maliasili, Ardhi na Mazingira, kwa kuona umuhimu wa kutatua migogoro hii ya ardhi katika nchi hii wakiwa wameanzia kwangu Mbarali. Walikuwa ni mchango mkubwa sana wa kuona kwamba wananchi wanabaki na ardhi yao na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nimshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kuungana na Kamati pamoja na Serikali, kuona kwamba wale wananchi wa Mbarali ardhi yao isingefaa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa nimekosea sana kama sitashukuru uongozi wa *TANAPA* kwa kukubali kwamba ni kweli *TANAPA* haiko kwa ajili ya kuwa na migogoro na wananchi, inataka mahusiano ya karibu na wananchi na hivyo iko tayari kufanya mahusiano ya karibu na wananchi wa Mbarali na siyo kugombana kwa kung’ang’ania mipaka. Hivyo na wenyewe naomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nawashukuru hao kwa sababu inawezekana wananchi wa Mbarali wakashangaa imekuwaje leo nawashukuru! Kwa kweli katika kikao cha pamoja tulichofanya tarehe 28 na 29 na hao wote niliowataja, tulifikia hatua hiyo nzuri ya maridhiano. Tatizo kubwa lilikuwa ni ramani iliyoridhiwa na *RCC* ambayo haikuwa imeandaliwa awali na *TANAPA*, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ile ramani ya mwanzo haikuwa na mgogoro kwa wananchi wa Mbarali, sasa ilipoongezwa hii ya *RCC* ambayo ililetwa kinyume na taratibu, ilileta mgogoro mkubwa, wananchi wa Mbarali wakakosa imani na Serikali yao lakini baada ya kukaa tumekubaliana kwamba, ramani ya mwanzo ndiyo itakayofuatwa na siyo ile iliyoongezwa na *RCC*. Naishukuru sana Serikali kwa kuwa sikivu. Wananchi wa Mbarali wana imani kubwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi lakini vilevile na uongozi wa ngazi ya Taifa kwa maana ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa baada ya kuongea hayo, niongelee migogoro ya ardhi Wilayani Mbarali na maeneo mengine yaliyopo katika nchi hii. Migogoro ya ardhi katika nchi hii tusipoiangalia, itatupeleka pabaya! Ni kweli kwangu Mbarali kuna migogoro lakini vilevile kama

nafuatilia vizuri Rutoro Muleba kwa ndugu yangu Charles Mwijage na Misenyi kwa ndugu yangu Assumpter Mshama, ni hivyohivyo kuna migogoro hiyo ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafikia mahali nchi hii tunawapa wawekezaji maeneo ambayo baadaye wananchi wanageuka kuwa watumwa kwenye nchi yao! Hayo maeneo niliyotaja hayo ni maeneo yaliyoko mpakani, matokeo yake *Ranchi* zile zimebinafsishwa kwa watu ambao siyo Watanzania na sasa uwezo wa kufuga mifugo wao hawana, kinachofanyika ni kukodishia watu kutoka Uganda, watu kutoka nje ya nchi. Hili liliniuma sana niliposikia, kwa kweli sasa kama tumefikia hapo Watanzania tumefikia pabaya. Tuna wafugaji wetu nchi hii, hivi haya maeneo ya *NARCO* kwa nini tusiwape wafugaji wetu wanaohangaika? Tunafika mahali tunaanza kukodisha maeneo ya *NARCO* yaliyopimwa! Kwa nini Serikali isipime maeneo mengi ya namna hiyo? Kama kuna masharti basi wapewe wafugaji kuliko kubinafsisha kwa watu wengine. Tatizo hili ninalo Mbarali na nadhani na wenzangu mtakuwa na maeneo yenye matatizo kama niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *NARCO* Mbarali, ndugu zangu wananchi wa Kata ya Ruiwa na Mwatenga wamenituma Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na naomba Serikali isikie, pamoja na wananchi waliohamishwa Msangaji, watu hawa wamepelekwa mahali ambapo kuna ukame, hakuna malisho, hakuna nini, lile eneo la *NARCO* ambalo ni zuri kwa kufuga na kilimo ambalo sasa wanakodishwa wananchi, wale waliochukua, uwezo wa kufuga hawana, sasa wanawakodisha wananchi. Naomba Mheshimiwa Waziri baada ya kikao hiki, ili uone mimi ni mwongo, ukashuhudie kule jinsi ambavyo ardhi ile watu wanakodishiwa. Watu wale walitoa ardhi ile kwa nia nzuri kwa Serikali kuwa inataka kuleta ufugaji wa kisasa, sasa Serikali imeshindwa, kwa nini isiwape wale wananchi ikawapa na masharti yaleyale ambayo wamepewa wawekezaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Serikali Ranchi zote za Taifa wapewe wananchi wetu wafugaji. Kama kuna masharti wamepewa wawekezaji, tuwape wafugaji wetu badala ya kuacha leo hii wanahangaika na hawana pa kwenda. Hili naomba Mheshimiwa Waziri, tukimaliza hapa aje Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka vilevile nikuambie migogoro ya ardhi iliyoko Mbarali, eneo la Igomelo pale Igawa njiani, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uzalendo wake na moyo wake wa busara. Eneo lile Serikali imewekeza pale, watu wanalima kiangazi na muda wote panalimwa pale. Wachina walijenga pale, lakini katika hali ambayo ni ya kushangaza sana mtu mmoja akafika akasema hii yote ni *Game Reserve*. Waziri Mkuu alipokuja pale wananchi wakamwambia, "Angalia Mheshimiwa Waziri Mkuu, eneo lote tumeambiwa sasa ni *Game Reserve".* Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwaambia kwamba "Hata kama mimi ningekuwa mwendawazimu nisingekubali". Eneo lile limebaki kwa kauli ya Waziri Mkuu. Naomba na kwenyewe Waziri afike akawatamkie ardhi yao ile, wanataka kuwa na uhakika kwamba inachukuliwa au wanabaki nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemualika aje nimpeleke *NARCO* akakae na wananchi wa Ruiwa na Mwatenga na wananchi waliohamishwa kutoka Msangaji ambao sasa wanahangaika hawana mahali pa kuishi, tabu tupu! Aje aone ninayoyasema kama ni ya uwongo au ya ukweli.

Mheshimiwa Waziri, siwezi kukulaumu sana, utendaji wako ninaufahamu kwa muda mfupi, Wizara hii wewe ni mpya lakini naomba tukuambie ili tukusaidie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unapojadili mjadala wako elekeza kwenye Kiti, kwa Mheshimiwa Mwenyekiti siyo unampa Mheshimiwa Waziri moja kwa moja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ardhi katika Wilaya ya Mbarali, nimeshukuru kuwa tayari limeshaonesha njia ya kulipatia ufumbuzi lakini nikianzia Madibira Kitongoji cha Mlonga, maeneo ya Kinyasuguni, maeneo ya Silyamboga ni maeneo ambayo ni muhimu sana kwa wakulima wadogowadogo, nikiacha lile shamba la awamu ya pili ambalo linatakiwa kuridhiwa tena ili kusudi wananchi wapate sehemu ya kilimo. Eneo hili wale wakulima ambao wameshindwa kupata nafasi kwenye yale mashamba yaliyoboreshwa ndiko wanakolima, lakini vilevile tukumbuke watu wale wanaongezeka na *TANAPA* ikiishachukua eneo huwezi ukaja

siku nyingine ukasema sasa tuusogeze mpaka, haiwezekani Sheria yake ni ngumu! Sasa wakati ni huu kwa Wizara husika kuona kuwa inalinda maeneo ya wananchi ili kusudi baadaye wasije kuwa watumwa ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikija Kata ya Igava. Kata hiyo vijiji vyote vya pale vilionekana vinakuwa ni hifadhi lakini namshukuru sana Waziri Mkuu baada ya kutangaza, wale wananchi wamehangaika, wamechanga fedha nyingi, kesi wamepeleka Mahakamani kujinasua lakini nafikiri imefikia pazuri sasa karibu lile jambo litaisha. Nashukuru sana Serikali kwa hilo. Kata ya Rujewa maeneo ya Nyelegeti, Kata ya Songwe Imalilo maeneo ya Mahongole, Mwanalala, Maningu, Mnazi nayo yalitaka kuchukuliwa hivihivi, wale wananchi wamehamishwa mara ya kwanza, wakahamishwa mara ya pili na sasa wangehamishwa ingekuwa mara ya tatu. Nchi hii ndugu zangu tunataka kufanya nini, hawa wananchi wetu tusipoangalia kuna siku watakuja kuwa watumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo ukienda Kata ya Luhanga. Kata ya Luhanga nitaomba Waziri anayehusika mara baada ya Bunge akija pamoja na eneo hilo nitampeleka. Kata ya Luhanga wamevamia wajanja, wamefika pale wameongea na Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji wamechukua eneo kwa kuwadanganya kuwa tutawajengea Ofisi, tutafanya nini na wananchi kuja kushtuka hekta zaidi ya 8,000 wamepewa wale wakubwa kutoka huko sehemu mbalimbali sitaki kuwataja. Wananchi wamenituma na wameniomba nije niseme hawataki ardhi yao ichukuliwe. Nimejitahidi sana kufuata ngazi mbalimbali kwamba watatue kabla mimi sijalileta huku wale wananchi bado wananipigia kelele kwamba Mheshimiwa Mbunge kama hili eneo hutalisemea Bungeni usirudi huku, sasa mnataka niende wapi? Kwa hiyo, ndugu zangu naomba wale wananchi wakasikilizwe wa Kata ya Luhanga wamechukuliwa ardhi yao na wajanja kwa kuwadanganya kwa kupitisha mihtasari kinyume na utaratibu. Naomba nalo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la shamba la mwekezaji la Kapunga. Mwekezaji yule alipewa hekta 5,500 ndio kisheria na zabuni yake ndivyo ilivyokuwa inatamka lakini baadaye wanapokabidhiwa lile shamba akakabidhiwa hekta 7,370. Sasa wale wananchi wakajikuta eneo la makazi yao ambalo ni hekta 1,070 amepewa mwekezaji. Eneo la *small holder* hekta 8,000 amepewa mwekezaji. Sasa wanasema hivi kumbe tumekuwa tunauzwa tuko hapahapa. Hili liko peupe tu hata hesabu mtu asiyeenda shule linaeleweka, kama alipewa hekta 5,500 ilikuwaje apate hekta 7,370? Nalo hili wananchi wale wamenituma kwamba kabla sijarudi wanataka kupata majibu sasa na majibu mimi sina naomba nielezwe leo ni hatua gani zinachukuliwa kuhakikisha lile eneo la wananchi linatenganishwa na mwekezaji ili kuondoa kero na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ina kazi kubwa. Eneo la mwekezaji pale baada ya lile shamba kuchukuliwa, Mheshimiwa Baba wa Taifa alikuwa na roho nzuri, kila walipowekeza Shamba la Taifa aliandaa miundombinu mbalimbali wananchi wasaidiwe, sasa hivi miundombinu hiyo haipo. Sasa wameniomba wananchi wa Chimara na Kapunga yenyewe, Mwashikamile, Yala, Kwambaa wanataka eneo la Mpunga ambalo lina zaidi ya hekta 4,000 waboreshewe ili waweze kulima baada ya kuchukuliwa shamba ambalo walikuwa wanalitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mwaishikamile vilevile wanaomba waboreshewe, wananchi wa Yala wanaomba waboreshewe miundombinu yao. Nasema haya kwa uchungu sana kwa sababu tusipoangalia nchi hii mwishoni tutapigana. Tutasema wananchi sio watii wa sheria kumbe sisi wenyewe tunawakosea. Kwa hiyo, naomba kwa dhati kabisa na Mheshimiwa Waziri samahani nakutaja nitakuomba ufike twende wote nikupeleke ukaone hali ninayoizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema hayo …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Najua hiyo ni kengele ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Basi Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ujumbe umefika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya bwana ujumbe umefika.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea nilisema atakayefuata ni Mheshimiwa Zarina, atafuatiwa na Mheshimiwa Rebecca Mngodo.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu halafu niwatakie Ramadhani Karim ndugu zangu wote waliofunga na nawatakia rehema na amani Watanzania wote*.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema siungi mkono hoja na nitawaomba Waheshimiwa Wabunge wanisaidie kutokuunga mkono hoja, kwa sababu gani? Kuna mradi mkubwa wa upanuzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi ambao unataka kuruka wakati wowote. Mradi wa dola milioni 76.5 takribani ni shilingi bilioni 115. Ninasema siungi mkono hoja kwa sababu sioni utashi kwa upande wa Wizara ya Ardhi kutaka mradi huu kweli uendelee, nitatoa sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya, *MUHAS* waliomba ardhi mwaka 2004 na wakapewa mwaka 2006 katika maeneo ya Kwembe na Mloganzila. Ardhi hii ilikuwa ni ardhi ambayo inamilikiwa huko nyuma na mpaka sasa hivi *title* ndio inavyosema ni ya KABIMITA na Tanganyika *Packers.* Wamepewa ardhi ile na Mheshimiwa Rais alikwenda kuomba mkopo Korea ya Kusini akapata fedha hizo dola milioni 76.5 kuja kujenga Chuo Kikuu hiki. Hiki Chuo Kikuu ambacho ndio tunatarajia kipanue nyanja zote za afya, kiweze kuwafunza wataalam wa afya, kiweze ku-*save* fedha za Serikali za kupeleka watu nje kwa sababu wengi watakuwa wanatibiwa hapa, lakini kumekuwa na *dillydally* isiyoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Rais alipokwenda Korea amepata mwekezaji, mikataba imesainiwa, mwekezaji amekuja, sio mwekezaji huyu anayetoa mkopo, tumekopa. Masharti ya ule mkopo unasema riba yake ni asilimia 0.01, ndogo sana. Muda wa kungojea miaka 15, malipo miaka 45, tunataka nini kingine? Ukiangalia bajeti ya Wizara ni shilingi bilioni 22 huyu anatupa mkopo wa shilingi bilioni 115. Sasa wataalam wako hapa tokea mwezi Juni hawajaweza ku-*access* kule kwenda kuchukua hata udongo. Wizara inalijua hilo, Wizara ya Elimu imeandika barua nyingi, *MUHAS* imeandika barua nyingi na naomba kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi ni Makamu Mwenyekiti wa *Council* ya *MUHAS*, kwa hiyo ninalijua vizuri sana suala hili. Mkataba umeshasainiwa na *consultant* ameshateuliwa. *Consultant* amekuja hapa akiamini kabisa kwamba anakuja kuanza kazi. Amekuja hapa hakuna kitu kinaendelea tokea mwezi Juni. Juni imemalizika, Julai imemalizika na Agosti kesho kutwa inakwisha hivi kweli sisi tunataka Chuo hicho kijengwe. Nasema hatuko *serious* kwa sababu kuna wakati Wizara ya Ardhi iliomba kwamba imege kipande cha ardhi ya pale Mloganzila ili wagawanye kwa watu wengine wakisema kwamba ni kubwa. Kama isingekuwa Mheshimiwa Rais kuingilia kati wangeshakata. Sasa kweli walikuwa wanataka huu mradi uendelee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekwenda watu wa ardhi wamefukuzwa lakini Serikali ilikwishatoa fidia ya shilingi bilioni nane tokea mwaka jana na shilingi bilioni nane hiyo ni watu 1,917. Wakatokeza watu wengine wakasema sisi bado, lakini malipo kesho, kesho kutwa watu 303 na leo wanatokea watu wengine wanasema hawajalipwa sasa wako 617. Nasema huu mradi ni wa maslahi ya wananchi wa Tanzania wote milioni 40, ndio tutategemea pale. Sasa hivi pale Mutumbili hao Wakorea wamejifinya wanajenga Chuo pamoja na hospitali kubwa, hivi nani ambaye haitamfaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Diwani wa Kwembe, nikawauliza, kwa nini mnakataa hawa *consultant* hata wasije kuchukua udongo? Wakasema ndio tumekataa kwa sababu tuliambiwa tutalipwa fidia na sasa hivi hatujui Wizara ya Ardhi inasema nini. Mpaka leo

Wizara ya Ardhi haijatoa tamko kuwaambia wale watu. Hivi kweli kama Serikali inataka itashindwa kuwasindikiza hata na Polisi wale watu waliokuja, huyu *consultant* akaenda kuchukua udongo, watashindwa kuwasindikiza hawa watu wa Wizara ya Ardhi kwenda kufanya *survey* au ndio kwamba huo mradi hautakiwi ili kusudi viwanja vibaki tupate kugawana? Mambo ya *Air Tanzania* na *KLM* ilikuwa hivihivi. *KLM* walianza kuja Tanzania lakini ikawa pa kunawa, pa kuoga, pa kunawa pa kuoga mwisho wamekwenda Kenya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkataba wa mradi huu unasema hivi, gharama yoyote itakayoongezeka kwa sababu ya kutokutekelezwa italipwa na Serikali ya Tanzania, hiyo moja. Pili, migogoro ya ardhi ikitokea watahamisha mradi huu na kuupeleka kwingine. Leo tokea tarehe 28 Juni wako hapa mpaka hivi ninavyozungumza hakuna kinachoeleweka, hivi hawaondoki hawa? Sasa wakiondoka hawa sisi tumepata nini jamani? Ni kweli Serikali inashindwa kwenda kuwasimamia wakachukua udongo tena baada ya kulipwa shilingi bilioni nane? Mimi sielewi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo siungi mkono hoja hii mpaka niambiwe ni jinsi gani wale watu watakwenda kuchukua udongo, ni jinsi gani Ardhi watakwenda kupima halafu waondoke waende wakatutengenezee mambo tuje kujenga. Kama hawa watu wengine wanadai shilingi bilioni mbili hivi kweli tuukose mradi wa shilingi bilioni 115 Rais aliokwenda kuutafuta huko Ughaibuni kwa ajili ya shilingi bilioni mbili? Haieleweki! Hilo naliomba la kwanza, Mloganzila wanasubiri, Diwani ananiambia hata tamko tu la Wizara, anasema Wizara wanashindwa kuja kwetu kutuambia jamani tatizo ni hili, moja, mbili na tatu. Sisi *MUHAS* wamekwenda kule wameongea nao wakatuambia sisi hatuwajui ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam Mji mkubwa, kuna migogoro mingi sana ya ardhi. Migogoro hii inaletwa na Wizara ya Ardhi na Wizara ya Ardhi namhurumia sana Mama Tibaijuka, kwa sababu mingine ameikuta, lakini pale pana Watendaji wabovu sana. Sio kwamba wanafanya labda kwa bahati mbaya hapana, makusudi kabisa. Kiwanja kinaweza kikatolewa kwa watu wawili au watatu na ukienda jina lako leo linaweza likawepo kesho ukienda halipo. Kubadilisha majina kwenye kompyuta shilingi million sita, inatokea hiyo. Akitaka nitamwambia na majina yao watu wanaofanya hivyo. Mimi niko tayari kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwa sababu vinatia aibu na vinatia uchungu lakini siku hizi jamani si kuna hawa *computer forensic,* kwa nini usiwaite *computer forensic,* nenda ukachambue zile kompyuta majitu utakayokuta kule utazimia. Ni mambo ya ajabu, ni mambo ya aibu na wana-*chain* kabisa Wilaya ya Kinondoni ndio wakubwa wa hao. Hata Mheshimiwa Lukuvi Kamati yake ilipowasimamisha wengine sasa hivi wanatafuta njia za kurudi kwa milango ya nyuma, tunajua kwa sababu ndio *chain* yao. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri ushughulikie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanja vingine ambavyo wananchi wamegawiwa, vimetoka Ardhi anakwenda kule kwenye kiwanja anafurushwa, aliyemkuta anasema mimi sijalipwa huwezi kuingia hapa na bahati mbaya sana wengine ni akinamama. Wakirudi Wizarani wanaambiwa wao hawana taarifa na Temeke wanasema hawana taarifa. Mheshimiwa Waziri naomba ulichukue hilo kwa sababu akinamama wamekuja kunililia hawajui mahali pa kwenda, Wizarani wamefukuzwa, Wilayani wamefukuzwa ofa zao wanazo mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie, kuna viwanja vinaitwa vya miradi, viwanja hivi vya miradi ni viwanja gani na ndio hivyo vinavyotumika kula. Mimi nakuomba uangalie hivyo viwanja vya miradi na utavikuta viko katika *lucrative arrears* lakini uvamizi wa viwanja umekithitri na unaondoa amani Dar es Salaam. Hilo lazima mliangalie jamani, naona watu wapo tu hakuna mtu analiangalia, jamani na wavamizi wanakwenda kila siku. Kuna mtu ambaye kila siku anavamia na anakwenda kubomolea watu nyumba, wanafukuzwa hakuna kinachosemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kengele yangu ya pili haijalia, naomba nizungumzie kuhusu hii Sheria ya Ardhi. Tunaomba Sheria ya Ardhi iangaliwe upya ina upungufu mwingi sana. Hilo silisemei sana maana kuna watu tayari wamelisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigamboni, hivi tunavyosema tuna-*develop* mahali halafu ukienda kumfukuza yule mwenyewe hapati hata kitu hivi inakuwa safi kweli? Mbona nchi za wenzetu wengine mtu anapokuja kuwekeza na wewe ndio wanapopata, lakini sisi mtu akija kuwekeza wewe ndio unakuwa maskini, sasa hali hii itakwenda mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, hivi viwanja vinavyopimwa ambavyo vinauzwa shilingi milioni sita au nane, kiwanja ambayo ni mita 20 kwa 30, hivi mwanamke wa kawaida anaweza kulipia? Hivi kuna kijana anaweza kulipia? Kuna mfanyakazi anaweza kulipia? Hivi hili tunalionaje na unapewa siku saba kwamba uwe umelipia, mwaka mmoja umejenga, inawezekana kweli? Hivyo viwanja ni vya matajiri? Sasa umekwenda kuchukua ardhi ya yule mtu maskini ndio umeigawa hiyo halafu na yeye unamgawia kiwanja halafu unamwambia alipie lakini fidia umempa kiduchu akienda kulipia kile kiwanja amekwisha, anajenga na nini, mtaji wote umechukua wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ni mengi sana na inahitaji kufumuliwa kabisa. Mimi namjua Mheshimiwa Katibu Mkuu amekuwa katika Wizara zingine na alikuwa anasifika, tuliposikia anakwenda Ardhi tukajua anakwenda kumaliza matatizo lakini wanamzunguka, wajanja wengi. Wizara inahitaji kufumuliwa, wajanja wanajulikana vizuri sana. Ukienda kuona mahekalu yao huwezi kuamini kwamba huyu eti anapata mshahara wa shilingi 300,000/=. Unapata mshahara wa shilingi 300,000/= unajenga nyumba ya shilingi milioni 600 zingine umezipata wapi wala huna mkopo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kengele inililie, naomba nisiunge mkono hoja mpaka suala la Mloganzila lieleweke. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zarina, kwa kweli mchango wako ni mahiri kabisa na leo umetupa msemo mpya pa kunawa pa kuoga. Kwa hiyo, tunakushukuru kwa mchango wako. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, naona Mheshimiwa Rebecca Mngodo hayupo basi naomba nimwite Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa ya kusema kidogo katika Wizara hii ambayo ni Wizara muhimu sana katika nchi yetu. Labda nianze kusema, nashangaa kidogo ninapoona kuna Wizara moja ya Serikali inapewa fedha *pending* bilioni 350 lakini Wizara nyeti kama hii unaipa shilingi bilioni 47, nashindwa kuelewa au tuambiwe hapa kuwa hizi fedha zimetolewa zimsaidie Mheshimiwa Waziri wa Ardhi akapime ardhi katika Jimbo lake lakini kama ni kwa ajili ya nchi nzima, hiki ni kichekesho kikubwa, haiwezekani. Niliamua nianze na hilo na hapa ndipo itakapokuja lawama hapo baadaye, umeacha fedha ya kununua ugali na kauzu unarudi nyumbani unasema pilau, *juice* na mambo mengine, utakuwa ni baba wa ajabu sana. Sasa Serikali kama itafikia pahali ikasema Wizara ya Ardhi haikufanya kazi yake, nafikiri itahitaji kulaumiwa yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Wizara. Ameshasema mtangulizi wangu hapa Wizara ya Ardhi kuna mambo mengi ya kusikitisha na nianze na migogoro inayojitokeza. Kuna maeneo watu wanavunjiwa nyumba zao na hapa Dodoma yapo maeneo hayo. Kuna maeneo yanaitwa Mji Mpya, miaka mitatu iliyopita watu wamevunjiwa nyumba 150 na mpaka leo hawajalipwa. Kinachosikitisha watu hawa wakati wanapiga matofali wanatafuta vitu mbalimbali wanaonekana lakini Serikali imenyamaza kimya, mpaka mtu anajenga nyumba ndio unakwenda kumvunjia Mtanzania mnyonge. Sasa huu kweli ni ubinadamu, huu ni uungwana au hiki ni kitu gani? Serikali ambayo unategemea ikulinde na ikusaidie katika matatizo yako, inakutafutia namna ya kuku-*fix* ili ikufilisi, ili ikumalize, ili ikurudishe nyuma. Mimi nafikiri huo si mwenendo mzuri na si ustarabu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mwingine wa hapahapa Dodoma pale Mzakwe, wamevunjiwa watu nyumba zao kwa kisingizio kuwa pana mashine ya maji, mimi nakubali, unahamisha watu lakini kwa nini unawahamisha wengine, wengine unawaacha? Wafanyakazi wapo, kama ni vyoo, kwenye nyumba zao kuna vyoo, kama wanaweza kuharibu maji na wale

wanaweza kuharibu. Kwa nini tunakuwa na *double standard*? Kama tunaamua kuwahamisha watu, tuwahamishe wote awe mfanyakazi au raia wa kawaida lakini mwenendo huu wa kuwahukumu wengine, wengine ukawaacha si mwenendo mzuri hata kidogo na ndiyo hapa wananchi wanapoona Serikali inawaonea. Kumbe Serikali imefanya kazi yake lakini imefanya kazi vibaya kwa sababu inafanya kazi kama ina aina fulani ya ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nafikiri wakati umefika wa Serikali kujitathimini. Wanapoona watu wamechukua ardhi au ardhi hiyo haitakiwi itumike wanavyotaka, Serikali basi katika hatua ya mwanzo wawaelekeze na ndiyo hapahapa linakuja suala kuwa wananchi wamepewa maeneo halafu wanaambiwa wamevamia maeneo. Mwananchi atavamiaje eneo na Serikali inaona? Eneo lako binafsi la nyumba, aje mtu ajenge, umwachie mpaka anapiga matofali, anajenga msingi, asimamishe nyumba, wewe unamwachia tu? Halafu akishamaliza nyumba wewe ndiyo uje uvunje, umwambie ulikuja kuvamia. Hutakubali hivyo. Sasa kama mtu binafsi hukubali na Serikali inakubali, mimi nafikiri kuna tatizo. Kuna tatizo la uwajibikaji na lazima katika hili Serikali ione kuwa kuna umuhimu wa kusimama katika kuwasaidia wananchi badala ya kuwadhalilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala ambalo Wabunge wengi wanalisema. Katika Bunge hilihili, katika nyumba hiihii, katika Bunge lililopita yamewahi kuulizwa maswali kuhusu suala la Kigamboni. Serikali imekuwa na majibu mengi sana. Mara hahamishwi mtu, mara havunjiwi mtu, mara zitavunjwa, mara kuna mwekezaji. Hivi Serikali hii kwa kupitia Wizara ya Ardhi inasemaje kuhusu Kigamboni? Kigamboni wanyonge wamenunua viwanja na wamejenga nyumba zao mnataka kuwatia umaskini kwa kuwavunjia kwa kisingizio cha uwekezaji na kama lengo ni hilo kwa nini hamuwaambii mapema, mkawapa fidia mapema wakajua pa kwenda? Mnasubiri mpaka kiwanja Dar es Salaam kiwe shilingi milioni 100 ili mwende mkawalipe shilingi milioni tatu warudi kwenye Mikoa yao waliyotoka, ndivyo mlivyokusudia? Ndiyo maana yake hiyo kwa sababu ardhi kila leo inaongezeka thamani. Sasa nyie mnasubiri, hawa watu ambao wana nyumba zao mkizivunja hamtaweza kuwalipa wakaweza tena kupata nyumba. Si vibaya kama mnataka kutumia kwa sababu Serikali ndiyo yenye kila kitu, ndiyo yenye ardhi, ndiyo yenye mamlaka, ndiyo yenye dola, mna haki ya kutumia vyombo vyenu hivyo, lakini msivitumie vibaya mpaka mkawaonea watu. Hali hii inasikitisha na mimi naomba Mheshimiwa Waziri atakapotoa majumuisho hapa atoe kauli ya Serikali kuhusu Kigamboni na kila mtu ajue mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo niende kwenye nyumba, *National Housing*. Kimsingi ilianzishwa ili kuwasaidia wanyonge ambao hawakuwa na uwezo wa kujenga nyumba zenye maana, wakaweza kukaa. Kwa muda mrefu mimi niseme naishukuru sana sera nzuri hii ya TANU ambayo imerithiwa na CCM lakini mwelekeo unaonyesha kuwa sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inataka kuondoka hapo ilipo na kwenda kwingine. Mwenendo wa namna Shirika la Nyumba linavyofanya, inasikitisha sana. Leo wataamka na kauli hii na kesho wataamka na kauli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilishawahi kusema Bungeni hapa kwamba hapa Dodoma kuna nyumba walisema wanapandisha malipo ya nyumba kutoka shilingi laki moja mpaka shilingi laki nne na isingekuwa kusema hapa Bungeni na Serikali ikasikia basi leo wanyonge wangelipishwa shilingi laki nne badala ya shilingi laki moja. Maana yake ni kwamba wale wasingekuwa na uwezo wangetoka kwenye nyumba wakaingia hawa waliokusudiwa waje wakae, yaani watu wenye uwezo. Sasa tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Unaondoka kwenye mwelekeo wa msingi, unafuata hela mbili, tatu na mimi nina wasiwasi kuwa wanaoongoza Shirika hili wao wenyewe wana uwezo. Sasa wanahamisha uwezo ule walionao wao wanaupeleka kwa wanyonge, wanyonge hawana uwezo hata kidogo. Usichukulie kuwa wewe una nyumba yako ya shilingi milioni 500, wewe una uwezo wa kupata pesa unazopata ukadhani na mnyonge anayetoa shilingi laki moja katika mshahara wake wa shilingi laki mbili akakodi nyumba, ukampandishia shilingi laki nne au laki tano ukategemea ataweza, haiwezekani! Matokeo yake watakuja wale wenye uwezo na ndiyo hapo mtakapoona joto ya jiwe kwa sababu wanyonge wakifikia mahali wakiona Serikali inawaonea patakuwa hapatoshi hapa. Msidhani mamlaka ya dola au nguvu za dola zinaweza kunyamazisha. Kwa wenzetu hizo balaa zinazotokea nguvu za dola zipo, Polisi

wapo, Majeshi yapo, bunduki zipo lakini watu wamezikimbia bunduki, wakakimbia Ikulu wakaondoka. Tafadhalini kaeni na watu vizuri, jaribuni kuwaridhisha watu na waone kuwa mnawahurumia. Msiwafikishe watu mahali wakalalamika sana mpaka ikapita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi. Sheria ya Ardhi ina matatizo. Ni nchi chache sana duniani leo ambazo anakwenda mtu mgeni kwa kisingizio cha uwekezaji akapewa ardhi anayokata, akafanya anavyotaka kama wanavyofanya hapa Tanzania. Lazima Sheria ibadilishwe ili mwekezaji aweze kuwekeza au awe *partnership* na Mtanzania na hiyo ndiyo namna ya kuwawezesha watu wetu. Kama tunataka kuwawezesha, tufanye hivyo. Si geni hili, leo huwezi kwenda nchi za Uarabuni pamoja na utajiri wao ukaweza hata siku moja kufanya biashara yoyote kama huna ubia na mzalendo wa pale. Maana yake ni nini? Hutaweza kuhamisha mali kiujanjaujanja ukifika mahali umeshindwa unaambiwa ondoka, biashara na mali inabaki ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa imekuwa ile lugha waliyosema, yupo mtu mmoja mashuhuru sana ndani ya nchi alifananisha timu yetu ya Taifa na Kichwa cha Mwendawazimu kila mtu anayekuja ananyoa anavyotaka. Haiwezekani, ardhi ni kitu muhimu sana, ndiyo rasilimali ya Watanzania halafu tunaiachia hivihivi tu, watu wanakuja wanapewa wanavyotaka, wanafanya wanavyotaka ilhali wanyonge hawana wanachoambulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali, hebu tufikie mahali suala hili la migogoro baina ya wafugaji na wakulima limalizwe. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliulizwa humu ikaundwa Tume. Maswali yanayokuja, yanaulizia masuala haya na kila leo linaendelea. Tutafika wapi? Hivi ni suluhisho unaondoa wafugaji katika eneo fulani unawapeleka kwenye eneo ambalo watu wa eneo hilo hukuwauliza kwa sababu tu ni raia wako? Haiwezekani! Kama wewe unaona wafugaji ni kero upande wako basi na wale ambao walikuwa hawajazoea kuwaona wafugaji vilevile wanaona ni kero. Kuna rafiki yangu Mbunge mmoja wa Mikoa ya Kusini aliwahi kusema hapa kwamba wao wakiona ng'ombe wanashtuka sana kwa sababu hawakuzoea kuwaona ng'ombe. Sasa kama mtu hakuwahi kuona ng'ombe, akiona ng'ombe mmoja anaogopa, unampelekeaje ng'ombe 3,000? Baya si hilo, watu wanagombana. Hivi kweli Serikali iko tayari ione watu wanauana kwa sababu hii ya kugombania ardhi? Kwa nini hampimi, mkasema eneo hili la wafugaji, eneo hili la wakulima, eneo hili la watu fulani, kila mtu akajua eneo lake. Yule anayevuka mipaka yake ni rahisi kumhukumu kwa sababu umeshamwekea mipaka yake lakini mnaacha hali mpaka iwe mbaya ndiyo mnapeleka Polisi wakapige watu, mnapeleka Majeshi wapige watu bure tu kumbe mngeweza kuondoa tatizo hilo kwa kutumia maarifa, kwa kutumia busara. Nguvu hazijengi kila wakati. Mara nyingi unapoamua kufanya kitu kwa kutumia nguvu unaharibu, fanya kitu kwa kutumia akili, akili itakuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kuhusu Wizara yetu hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya njema na kuwepo katika Ukumbi huu wa Bunge jioni hii. Vilevile niwapongeze ndugu zangu Waislam kwa mfungo mzuri wa mwezi wa Ramadhan. Nawatakia kila la kheri lakini na ninyi ndugu zetu tuwe pamoja na tushirikiane maana mfungo huu ndiyo ni kwa Waislam lakini vilevile na nyie mko ndani yake. Kwa hiyo, kwa pamoja nasema Mungu atujalie kila la kheri tuendelee kumaliza shughuli hii ya kufunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusukuma maendeleo ya wananchi kupitia Wizara yao. Niwapongeze sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri yeye ni mgeni katika Wizara lakini kwa jinsi alivyokuja na kuelewa na kuisoma na jinsi alivyowasilisha hotuba yake, nina uhakika ataendelea kuisimamia vizuri. Nakutakia kila la kheri Mama Tibaijuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nianze na suala la migogoro ya ardhi. Hili ni tatizo kubwa maana kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama anazungumzia hilo na migogoro mingine imekuwa ya muda mirefu sana, mingine ina zaidi hata ya miaka mitano, miaka sita mingine mpaka miaka kumi bado haijatafutiwa ufumbuzi. Mimi niiombe Wizara kwa kushirikiana na Mabaraza ya Ardhi pengine ianzishe Dawati la kushughulikia migogoro ya ardhi peke yake. Kwa sababu migogoro hii inafanya watu wavunje amani, watu washindwe kusaidiana na kushirikiana kwa sababu ardhi kila mmoja anaithamini na bila ya kufanya hivyo mimi nina uhakika pengine watu wanaweza wakafarakana. Kwa hiyo, kwa hilo niiombe sana Wizara kwa mfano nichukulie mgogoro wa mpaka wa Kiteto na Kondoa, mipaka kati ya wananchi na hifadhi, mipaka kati ya vijiji na vijiji, naomba Wizara ijikite katika suala la kutatua migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hilo niendelee na suala la matumizi bora ya ardhi. Ili migogoro hii iishe na kama si kwisha kabisa naamini na hata Serikali inajua hilo na ndiyo inalifanyia kazi kwamba bila ya kupima ardhi ikapangwa katika matumizi yake, nina uhakika migogoro hii haitaisha. Ni vizuri katika nchi hii, katika vijiji, katika vitongoji kila mmoja ajue eneo lake ni lipi na ndipo atakapoona umuhimu wa kutunza ardhi kwa kupanda miti na kulima kwa kutumia kilimo cha kisasa na masuala mengine ambayo yanahitaji matumizi bora ya ardhi. Bila ya kufanya hivyo kwa kweli migogoro itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nitake kujua tu kwamba kuna maeneo kwa mfano Ranchi zetu mbalimbali na sisi Dodoma tunayo Ranchi ya Kongwa. Bunge lililopita tulikubaliana pengine ardhi ile au Ranchi ile ibaki kwa ajili ya wananchi wanaizunguka. Sasa kilichotokea ni kitu gani mpaka ikabadilika na kwa kweli mpaka sasa hivi hatuelewi tunafanya nini nayo maana tayari inawezekana imepata wawekezaji au imepata watu wengine. Sasa tunaomba Serikali pengine ione kwamba umuhimu wa Ranchi hizi ziwe kwa faida ya wananchi wanaozizunguka isije wakatoka watu maeneo mengine wanapewa, wananchi wanaoizunguka hawana ardhi ile tena. Hili naomba Serikali ilishughulikie kikamilifu na ione kwamba wanaoizunguka Ranchi vilevile ni watu wanaohitaji ardhi na wanaweza kuitumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la fidia. Serikali inapopima ardhi au viwanja, maeneo mengi wanakuta kuna wananchi ambao tayari walishajenga nyumba zao pale na bahati nzuri wengine hupewa viwanja na wengine hawapati. Kinachotokea ambacho mimi binafsi kinanisikitisha sana ni kwamba baada ya wananchi hao kupewa viwanja wakati mwingine unakuta wengine hawana uwezo kabisa, sasa uwezekano wa kusema na yeye ajenge nyumba inayolingana na ya mwenzake mwenye hela anakuwa hana. Sasa unakuta wananchi wetu wanaanza kuuza kwa maana kwamba pengine aende mahali pengine. Sasa unakuta mwananchi kama huyu anakuwa ni mhamajihamaji. Anamkimbia mwenye hela yeye anakwenda kuchanganyika na wasio na hela wenzake. Sasa tunawafanya wananchi wetu waishi maisha ambayo ni ya kuhangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kauli na mipango aliyonayo sasa kwamba mtu hatahamishwa, ni lazima apatiwe eneo na vilevile asaidiwe hata kujenga. Kwa hiyo, nimshukuru sana na naishukuru sana Serikali kwa suala hilo. Sasa sijui suala hili litatolewa kwa maandishi kwenda kwenye Halmashauri na Manispaa waelekezwe kwamba sasa ifike wakati watu wasinyang'anywe viwanja kwa sababu wameshindwa kujenga, kwa sababu tunao wananchi wengi wa aina hiyo katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Dodoma na maeneo yote ya miji na vijiji. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwamba watu kama hawa wanaoshindwa kujenga basi wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami vilevile nizungumzie suala la Kigamboni kwa sababu Jiji la Dar es Salaam, ni mji wa wananchi wote wa Tanzania na kila mmoja anapokwenda pale anauangalia na wengi wanatamani wanapofika pale watafute viwanja wajenge. Suala la Kigamboni limekuwepo sasa karibu miaka mitatu na kila bajeti inapozungumzwa ni kwamba wawekezaji wanatafutwa, wakipatikana wanajenga mji ambao kwa kweli wote tumefurahia kama utajengwa utakuwa mji mzuri lakini sasa kuna wengine walishanunua viwanja, kuna wengine walishaanza kujenga, kuna wengine wamekamilisha kujenga na kuna wengine wamebaki hawajajenga kwa kutii Waraka wa Serikali kwamba msijenge, acheni Mji unatayarishwa kwa kujenga Mji mzuri zaidi. Sasa Serikali tuiombe sana katika hili kwa kweli itoe tamko kuwaarifu

wananchi kwamba utaratibu tuliojiwekea wenyewe unakamilika lini? Kwa sababu wameshasubiri mpaka wamechoka. Sasa wengine wanaweza wakaamua hata wakajenga na mkaona kwamba si watiifu lakini kumbe ni kule kusubiri watu wameshachoka. Wameshachoka kusubiri kwa hiyo wanaamua kuvunja Sheria. Niiombe Serikali iwaambie wananchi kwamba suala la Kigamboni mwisho wake ni lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *National Housing*. Kwa wale ambao waliiona *National Housing* toka mwanzo inaanza na mpaka ikaendelea ikajenga nyumba katika Mikoa mingi mpaka sasa ilivyo, niwaombe sana na pengine nimwombe Mheshimiwa Waziri mhusika, labda ifike siku moja Wabunge waandaliwe semina ili waelezwe jinsi *National Housing* sasa hivi inavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Housing* iliyopo sasa, siyo ile ya siku zilizopita, ambayo ilikuwa hoi bin taaban. Ilishafika mahali haikuwa inaweza hata kukarabati nyumba. Lakini kwa sasa hivi *National Housing* iliyopo ni tofauti kabisa. Imekwishakarabati nyumba nyingi, imekwishajenga nyumba nyingi na kwa kweli inafanya kazi ambayo ni ya uhakika. Kwa mipango waliyonayo kwa sisi wa Dodoma, kwa kweli tunashukuru Mungu. Tunashukuru sana kwa sababu zitajengwa nyumba 260 na nyumba 160 zitakuwa za kukodisha na nyumba 100 zitakuwa za kuuzia wananchi. Kwa kitendo hicho, nasema tunawashukuru sana vijana wetu wa *National Housing* na hasa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili, kijana wetu Msechu amejitahidi kufanya kazi akishirikiana na wenzake na Wizara pamoja na Bodi inayohusika. Kwa hiyo, waendelee kuchapa kazi na wala wasirudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Dodoma tutakuwa tayari kununua hizo nyumba zitakazouzwa. Ila ninachokiomba, bahati nzuri jana walifanya uzinduzi wa ujenzi wa nyumba hizo na bahati nzuri maghorofa mawili tayari yamekwishajengwa. Sasa ninachowaomba au ninachoiomba Serikali, ambapo na Mheshimiwa Waziri alikisema mbele ya Waziri Mkuu kwamba, kuna gharama ambazo zinasababisha kupandisha bei ya nyumba, ni zile gharama za kupeleka maji na umeme. Niiombe sana Serikali na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu alikubali kukaa na watu wa maji na watu wa umeme. Sasa niombe basi, watakapokuwa tayari, basi ili kupunguza bei ya nyumba ambazo wananchi watauziwa, gharama hizo zigharamiwe na Serikali. Hata kama hizi zinazojengwa Dodoma ambazo tayari *National Housing* wamekwishapeleka umeme, watapeleka maji, basi hizo gharama zilipwe na Serikali ili nyumba zitakapokuwa tayari, zitakapouzwa, ile gharama ya umeme na maji iwe imekwishaondolewa pale ili bei kwa mnunuzi iwe rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niishukuru sana Serikali na nimshukuru sana sana Mheshimiwa Waziri kwa suala zima hili la kusimamia *National Housing* vizuri na mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ardhi. Kwa hiyo tutashirikiana, tutasaidiana kuona kwamba nyumba nyingi zinajengwa kama walivyoahidi na kwa kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, tutashirikiana na tutasaidiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mwisho ambalo ni kuhusu raia wa nchi za nje wanapoingia nchini kutafuta ardhi. Kuna maeneo ambayo wanapita na bahati nzuri wanajifunza nchi hii uendeshaji wake ukoje. Sisi Dodoma kuna hawa watu waliokuja kuchukua ardhi wakasingizia kwamba wanapanda Jatrofa. Kwa hiyo, wamechukua ardhi kubwa na Jatrofa hawapandi na mpaka sasa ardhi imekaa haina....

*(Hapa kengele Ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mfaki, kengele ya pili!

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana na naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ujumbe wa Jatrofa umefika.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kipekee kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Lakini pia, niungane na wenzangu ambao wamekwishatangulia kuchangia kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, watendaji wa Serikali pamoja na Serikali kwa kuleta hoja hii ambayo imenipa fursa kuchangia mambo mbalimbali hasa yanayohusu Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu hizo, nianze kwa kusema kwamba sitaunga mkono hoja hii. Kwanza, naomba nianze kwa kuzungumzia matatizo ambayo yanahusu suala zima la kutathmini, suala la malipo ya fidia na suala la mahali wanapopelekwa watu hao ambao wanalipwa fidia na kuhamishwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutathmini limekuwa linaleta mgogoro mkubwa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza, ni maeneo ambayo yanatathminiwa kutokupewa haki kufuatana na jinsi ambavyo Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inavyosema kwamba, wanapotathmini wanatakiwa watathmini kwa hali halisi ya soko jinsi ilivyo *(market value)*. Wananchi wamekuwa wakilalamika mara nyingi kwa sababu ya kupewa fedha kidogo kulinganisha na mali zao walizonazo katika eneo husika, lakini pia hata mazao waliyonayo mahali hapo wanapohamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika eneo la pili ni wananchi ambao wanafanyiwa tathmini na wanaachwa mahali pale kwa kipindi kirefu. Nitoe mfano halisi, wapo wananchi wanaoishi Kipunguni A. Wananchi wale walifanyiwa tathmini kuanzia mwaka 1977. Ni miaka takriban 34 sasa, ni miezi takribani 420 na kitu. Mpaka sasa wananchi wale wanaishi sehemu ile kama vile wafungwa, hawaruhusiwi kujenga, kuendeleza sehemu zile, hawaruhusiwi kwenda kuomba kibali cha ardhi ambacho kingewasaidia sana kwa ajili ya kutumika ili kukopea na kuendeleza maisha yao. Mpaka sasa miaka hiyo 34 wako kama vile wako kifungoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 34 ni mingi. Hata kama ni mtoto ni kwamba, amezaliwa na amezaa na akizaa kama mtoto wake ni mtundu, ana wajukuu tayari. Ni kipindi kirefu sana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kupitia wewe Mwenyekiti, aliangalie upya suala hili la kutathmini ili wananchi waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo, liko suala zima la kulipwa fidia ambalo wananchi wengi wamelipwa kiwango kidogo na wameshindwa kulipwa kufuatana na Sheria ile kiasi kwamba kama wakija sasa Serikali kuja kulipa, wanalipa kwa *value* ya wakati ule ya mwaka 1977 walipotathmini, wakati ambapo Sheria ya Ardhi inasema kwamba wanatakiwa waende wakatathmini na baada ya miezi sita wanatakiwa wawalipe wananchi hawa. Vinginevyo, wanatakiwa walipe asilimia sita kwa kila mwezi ambao unapita. Kwa hiyo, naomba sana kama zoezi hilo litafanyika, basi wananchi wale walipwe asilimia sita ya *market value* ya pale walipo kwa miezi hiyo 428.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la sehemu wanakopelekwa wananchi hao. Ni kawaida kabisa kwamba Serikali inahitaji maeneo ya wananchi walioko karibu na mjini kwa ajili ya maendeleo. Lakini cha kushangaza, hawaandai miundombinu mizuri ili wananchi wale wakaishi mahali ambapo angalau panafanana na mahali pale walipotoka. Kwa mfano, wapo wananchi ambao walihamishwa kutoka Kipawa, wengine Kigilagila, wananchi wale walikwenda kutupwa katika sehemu ya Pugu Kinyerezi. Kule hakuna maji, hakuna barabara, hakuna shule, hakuna afya na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kwamba niliwahi kutembelea shule moja ya Kimwani kule, shule ile ilikuwa na wanafunzi 900 lakini ina madawati 60 tu. Ni kwa sababu ya ongezeko la ghafla la wananchi waliohamia sehemu ile ambao walihama na watoto wao, kwa hiyo wakaenda kujijaza kwenye ile shule. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikaanza kutengeneza mazingira ya miundombinu kabla haijawahamishia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sasa katika suala zima la migogoro ya mipaka. Katika Wilaya ya Ilala tunayo mipaka ambayo imetuletea matatizo makubwa, lakini cha kushangaza ni kwamba Wizara ya Ardhi imekaa kimya. Upo mgogoro ambao ni wa miaka mingi sana ambao

unatokea katika Kata ya Chanika, kati ya Wilaya ya Ilala na Kisarawe kwa kutumika ule Msitu wa Kazimzumbwi. Huo mgogoro ni wa muda mrefu sana. Lakini tu mwaka huu mapema, wananchi walikwenda kubomolewa tena nyumba zao, mifugo yao ilichukuliwa na mpaka sasa Wizara ya Ardhi imekaa kimya. Naomba sana waende wakaangalie na kutuonyesha kwamba mipaka ya Kazimzumbwi iko wapi ili wananchi waweze kuendelea kuishi maisha ya amani na furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hapo tu, iko migogoro mingi katika Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Kinondoni, sehemu ya Kinyerezi. Mpaka sasa kuna ugomvi na kesi ziko Mahakamani kwa sababu ya kutokueleweka vizuri mipaka ya namna hiyo. Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hapo tu, hata Kitunda kule. Kitunda tuna mgogoro na Temeke kwa kupitia sehemu moja inayoitwa Kipera. Napo pale wananchi hawaelewi kama wako kwenye Wilaya ya Ilala au wako kwenye Wilaya ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanishangaza kwamba, hivi hawa Maafisa Ardhi, wanakaa ofisini huko kuna viwanja au kuna nini? Hebu watoke ofisini wakasuluhishe migogoro hii ya wananchi. Nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri, najua kwamba ana *experience* kubwa ya Kimataifa, lakini naomba sana ajikite zaidi kushuka chini na kuhakikisha kwamba anashughulikia migogoro ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee sasa kuzungumzia uharibifu mkubwa wa ardhi wa watu wanaohusika na kuchimba mchanga katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Ukonga. Kwanza kabisa, nimwombe Waziri atoe tamko rasmi kuhusu watu hawa. Iko kampuni moja ya Mbezi *Tiles* ambayo inachimba mchanga kwa kipindi kirefu sana katika eneo la Majohe, wamechimba mpaka wamefika kwenye maeneo ya watu, lakini pia wanakaribia katika barabara ya reli. Naomba sana Waziri atoe tamko kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wapo wafanyabiashara wengine ambao siyo waaminifu na wao wanakwenda tu, wanavamia eneo lolote lile, wanaanza kuchimba mchanga na kuwauzia wafanyabiashara wanaoendesha malori. Naomba sana pia Wizara itoe kauli kuhakikisha kwamba biashara hii haiendelei ili kuhakikisha kwamba ardhi inabaki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nijikite sasa kwenye suala zima la wananchi waliopata ajali ya mabomu katika Jimbo la Ukonga, Gongolamboto. Nitoe masikitiko yangu kwamba, ni mwezi wa saba sasa wananchi wale wanasota, hawajajengewa nyumba, bado wanaishi kwenye mahema, mvua ni zao, jua ni lao. Mvua zimenyesha, wale wananchi wanalala kwenye mvua kwa sababu mvua inapita chini ya mahema. Sasa ni miezi saba wale watu wanaishi kama wafungwa, kama wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tamko la Serikali, Serikali ilikataa kuwapa fedha wakisema kwamba watawajengea nyumba. Hivi hizo nyumba zitajengwa lini? Ninyi mtakuwa mashahidi wangu kwamba hakuna maafa mengine yaliyoweza kupata ufadhili mkubwa wa wananchi kama ajali ya Gongolamboto. Zile fedha zilizochangwa, naomba Serikali itumie mara moja kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata mahali pa kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru pia Waziri kwa kutoa eka 70 kwa ajili ya dampo la Pugu – Kinyerezi. Lakini nimweleze tu kwamba, dampo hili limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Limekuwa na madhara makubwa kwa sababu watu wa Kinyamwezi hawezi kuishi maisha ya kawaida na hawaishi maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea lile dampo, wananchi wananionesha kwenye mti wamefunga neti. Ile neti, asubuhi ndiyo hapo wanaponywea chai, mchana wanalia chakula hapo na jioni wanalia chakula hapo kwa sababu hawawezi kula bila kuwa ndani ya neti kwa sababu ya inzi. Lakini, siyo hivyo tu, yapo madhara mengine. Kwa mfano, ni wiki ya tatu sasa wananchi wale wameshindwa kuendelea na shughuli zao za kiuchumi kwa sababu kumelipuka moto ambao umesambaza moshi katika eneo zima. Kwa hiyo basi, namwomba sana Waziri alifuatilie jambo hili. Nasikia kwamba wamegoma siku tatu zilizopita na sasa vikao vimekwishaanza katika Ofisi za Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka kuliuliza, ni kwa nini Serikali hii inataka kupandikiza kwenye vichwa vya wananchi kwamba hakuna jambo linaloweza kushughulikiwa, ni mpaka wananchi wagome au waandamane? Kama mtakuwa mashahidi wangu, nafikiri vyombo vya habari vimekuwa vinaonesha mara kwa mara ni namna gani lile dampo linakuwa kero kwa wananchi, lakini hakuna kikao chochote ambacho kimekwishafanyika! Vikao vinaanza kufanyika sasa baada ya wale wananchi kugoma. Naomba sana Wizara ya Ardhi ishughulikie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine kwa haraka haraka, la Kipunguni B. Mheshimiwa Rais alipopita wakati wa kampeni aliruhusu eneo la Kipunguni B kubadilishwa matumizi yake kwamba wananchi sasa wanaweza kuruhusiwa kuishi pale na kutafuta sehemu nyingine ya kuwekewa viwanda. Lakini mpaka sasa ni mwaka, wananchi wa pale wameshindwa kupata hati ambazo zingewawezesha kwenda kukopa na kuendeleza sehemu ile. Lakini pia, wameendelea kuishi kwa wasiwasi kwa sababu hawajui hatima yao. Namwomba sana Waziri wakati wa hitimisho, ahakikishe kwmba ananipa jibu la msingi ili wananchi wa Jimbo la Ukonga waweze kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa haraka haraka kwa sababu nimepata sana nafasi nzuri kwenye Wizara hii kuchangia. Lakini, ukiangalia katika kitabu cha Waziri, wanasema kwamba wanajenga nyumba kwa ajili ya kuwauzia wananchi. Namwalika Waziri wa Ardhi aje katika Jimbo la Ukonga ambako kuna nafasi kubwa aweze kujenga nyumba hizo ili wananchi waweze kuhama na wakakute maeneo mazuri katika Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tena kwamba, sitaunga mkono hoja hii kwa sababu Wizara hii imekuwa ni Wizara ambayo imegonganisha sana vichwa wananchi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ya migogoro ya mipaka na kadhalika. Kwa hiyo, Waziri mpaka hapo atakaponiletea majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, nikiangalia ndiyo Wizara pekee inayoweza kuondoa umaskini katika nchi hii, ndiyo Wizara pekee inayoweza ikaondoa umaskini ikiamua kuanzia kesho. Lakini kwa bahati mbaya hawajaamua. Wataamua lini, sijui!

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo linasemwa la ardhi nchini, migogoro ya ardhi. Sisemi kama kuna mgogoro wa ardhi. Liko tatizo la Wizara ya Ardhi kutotatua migogoro yetu. Tukiamua leo kama nchi na toka naingia humu Bungeni, moja ya tatizo la kutatua kwenye ardhi ni kuipima nchi yetu, kila mwenye nyumba apewe hati miliki, kila mwenye shamba apewe hati miliki, ardhi iliyobaki, tujue hii imebaki ni kwa ajili ya kufuga, hii kwa ajili ya kulima, hii ni kwa ajili ya *reserve*. Matatizo ya ardhi nchi hii yataondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kuna jambo gumu nchi hii kupata ni *title deed*. Watu wengi humu ndani hata Wabunge wana nyumba, hawana *title deeds*. Lakini, sababu ni Wizara ya Ardhi. Huwa najiuliza, hivi, nilidhani mtu ukipewa madaraka, lazima useme, katika muda wangu niliacha hiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba leo Profesa aamue, ukikaa miaka miwili, mitatu, miaka mitano, ukiondoka, angalau kila Mtanzania mwenye ardhi, mwenye nyumba mpe hati miliki, utakuwa umemwondolea umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na hati miliki nchi hii mambo yafuatayo yatawezekana, mabenki ni rahisi sasa kukopesha watu kwa sababu tutakuwa tunazo dhamana, *interest rate* za benki zitashuka kwa sababu *risk* itakuwa imepungua, kama wenzetu wamefanya kwa nini sisi

hatuwezi kufanya? Kwa hiyo, naomba Wizara ya Ardhi, jambo hili mlifanyie kazi ni kero kubwa kwa Watanzania. Sioni kama kuna kero kubwa kama kwenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Kigoma Manispaa, akinamama wanashinda pale huoni tatizo, wanatafuta *title deeds* hazipo, tatizo ni nini? Watu wa Mipango miji, hakuna Idara ambayo haifanyi kazi nchi hii kama Mipango Miji, tumeifanya nchi hii kila mtu anafanya anachotaka. Nenda leo pale Dar es Salaam, Mwalimu alitengeneza Osterbay pamoja na Masaki, *it is a shame* kinachoendelea Oysterbay na Masaki leo, ni *as if* Serikali haipo, Wizara haipo. Unajua kuna vitu unaweza ukajiuliza na wanaoongoza kuharibu Dar es Salaam ni viongozi wa Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mikataba ya waliouziwa nyumba wote, waliambiwa msifanye *major operation* kwa miaka ishirini na tano, kaangalie wameziuza, wamejenga maghorofa na hao ndiyo viongozi wanaosimamia kuvunja sheria, nani ambaye hatavunja sheria baada ya hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *National Housing*. Kwanza naomba leo nimpongeze *Comrade* kaka yangu Mzee Chiligati alifanya kazi kubwa, *National Housing* akatupa viongozi vijana wanafanya kazi nzuri, lakini leo wamekuja na ajenda ya kujenga nyumba wauze. Serikali hii leo, tunasema kila nyumba uweke *VAT*, haiwezekani jamani. Hawa wananchi hawawezi, leo nyumba hizi ambazo juzi tumekwenda pale na Waziri Mkuu, tunasema nyumba moja ni milioni mia moja lakini *VAT* asilimia kumi na nane ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nyumba hii ikijengwa kila kilichoingia pale kimelipiwa *VAT, VAT* ya mwisho ya nini? Simenti imelipiwa *VAT,* nondo imelipiwa *VAT,* bati imelipiwa *VAT*, kila ambacho kitaingia kwenye nyumba hiyo kimelipiwa *VAT, VAT* ya mwisho ya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukitaka kununua mbao za kuezekea ni vizuri uende Malawi, mbao ni bei rahisi kuliko za Tanzania kwa sababu mbao za Tanzania tumeweka kodi kila kwenye mbao hiyo. Hatuwezi kuondoa umaskini wa Watanzania kama kweli *we are serious* tunataka kuondoa matatizo ya Watanzania, ni lazima tuache biashara ya *VAT* kwenye nyumba. Leo angalia suala la *National Housing*, naomba wafanye kazi moja, waende nchi hii wajenge nyumba. Leo nyumba Tanzania ni *crisis*, ndiyo maana leo wenye nyumba zao wanaweka bei wanazotaka wao, kwa sababu hatuna nyumba. Kwa hiyo, naomba Serikali tuiachie *National Housing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena lipo tatizo hapa, *National Housing* wakitaka kukopa waombe kibali Wizara ya Fedha, hivi *bureucracy* ya nini? Sheria hii iliwekwa mwaka 1975 ili makampuni yetu ya ndani yasiende kukopa nje bila kuomba Wizara ya Fedha, leo Wizara ya Fedha haiwapi dhamana *National Housing*, haiwapi chochote, lakini tuna wa-*demand* waende kuomba kibali ili wakope wakati leo nchi hii ina *demand* kubwa ya nyumba, watu hawa wakikopa wana ardhi watajenga nyumba, nyumba zikiwa nyingi, bei za nyumba Dar es Salaam na miji yote zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema kama kuna kitu kinaumiza Watanzania ni nyumba, leo nyumba ukienda pale Sinza chumba kimoja shilingi laki mbili, laki tatu, *what kind of a nation*? Ni mara mia moja uende ukanunue nyumba South Africa ni bei rahisi kuliko kununua nyumba Mbezi *Beach*. Nchi hii tukiamua tutaweza kuondoa umaskini. Kwa hiyo, naomba moja, suala la *National Housing* wajenge nyumba Dar es Salaam, zile nyumba ndogo ndogo zilizojaa, nendeni mkajenge nyumba, mkimaliza yule aliyekuwepo mpeni na yeye nyumba moja, zingine wapeni watu wengine nchi hii ndiyo itaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watapanga Mji na Vijana wetu wakimaliza Chuo Kikuu anapewa nyumba, leo nyumba ukikopeshwa hata nyumba hizi, unalipa ndani ya miaka kumi uliona wapi? *The mortgage financing* inavyofanyika duniani kote ni miaka ishirini mpaka miaka thelathini ili interest iwe kidogo. Tukifanya hivyo tutaweza kuwapa Watanzania wote nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala la *National Housing,* suala la VAT hapana, suala la kuomba kibali kukopa hapana, lakini pia wapo watu pale Dar es Salaam wajanja,

wamekaa nyumba za *National Housing* miaka yote, wao wamejenga nyumba Osterbay, Masaki, leo wanasema wauziwe zile nyumba, tena wauziwe kwa bei ya zile hela walizotoa kwa miaka yote, mliona wapi hii biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaosema wauziwe nyumba wao wana nyumba tatu au nne wenye shida, hapana! Jamani haliwezi kuwa Taifa la kusaidia walio nacho peke yake hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitengeneza sheria hapa ya kumiliki sehemu ya jengo, inaanza kutumika lini? Hatuwezi kuwa tunatengeneza sheria kila siku hapa, halafu hazitekelezwi. Wizara ya Ardhi naombeni muisadie nchi hii, mkiisaidia nchi hii tutaondoka kwenye umaskini kwani ndiyo Wizara peke yake inayoweza kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo katika nchi hii linasemwa sana kuhusu Wawekezaji na hasa imesemwa leo na watu wa Upinzani la *AGRISOIL*. Naomba uniruhusu nisome kitabu, ni historia ya Singapore kwa nini walifanikiwa sana. Naisema hii ili niweze kujenga hoja yangu *on AGRISOIL*, Waziri Mkuu wa Singapore wa kwanza alisema naomba nisome kwa Kiingereza, *The accepted wisdom of the whole economist at the time was multinational campanies were exploitors of cheap land, labour and raw materials, these depandant school of economics argue that, multinational campanies continue the colonial pattern of the exploitation that led development countries like Tanzania* kwamba anakuja kuchukua *raw material* zetu anasema*, third world leaders believed this theory of neo-colonialist exploitation but, Lee Kuan Yew, were not impressed But he said, if multinational companies could give our Tanzanians workers employment, technology let them come.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli leo tunasema tuna ardhi, Kigoma hekta elfu kumi tumewapa *AGRISOIL*, hizo hekta elfu kumi ilikuwa ni makazi ya wakimbizi, pale Lugufu, yote ina hekta elfu ishirini na tatu, hekta elfu kumi na tatu tumewagawia Watanzania, wana Kigoma mpaka leo hakuna aliyelima hata heka moja. Tunasema huyu anakuja anasema nikilima hawa wote wanakuwa *outgrowers,* nitawapa mbegu, nitafanya nini, kwa kufanya hivi ndiyo nchi yetu itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasema shilingi yetu inaanguka, sababu ya shilingi kuanguka ni kwa sababu hatuna *exports*, kwa hiyo kile ambacho tunaweza tuka-*minimize* tukaweza kupata *optimal* ya *export* tufanye. Ardhi ile ya Mpanda ilikuwa ya Wakimbizi, leo tunasema watu wasilime hiyo kampuni inayokuja, haiwezekani kuna Watanzania hapa ni wazuri Watanzania wengine ni wabaya, haiwezekani! Hili Taifa leo tunapiga kelele tuna njaa, watu wanakuja wanataka waweke teknolojia, kama kwenye Kilimo hatufanyi *mechanization,* hiyo ardhi hata tukae nayo miaka mia moja haitatusaidia kama Taifa. Namna pekee ya kuondoa migogoro hii ya ardhi ili watu wajamaa waliobaki, maana katika nchi hii kuna wajamaa waliobaki ambao hata wale walioanzisha ujamaa hawapo tena, ninachosema ardhi ipimwe, kila anayetaka ardhi apewe, inayobaki tujue ni ipi tunaipeleka kwenye biashara, ni ipi ambayo tunawapeleka wafugaji wetu. Tukifanya hivyo ndipo tutaweza kuisaidia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nirudie kuongelea suala la bei za nyumba. Wenzetu wamesema tuweke *authority* ya kusimamia, wala hiyo siyo *solution*. Tumeondoka huko, uchumi hauko tena wa ku-*regulate*. Namna bora ya kufanya ni kuongeza *supply* ya nyumba na wanaoweza kuifanya kazi hii siyo wengine ni *NHC*, *National Housing* wajenge nyumba wauze, wajenge nyumba za kupangisha. Lakini hizo *rate* za kupangisha tujue, hili shirika ni letu, ni shirika la Serikali, hawawezi kwenda kushindana na soko, hapana! Tunawaambia wauze, zingine wapangishe, wajenge maghorofa mengi, vijana wanatoka Chuo Kikuu wakifika wana mahali pa kwenda kukaa. Kama watu wamekaa Upanga kwa hela ndogo kwa miaka yote, haiwezekani kizazi chetu sisi, ndiyo tuanze kuwa *punished* hatuko tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba tusimamie sheria za nchi yetu, naomba Waziri usimamie sheria, tuache maneno mengi yamezidi, umefika wakati wa kutenda, hatuwezi kuwa tunaongea kila siku mambo ambayo hayawezekani. Leo tunataka kujenga Chuo Kikuu cha Muhimbili amesema Mama pale, hatulipi fidia mpaka leo maana yake nini? Kwa nini tunajizuia

maendeleo? Tukijenga Chuo Kikuu kile jamani ndiyo *legacy* ya CCM hiyo, ndiyo *legacy* ya Rais huyu, tulipe zile fidia ili Chuo Kikuu kianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, lakini naomba Waziri aje na majawabu ya mambo niliyoyasema. Jambo la kwanza, *VAT,* hapana. Pili, hatutaki *National Housing* iwekewe mizengwe, iachwe ifanye kazi. Tatu tusimamie nyumba nyingi zijengwe ili bei za nyumba za makazi zipungue. Jambo la Nne na la muhimu ni *Title Deeds*, nchi hii haina *Title Deeds* na huu ndiyo ukombozi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba na kule Kigoma wamekusikia. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea naomba nimwite Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Hasnain Murji ajiandae.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pili, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na wenzangu kuwapongeza Waislam wote waliofunga katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani na kumaliza kumi la rehema na sasa tupo katika kumi la *maghfira*, naomba Mwenyezi Mungu atusaidie, atusamehe dhambi zetu zote. Vile vile nawashukuru sana Wabunge wote ambao wanatuunga mkono katika mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda mbele, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri katika kitabu hiki. Kwa kweli mikakati aliyoiweka ni mizuri. Hapa kuna masuala mawili tofauti, suala la kuandika na utekelezaji, ninachomwomba Waziri kama kweli aliyoyaandika humu ni kwa dhati, naamini kwa sababu ya uzoefu wake mkubwa alipokuwa nje, naomba sasa atolee macho yake mawili katika *implementation*, kama kweli wakifanikiwa hili, watasaidia kwa kiasi fulani. Lakini nina wasiwasi mkubwa kutokana na uzoefu unavyojionesha hapo nyuma katika utekelezaji kazini kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie mada iliyo mbele yetu kwa kuanza na ardhi na nitajikita zaidi katika ardhi. Ardhi ni mali, ardhi ni nyenzo muhimu sana katika maisha ya binadamu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Sote tunafahamu kuwa kwa sasa hii Watanzania hasa wa Vijijini tegemeo pekee kabisa kwao ni ardhi kwa familia zao na kwa uchumi wa Taifa kwa ujumla, ninachoomba utandawazi, uwekezaji, soko huria, isiwe sababu ya kuchukua ardhi yote ya Tanzania na kumwacha Mtanzania wa kijijini ambaye ni maskini na fukara kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo nina sababu, ninaomba nizungumzie mfano halisi wa upande wa Tanga. Matatizo katika Wizara ya Ardhi ni migogoro iliyopo kwa sababu ya sheria ambazo ni mbovu, Tanga katika Kijiji cha Pande B, kuna mgogoro mkubwa kabisa wa ardhi kwa sababu ya mfumo mbovu uliopo kwa wawekezaji. Waheshimiwa wengi hapa wamezungumzia mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango miji na Wawekezaji ndiyo tatizo kubwa kabisa linalopelekea migogoro katika maeneo yetu, hao Maafisa Mipango Miji ni watendaji wa Halmashauri ambao kwa kweli ninaweza kusema ni wabinafsi wa hali ya juu, vile vile hawana uzalendo, na ubinadamu kwa upande fulani kwao ndiyo umekufa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu uliopo Pande B, umeanza tangu mwaka jana mwezi wa kumi, hapo ndiyo ulikuwa umekolea, ulianza mapema kidogo wakati wawekezaji ambao ni Tanga *Cement* walipokuwa wanajipanga kwa ajili ya kwenda kuomba eneo hilo, mpaka kufikia mwezi wa kumi kabla ya uchaguzi mgogoro huu ulikuwa umekolea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mkubwa kwanza kabisa Wawekezaji wale hatua za mwanzo zilifuatwa, walikwenda kwenye mkutano wa Kijiji wakaomba eneo lile la Pande B ambalo lina ukubwa wa kilomita moja na nusu sawasawa na ekari 371 na wanakijiji wale walikubali. Mgogoro ulianza wakati wa kufanya tathmini katika maeneo yao. Kuanzia hapo

hawakushirikishwa hata kidogo. Maafisa wa Mipango Miji walichofanya walikwenda katika maeneo ambayo kwa wanakijiji wale ni maeneo muhimu sana kwao kwa sababu walikuwa wakilima mazao ya kudumu, kulikuwa na minazi, miembe, na mazao ya muda mfupi, kulikuwa na makaburi, walikuwa na eneo la kuweza kuchungia wanyama wao kama ng'ombe, kondoo na mbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichofanya ni kwamba walipima kwa ujanja ujanja ambalo ni kosa la kwanza walilolifanya. Pili, hawakuwapa fomu namba 69, ambayo ni muhimu sana kwani ndiyo inayoonesha vitu vyote vitakavyofanyiwa tathmini. Wanakijiji walipohoji siku hizi wanakijiji wote siyo kama hawaelewi, afadhali kidogo shule za Kata zimesaidia, kuna vijana wana uelewa mzuri. Walipohoji mbona hatukupewa fomu namba 69, Afisa Mipango Miji Ndugu Mapunda akawajibu kuwa kama mnaona mnadhulumiwa nendeni Mahakamani. Kwa hiyo amewadhalilisha kwanza, amewadharau wanakijiji wale, ndivyo ambavyo walijisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Tanga *Cement*, baada ya kufanya tathmini na kutokuwapa kila mmoja kujua ana ekari ngapi, kampuni ya Tanga *cement* ikalipa, ikatoa pesa zile kwa Halmashauri, awamu ya kwanza walilipa milioni 345, pesa hizo ziligawanywa kwa Serikali ya Kijiji ilipata milioni 26 kwa wakati huo, sijui ni kweli, zipo kwenye akaunti au nazo zimeliwa. Kwa baadhi ya wanakijiji waliobahatika kupata fidia hiyo ambao ni wachache tena waliwalipa kwa kuwalaghai kwa sababu ilikuwa ni mwezi wa Ramadhani na sikukuu inakaribia, wakawaita, wakaona hawana jinsi kwa sababu ni maskini bila kuambiwa una heka ngapi. Aliyelipwa laki saba, aliyelipwa milioni mbili, ambapo kwa jumla haifiki hata milioni hamsini kwa wale baadhi waliolipwa, wengine waligoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukiangalia pesa zote zilizobakia milioni takriban mia mbili na zaidi hazijulikani zilikokwenda. Hii inaonesha kuwa, pesa zote hizo wamezitafuna bila ya imani, bila ya huruma, bila ya hofu hata ya kumuogopa Mwenyezi Mungu. Hapa kuna tatizo kubwa sana katika kijiji hiki na uongozi wa Mipango Miji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Wanakijiji ambao walikuwa wanadai walikuwa ni 30 katika orodha, lakini watu wa Mipango Miji kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji ambao nao waliwaingiza katika mtego waliongeza watu hewa 36, kwa hiyo jumla wakawa watu 66. Wanakijiji wale hawakukubali saruji kuchimbwa katika eneo lao, waligoma na walikaa kikao wakaunda Kamati Ndogo ya kwenda kushughulikia tatizo lao hilo. Walikwenda kwa Mkurugenzi na wengine walijigawa kwenda kwa mwakilishi wa saruji. Saruji alipoona matatizo yanaongezeka akaongeza milioni 70 ili walipwe wale wanakijiji ambao wana malalamiko. Kwa taarifa nilizonazo, hiyo milioni 70 mpaka sasa hivi iko Halmashauri haijagawiwa kwa sababu kila leo wanaongezeka watu, au yanaongezeka madai mapya, ndio sababu walizozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla fedha zote zilizolipwa na mwekezaji huyu saruji milioni 415. Kwa haraka haraka ukiangalia zoezi zima la uthamini mpaka ulipaji fidia lilikuwa na kasoro nyingi pamoja na usiri mkubwa na limegubikwa na mazingira ya rushwa tena ya hali ya juu. Mkurugenzi akaona njia pekee ya kuwatuliza wanakijiji ni kuunda Tume, Tume ikaundwa ya kuchunguza, Tume ile imechukua takriban miezi mitatu bila kutoa taarifa yoyote. Mkuu wa Wilaya hali kadhalika alikuwa na Tume yake lakini hakuna ambacho wamekuja nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale wanacheleweshwa kila leo wanapewa taarifa mpya na huku mwekezaji cha kushangaza sasa tarehe 13 Juni, 2011 saruji walipata ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya na kwenda kuchimba tani 5000 za majaribio kwa malighafi hiyo. Ni udongo ambao unachanganywa na *material* nyingine kutengeneza saruji. Wanakijiji wale walistuka sana na hawakukubaliana na hilo lakini alichofanya Mkuu wa Wilaya aliwashirikisha baadhi ya Viongozi wa Kijiji na Kata ambao wamepata marupurupu haya, wakaenda kwa nguvu katika eneo hilo wakasafisha eneo wakaweka ulinzi mkubwa ili mwekezaji yule achimbe. Sisi tunasema kuwa Tanzania tuna amani kama kweli, wanakijiji wale wameridhia Mtendaji yule kwa nini kumewekwa ulinzi mkubwa wa mgambo na marungu na mapanga ili mwekezaji yule aweze kuchimba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Hasnain Murji nimeletewa tangazo na Ofisi ya Bunge, naomba niwasomee kama ifuatavyo: Nyumba za Kuishi Kwenye Mradi Medeli. Naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi anawajulisha Wabunge wote kuwa Wizara yake kupitia Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing Cooperation)* wapo hapa Bungeni kwa ajili ya kuuza nyumba za kuishi kwenye mradi wa Medeli uliozinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 13 Agosti, 2011. Kituo cha Mauzo kipo kwenye viwanda vya maonyesho ya Bunge kuelekea jengo la habari, Wabunge wote mnakaribishwa kupata maelezo zaidi na kuchukua fomu na kuziwasilisha kwa Kaimu Katibu wa Bunge, Ndugu John Joel.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu. Lakini naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye rehema nyingi ambaye ameweza kunifikisha siku ya leo na kuweza kusimama hapa na kuweza kuja kutoa mchango wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa Hotuba yake, nimeisoma, nimeridhika nayo, namshukuru na nampongeza. Lakini pamoja na kumpongeza nina imani kubwa kwa kipindi kifupi alichokaa Wizarani tumeanza kuona dalili na tumeanza kuona mabadiliko. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, akaze buti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kumpongeza naomba nichukue nafasi hii kutokuunga mkono hoja. Siungi mkono hoja kwa sababu kuna vitu nimetumwa na wapiga kura wangu, nitakapopata majibu basi nitaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mji wa Mtwara Mikindani, ulipata hadhi ya kuwa Mji Mwaka 1963. Ndipo ikaanzishwa Halmashauri ya Mji wa Mtwara Mikindani. Hata hivyo, Historia ya Mji huu ilianzia mwaka 1948 wakati Serikali ya Kikoloni ya Mwingereza ilipoamua kuihamisha Bandari kutoka Mikindani na kuileta Mtwara kwa vile ilikuwa bandari kubwa *(Deep Labour)* hapo ndipo Mji ukaanza kuendelezwa. Hiyo ni mwaka 1963. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004, tukaja kupata heshima ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani. Lakini heshima hii tuliyopata ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kulikuwa na vigezo, kulikuwa na masharti ambayo lazima yafanyike ili tuweze kupata hadhi ya Manispaa. Sharti mojawapo ni kwamba, tulikuwa hatukidhi hadhi za watu na vitu vingine. Kuweza kukidhi haja ya kuweza kupata Manispaa basi tulipanga tuweze kupata Kata mbili kutoka Halmashauri ya Mtwara Vijijini ambayo ni Kata ya Ziwani na Kata ya Namayanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama mbele yako hapa leo, ninao muhstari wa vikao ambayo Waheshimiwa Madiwani wa Mabaraza walikaa, walikubaliana kwamba, hizi Kata mbili sasa zije ndani ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, wakakubaliana Vikao vya *RCC,* vimekaa vikakubaliana, tukaleta huku juu wakakubali na wakasema sasa Kata hizi zitatoka Mtwara Vijijini na kuja Manispaa ya Mtwara Mikindani. Nasikitika kusema tangu mwaka 2004 mpaka leo Kata hizi hazijafika bado Mtwara bado ziko huko ziliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*windup* basi aidha, aifute hadhi ya Manispaa ya Mtwara Mikindani hatuna hadhi kama Kata hizi mbili haziingii pale, la sivyo basi atamke sasa rasmi kwamba Kata ya Namayanga na Kata ya Ziwani ziko ndani ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani. Tunashindwa kufanya mambo mengi, Mheshimiwa Rais, juzi alikuwa yuko Mtwara ameongea na wawekezaji wakubwa, leo nchi hii na hata nchi mbalimbali inaiangalia Mtwara leo kwa jinsi rasilimali za gesi na Mungu akitujalia hata mafuta tutapata. Sasa hivi kila mtu anaiangalia Mtwara na sisi kuweza kupanga mji, ule mji ulishabana haya maeneo mengine tuliyoyaomba yaje basi ni ili tupange Mji, Mheshimiwa Waziri ili hawa wawekezaji wakija wasipate tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, haya ni makubaliano ambayo tumeshakubaliana tayari, vikao vimekaa na ushahidi upo. Sasa kuna nini kinachotukwamisha sisi kuhamisha Kata mbili zile kuja mjini? Tunataka jibu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee, sisi tuna mji leo ndani ya nchi yetu Mikoa miwili tu ndio inayofanana ni Mtwara-Mikindani na Kigoma-Ujiji, tuna Mji pale unaitwa Mikindani ni Mji wa kihistoria. Tangu sijazaliwa watu wako pale, marehemu baba yangu alikuwa anafanya kazi pale bandarini Mikindani, wazee wameacha majumba yao mpaka wamekuwa wameacha na urithi wa majumba kwa watoto wao. Leo tuna tatizo ndani ya Mji wa Mikindani, tunaambiwa ule mji hawawezi kupima na kutoa hati. Wale watu wamejenga wazazi wetu wameacha majumba pale kwa miaka mingi, wametuachia urithi sisi watoto, leo tunaambiwa kwamba hamwezi kutupimia, mkatupa hati eti kwa sababu Mikindani iko *below sea water*. Hivi Bagamoyo, Kilwa, Lindi na maeneo mengine ya Zanzibar hayafanani kabisa na Mikindani? Kwa nini wenzetu wanapimiwa na wanapata hati, sisi tusipate?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba ule Mji ni Mji wa kihistoria kuna wawekezaji wengi wanataka kuja kuwekeza, wanataka kujenga Mahoteli makubwa na kadhalika, lakini wanashindwa kwa sababu tunaambiwa kwamba hatuwezi kupima. Mheshimiwa Waziri tunaomba utufikirie utumie ujuzi wako na maarifa yako ili watu wa Mikindani sasa wapimiwe, wapate hati miliki ili na wao waweze kujidai pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Halmashauri ya Miji na Manispaa hakuna hati ya mashamba. Lakini sisi bado tuna vijiji ndani ya Manispaa yetu ya Mtwara Mikindani. Tuna kijiji ambacho kiko mbali na Mji kinaitwa Lwelu, Naliendele, Mbawalachini, Mkunjanguo, huko kote vijijini watu bado wana mashamba wanalima. *Master plan* yetu ya Mji kuweza kuwafikia kule inaweza ikachukua zaidi ya miaka 10 au 15. Lakini wale watu leo wanakosa kupimiwa wakapata hati hata za kimila. Mheshimiwa Waziri tunafanya nini miaka 10 mtu kukaa unasubiri mpaka *master plan* ya mji ifike kule, wale watu wanateseka. Leo mtu ana shamba lake zuri ambalo anapata mazao yake mazuri anakuja kukwama kwenye pembejeo anaambiwa kwamba lete dhamana ya shamba lenye hati hana dhamana, kwa hiyo, anashindwa kuendelea na anashindwa kujiendesha. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, alifikirie pia suala hili kwamba hivi vijiji ambavyo viko katika Miji na vipo katika Manispaa ambayo *master plan* yetu kufikia kule itachukua muda mrefu sana. Sasa tunamwomba sana atuangalie, halafu atujibu kwamba tunafanya ili wale watu nao wajisikie na waweze kupata hati hata kama ni za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Ilani yetu ya Uchaguzi, ukurasa wa 60, tunasema kwamba tutapeleka huduma za Ofisi za Ardhi katika Mikoa na hususan imeelekeza kabisa kwamba tutapeleka huduma ya ardhi Kanda ya Mtwara kwa maana kwamba tuwe na ofisi ya Kamishina wa Mtwara. Ofisi ya Kamishina wa Mtwara imeanzishwa tangu mwaka jana, lakini ofisi hii haifanyi kazi. Watalaam wapo, wasiokuwa na kazi kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Tatizo linasababishwa na kwamba Kamishna hayupo pale, Mheshimiwa Waziri hajateua Kamishna bado. Tuna ofisi ya kanda ipo, watalaam wapo lakini tatizo Kamishna hayupo. Sasa leo ukuaji wa Manispaa yetu ya Mtwara inakua sana na ile huduma ilikuwa ni kwa sababu ya Kanda ya Kusini, Mikoa yote ya Kusini iweze kupata huduma haraka pale. Leo ukitaka hati mtu yeyote wa Mtwara inachukua zaidi ya mwaka mmoja na nusu au miwili ndio unaweza kupata hati wakati tuna Ofisi ya Kanda iko pale lakini tatizo ni Kamishina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri ajibu na tunaomba amteue Kamishna haraka iwezekanavyo ili aweze kuja kutoa huduma ile pale ili tuweze kupata huduma za hati kwa muda mfupi. Ni kero sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu pale hati zinasafirishwa mpaka Manispaa wakusanye zile hati, ziwe sijui 50 au ngapi, wachange nauli ndio wamtume mtu aje Dar es Salaam, wakati Ofisi ya Kanda iko pale lakini Kamishna tu hayupo. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri, sisi pale kuna eneo ambalo tunazikana tunaita Makaburimswafa, lile eneo sasa limejaa, imefikia hatua sasa tunachimbua kaburi tunazika juu ya kaburi, ndio hatua tuliyofikia kwa sababu eneo limejaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeleka ombi kwa Mheshimiwa Waziri, tumeandika barua kwake na imepelekwa ofisi kwake, kwamba, kuna eneo moja la magereza, ile barabara kama unakwenda Newala kwa upande wa kulia, wana eneo kubwa sana. Wale watu wa Magereza pale Mtwara wana eneo kubwa ambalo halina kazi. Tumeomba lile eneo, tuweze kulitumia kwa ajili ya kuzika ili tuache kuzikana juu ya maiti. Tunaomba sana, hilo ombi tumelileta kwake, tunaomba Mheshimiwa Waziri akalifikirie na atukubalie ili tupate hilo eneo ili basi itikadi zote na dini zote tuweze kuzikana pale kwani hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, tunaomba sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi lingine tena, tumepata shule, eneo la bandari kulikuwa na eneo kubwa sana la Mamlaka ya Bandari katika Kata ya *Railway* na tumefanya mazungumzo na Mamlaka ya Bandari wamekubali wametupa lile eneo tumeshajenga tayari madarasa manne, tumeshajenga matundu ya vyoo 16 na tuko kwenye hatua ambayo tumeanza kujenga maabara, ile shule tunataka iwe *high school*. Lakini kuna eneo ambalo wanahodhi watu wa *TBA* na kwa sababu nyumba zile zote za Mamlaka ya Bandari zimechukuliwa na *TBA,* sasa Mheshimiwa Waziri tumeomba watu wa *TBA* watuachie lile eneo. Sisi kama Manispaa tuko tayari kuwatafutia eneo lingine tuwape na tunalo lakini hawataki. Tunaomba Mheshimiwa Waziri nalo hilo aliangalie, atusaidie ili tuwe na *high school* ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie hapo, niseme kwamba, baada ya kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri ndio nitaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja hii. Naomba nianze kwa kusema kwamba na mimi siungi mkono hoja. Nataka nitoe sababu zangu sita za msingi kwa nini siungi mkono hoja. Awali ya yote nataka kuwatakia Waislam wote wanaofunga katika mwezi huu Mtukufu wa Radhamani Kareem. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni rasilimali ya mnyonge, ni kitu pekee ambacho anacho. Ni lazima sasa tuwe na utaratibu mzuri na madhubuti kwa kuhakikisha kwamba matumizi ya ardhi yetu yanaratibiwa yanasimamiwa na uwekezaji unaofanyika katika nchi yetu uwe wa makini. Naomba nianze kutoa sababu kwa nini siungi mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, kule katika Kata ya Pembamnazi kuna mwekezaji anaitwa Amadori. Mwekezaji huyu kachukua eneo kubwa sana la Kata ya Pembamnazi. Hakuna maendelezo makubwa ambayo yanafanyika pale, wananchi wale wanalalamika, hawana sehemu za kulima wala kujenga makazi yao, nataka kujua mkataba ambao anao mwekezaji huyu ni wa aina gani, uhalali wa mkataba huo na kwa nini ardhi ile isitwaliwe na kugawiwa wale wananchi ambao wana shida kubwa sana ya ardhi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili, kwa nini siungi mkono hoja hii katika mradi wa viwanja 20,000 kule Kibada, wananchi wale waliuziwa viwanja na Serikali hii hii kupitia Wizara ambayo inawasilisha bajeti yake leo hii. Kuna maeneo pale Kibada wamepimiwa viwanja lakini barabara na miundombinu mingine haikutengenezwa. Wananchi wale wamejenga nyumba lakini hawana njia za kufikia katika makazi yao. Hii ni dhuluma kubwa sana ambayo inafanywa na upande wa Serikali. Nataka kujua mkakati ambao Wizara inao kuhakikisha kwamba wale wananchi wa kule wanajengewa zile barabara kwa sababu walipokuwa wanalipa zile gharama za viwanja walilipia pamoja na gharama za miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tatu kwa nini siungi mkono hoja, kuna wananchi takriban 105 ambao walikuwa na maeneo yao, makazi yao na kujishughulisha katika masuala ya kilimo maeneo ya *Dungu Farm* nikiwemo mimi mwenyewe pamoja na wazazi wangu. Naomba ni-*declare* interest kwamba mimi na wazazi wangu tulikuwa na maeneo pale. Tathmini iliyofanyika watu walilipwa mazao lakini watu ambao walikuwa na nyumba na waliofanya maendeleo pale hawakulipwa hata senti tano. Sasa nataka kujua kupitia Waziri husika ni taratibu gani ambazo zitatumika ili wale watu waweze kupata haki zao za msingi ambazo wamekuwa wanazungushwa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya nne kwa nini siiungi mkono hoja, katika eneo la Vijibweni, Wizara ya Ardhi bila kufuata utaratibu, imevamia eneo lile na kutaka kutwaa takriban

heka 240 bila kushirikisha Viongozi, bila kufuata taratibu na sheria za nchi kwa *pretext* kwamba wanataka kujenga Bandari. Sasa kama kule Kurasini kunawashinda, kwa nini mnataka kuja Vijibweni na kuwahangaisha wananchi? Huu mpango ambao mnataka kuja nao, una *fit* namna gani katika Mji Kabambe wa Kigamboni? Cha kusikitisha zaidi katika suala kubwa na la msingi namna hii, Wizara inadiriki kutuma Maafisa wa ngazi za chini kwenda kukaa na kuongea na wananchi pasipo kufuata taratibu. Naomba zoezi hili lisitishwe na taratibu za msingi ziweze kufuatwa. Hata kwa suala la msingi kama upanuzi wa Bandari, lazima taratibu za msingi zifuatwe. Mheshimiwa Waziri naomba sana zoezi hilo lisitishwe ili utaratibu wa msingi uweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tano kwa nini siungi mkono hoja, katika eneo la Kisota, kuna viwanja 20,000 vilivyopimwa na Serikali, lakini watendaji wa Wizara ya Ardhi, wamepima na kutoa kwa wananchi viwanja vichache kuliko maeneo ambayo yamepimwa. Sasa hivi pale Kisota kuna mapori mengi kweli kweli, hali ambayo imepelekea kuwa na hali kubwa sana ya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Wizara husika, wafanye *audit* ya maeneo yaliyopimwa na idadi ya viwanja vilivyotolewa kwa sababu wajanja wachache ndani ya Wizara ya Ardhi wanachokifanya sasa hivi, wanapita tena katika yale maeneo na kuanza kutoa kiwanja kimoja kimoja. Kwa hiyo, naomba hili suala lifuatiliwe, *audit* iweze kufanyika na yale maeneo ambayo tayari yamepimwa lakini viwanja havikutolewa basi hayo maeneo yaweze kutolewa kwa wananchi ambao wanahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya sita kwa nini siungi mkono hoja, ni suala la Mji mpya wa Kigamboni na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wameniunga mkono katika suala hili. Suala hili ni kubwa na suala hili ni zito, lakini suala hili Serikali mnalichukulia kimzahamzaha. Wanakigamboni wanataabika tangu wameingia kifungoni Oktoba mwaka 2008 na hawana matumaini ya kutoka kifungoni. Hawajui tarehe ambayo mtawatoa kifungoni, Serikali imekuwa kimya mno na majibu ambayo yamekuwa yakitolewa ikiwa pamoja na yale ambayo yametolewa katika hotuba hii, kwa kweli hayaashirii kwamba Serikali inawatakia neema Wanakigamboni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kigamboni, hawawezi kuuza ardhi yao, hawawezi kuuza nyumba zao, hawawezi kuziendeleza na hawakopesheki. Kwa takriban miaka mitatu sasa hivi, hakuna kitu chochote cha maana ambacho kinaendelea pale Kigamboni na maswali ambayo Wanakigamboni wanayo na wangependa kupata majibu ni maswali manne tu. Mradi huu utaanza lini? Mradi huu utaanzia wapi? Haki zao za msingi ni zipi na hatima yao ni ipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa miaka mitatu Serikali hii imekuwa inapiga chenga kutoa majibu ya maswali haya ya msingi. Nasikitika kusema kwamba sitaunga mkono hoja mpaka majibu ya haya maswali manne ya msingi yaweze kupatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, nitakubali mradi huu ikiwa tu mambo mawili yatafanyika; moja wananchi wa Kigamboni wanufaike na pili wananchi wa Kigamboni wasisumbuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kigamboni wamenituma, Serikali ilipotoa tamko ilisema kwamba ndani ya miaka miwili wangekuwa wameanza mpango wao, sasa wameshapita hiyo miaka miwili. Wananchi wa Kigamboni wamenituma, itakapofika tarehe 30 Juni, 2012 hawataki kusikia tena kuhusiana na masuala ya mradi huu. Naomba nirudie, wananchi wa Kigamboni wamenituma, kama Serikali haitakuja na mpango thabiti, itakapofika tarehe 30 Juni, 2012, hawataki tena kuusikia mradi huu, chukueni mradi huo pelekeni sehemu nyingine yoyote, lakini baada ya hapo wananchi wa Kigamboni hawataki na hawatatoa ushirikiano kwa Serikali katika suala hili. Ni vema Serikali inapokuja na miradi kama hii, muwe mmeshajipanga, sio mnatoa zuio wakati wenyewe hamjajiandaa. Kuna matatizo ya msingi na nilipokuwa naangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 26 na 27, wanasema bado wako kwenye mchakato; wakati wananchi wa Kigamboni wanaumia, Serikali iko kwenye mchakato, wakati wananchi wa Kigamboni wanaendelea kuwa maskini, Serikali iko kwenye mchakato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa Wabunge wenzangu, naomba mniunge mkono, naomba tusipitishe hii bajeti ya Wizara mpaka pale Serikali itakapokuja na majibu ya msingi, najua ndani ya Bunge hili Tukufu kuna Wabunge zaidi ya 50 ambao ni wakazi au wamewekeza katika Jimbo la Kigamboni, naomba waniunge mkono katika hili, tuwatetee wananchi wa Kigamboni, naomba bajeti hii isipite mpaka pale majibu ya msingi yatakapoweza kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tena, kauli ambayo nimeitoa kwamba baada ya tarehe 30 Juni, 2012, kama Serikali hamtakuja na mpango thabiti ambao unaainisha na kujibu masuala ya msingi, naomba msije tena Kigamboni. Mimi nitakuwa wa kwanza kuwasimamia na kuwatetea wale wote ambao watakuwa wamevunja agizo la Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu muwe makini, mkajipange, mje na mpango thabiti ambao utaonesha lini na wapi mnaanza na mnaanza na nini, haki za Wanakigamboni zitakuaje? Naomba niseme wananchi wa Kigamboni katika masuala ya fidia wanataka mambo matatu; kwa wale ambao hawatoweza, wapewe fidia yao na wahame na fidia iwe katika bei ya soko. Wale ambao watakuwa na uwezo wanataka kuingia ubia na wawekezaji na wengine ambao wana uwezo mkubwa zaidi wanataka kuyaendeleza yale maeneo yao wao wenyewe, watachukua fedha benki, watafanya hiyo kazi. Kwa hiyo, naomba utaratibu huo utumike, najua kabisa Mheshimiwa Waziri ana uzoefu mkubwa, wananchi wa Kigamboni wana imani ingawa majibu yake ya tarehe 31 Machi, 2011 hayakukidhi haja. Kwa hiyo, naomba arudi tena akiwa na majibu ya msingi katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, siungi mkono hoja. (*Makofi)*

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu vile vile kwa kunipa fursa na pumzi kuwepo hapa pamoja na wewe na Watanzania wote na Viongozi wetu wote. Nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Ilala kwa kunisaidia na kushirikiana na mimi katika maendeleo ya Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi naanza kwa kauli thabiti na swaumu yangu siungi mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja, narudia maneno kwanza aliyoandika Mheshimiwa Waziri kwa maneno mazuri na matamu na kuya-*highlight* kwa maandishi makubwa anaposema kuwa Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maeneo ya kupumzika, tunakubali kabisa Jiji la Dar es Salaam halina maeneo ya kupumzika. Lakini Jiji la Dar es Salaam sio halina maeneo ya kupumzika tu, halina hata maeneo ya kuegesha magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika eneo ambalo umeliona mnataka liwe eneo la kupumzika, ni eneo la Jangwani, nakubaliana na wala sikubali kabisa mazingira ya watu wanaoishi Jangwani kwa hali ile. Lakini hawana budi kuishi vile kutokana na umaskini ambao wanao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama kuna mpango ambao unaletwa na Serikali Jangwani na Mchikichini na maeneo yote ya Majangwani yaliyoandikwa hapa, ni lazima yashirikishe wananchi wenyewe waliohusika. Ni lazima washirikishe watu waliowakuta katika maeneo yao, sasa kama mnataka kufukuza watu Mchikichini na maeneo ya Jangwani, ili muweke maeneo, mkitoa Oystebay mje kula *ice cream* pale, hatukubali. Tutabanana hapo hapo na ikibidi niko radhi mimi Mussa Azzan Zungu, Mbunge Jimbo la Ilala kujiuzulu Bunge, kujiunga na wananchi na kwenda Mahakamani kuzuia mpango huu kama hamtashirikisha wananchi waliokuwepo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema kuna agizo la Rais, na sisi tunaheshimu, mbona kuna agizo la Rais kuuza nyumba mlishindwa wala hamtaki kuuza nyumba? Kwa hiyo, huo upepo wa Jangwani na sisi tunataka tupumzike. Nilikuwa nategemea mseme mnakuja na mpango. Mheshimiwa Waziri umenitia hofu, sasa hivi Jangwani watu hata kufuturu hawajui watafuturu wapi, roho zao zimewaruka na mimi nawathibitishia wananchi wote mabondeni, tulieni, tutakaa na

Serikali kufikia muafaka wa kuhakikisha wananchi wale hawadhalilishwi. Nakataa kabisa kauli ya Mheshimiwa Waziri ya kusema maeneo hayo yamevamiwa. Hakuvamia mtu pale. Wanaovamia maeneo ni vyura sio watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wako pale, wamejenga, wana huduma ya maji, umeme, barabara na leo Serikali Kuu inajenga barabara mpya kutokana na watu walivyoboresha maeneo yale. Kwa hiyo, kama kuna mpango Jangwani, kwanza uwajali watu wa pale, wajengewe maeneo mazuri pale pale, halafu ndiyo mtuletee maeneo ya watu kupumzika na mkija na *ice cream* zenu ndiyo mtakula, sisi tutakula ubuyu nyie kuleni *ice cream*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa hawana ndoto ya utajiri, watu hawa hawana ndoto za nyumba, watu hawa ndoto zao ni kusomesha watoto wao, watu hawa ni maskini, hawana mbele hawana nyuma, wako watu wamekaa pale zaidi ya 10,000 na hao ndiyo watu wamekichagua Chama cha Mapinduzi, ndiyo watu wanaompenda Rais, leo Waziri anakwenda, anaibua mpango wa mwaka 1979 anatuletea hapa anasema ndiyo anataka tuufanye? Hiyo sisi hatukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aje akae na sisi, atueleze sisi viongozi, tuelewe mpango huu kwanza kwa kujali wale wanyonge wa maeneo yote ya Jangwani na Mchikichini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena hakuna mtu anayependa watu wale waishi vile, lakini hakuna njia nyingine. Wale watoto wao wote wanasoma mjini, hivi uwatoe pale uwapeleke Maji Matitu, watoto hawa watasoma lini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo hatukubali, mnatakiwa mlielewe hilo. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri angekuja na bajeti yake ashughulikie hati feki, migogoro ya viwanja, rushwa ndani ya Wizara yake, kitu ambacho anashindwa kukisema, matokeo yake mnakwenda kunyanyasa maskini wa Mungu, hawana mbele wala nyuma, hilo muache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hata maeneo yenu Mheshimiwa Waziri na Naibu huko kwenu kuna mabonde vilevile anzeni kule kuweka mahali pa kupumzika sio huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hata bajeti yenyewe hamna, hamna hela za kuendesha Wizara yenu mtakwenda kuboresha nini? Huu mtikisiko wa uchumi duniani kweli mtampata mtu? Mnarusha watu roho, watu wanashindwa kuamka asubuhi sababu ya mambo yenu hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nakuja, katika suala la *National Housing*. Kwanza niwapongeze *National Housing* na Bodi, namjua *Chairman* Mitta na *Director General*, wanafanya kazi nzuri na mpango wao wanaosema ni mzuri wa kuondoa nyumba ndogondogo mijini, kuweka nyumba kubwa, hiyo ndiyo njia ya kuwakomboa watu na hiyo ndiyo *spirit* ya kufanya, lakini lazima kwanza Serikali hii kwenye Bunge lililopita na Mbunge wa Temeke kasema na mimi sasa nanukuu, watu wanasema Wabunge wa CCM hawasomi, hawafuatilii hivi vitabu, si kweli sisi tunasoma zaidi ya hawa wengine. Sasa nitamsomea Mheshimiwa Waziri, hii ni bajeti ya Chiligati ya mwaka jana ukurasa wa 57 kitu ambacho Mheshimiwa Waziri hakusema wala Kamati ya nyumba haikusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema hivi katika ukurasa wa 57, bajeti ya 2010/2011 kwa ruhusa yako, naomba ninukuu:-

"Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti iliyopita, iliyopita hii sasa ya mwaka jana, iliyopita ina maana ya 2009/2010, hii ilikuwa 2010/2011 niliarifu kuhusu azma ya *National Housing* kuuza baadhi ya nyumba zake ambazo gharama za kuziendesha ni kubwa kuliko mapato. Zoezi hili linahitaji maandalizi makubwa, maandalizi hayo yanahusu kuwatambua wapangaji wa nyumba hizo na uwezo wao wa kulipia ununuzi. Kutafuta benki ziwakopeshe fedha za ununuzi, hizo *flats* na pia kuelimisha wahusika taratibu za umilikishaji nyumba hizo chini ya sheria ya umilikishaji wa sehemu ya jengo. Maandalizi haya yakikamilika ndipo zoezi la uuzwaji wa nyumba hizi utaanza kutekelezwa. Napenda kurudia tena kwamba *National Housing* watauza sehemu tu ya nyumba zilizowapa hasara kuziendesha na sio nyumba zote."

Leo amekuja Mheshimiwa Waziri humu ndani hata hii taarifa sidhani kama anayo, watendaji wake wamwambie, wanamwingiza mkenge mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh! Kwa hiyo kama kuna maagizo ya Rais msichambue mkanyofoa maagizo ya Rais, mkaacha maagizo mengine, hili nalo ni agizo la Rais wasaidieni hawa watu waliokaa zaidi ya miaka 40 kwenye nyumba hizi. Kigeugeu kiko wapi? Nyumba za Ilala, Amana, Buguruni, Tandika, Ubungo, hizi nyumba haziwasaidii chochote. *Let the people live and the state will live.*ndiyo eeh! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchechu aendelee kujenga maghorofa mjini ili watu wakae katika nyumba safi na salama, hilo nawapongeza sana *National Housing*, lakini mjenge *affordable houses*, mjenge nyumba ambazo mtu wa kawaida ataweza na yeye kumudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo umetutangazia hapa kuna nyumba, hizo nyumba zitakuwa milioni 100, hivi wale watu hatuzungumzii Dar es Salaam, Mtanzania gani wa sasa hivi ataweza kununua nyumba ya milioni 100? Jengeni nyumba ndogo, nyumba za kawaida ambazo watu wa kawaida na wao waone raha kuishi katika makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya nyumba ambazo tunazo mjini, naomba radhi hata ile raha na tendo na heshima ya ndoa hakuna, hakuna. Mtu anakaa chumba kimoja na mkewe na watoto watatu, hajui cha kufanya, asubuhi akitaka shughuli zingine watoto wameshaamka kwenda shule. Jengeni nyumba ambazo zitawafanya watu wawe na heshima za ndoa zao kwenye nyumba zao nchini mwao kwa gharama ndogo na kwa mkopo wa miaka 20. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za viwanja, kiwanja cha rahisi Ilala milioni nne na laki tano. Hivi *squatters* wataacha kuwepo Dar es Salaam kama viwanja bei zake ni hizi? Lazima viwanja viwe bei ya chini na maeneo maalum ya kuwasaidia watu wa kipato cha chini, kununua viwanja hivyo kwa gharama ndogo na hakuna mtu yeyote mwenye uwezo mkubwa kisheria, anaruhusiwa kuingia kununua viwanja hivyo na yule ndiyo anaruhusiwa kuuza. Lakini leo vikija viwanja vya bei ndogo anataka huko huko, ana viwanja 20 huku, 20 huku, 30 huku. Hii ni roho mbaya, ubinafsi na ni dhambi kubwa sana tunayowafanyia watu wetu na watu wakome kujilimbikizia ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeanzishwa mpango mzuri wa benki ya ardhi, *land bank*, *very nice*. Huwezi ukawa na benki ya ardhi bila kuwa na *Land Ceiling Act*, lazima Mheshimiwa Waziri alete sheria ya kuzuia watu kujichukulia ardhi nyingi bila sababu. *Land Ceiling Act*, lazima Mheshimiwa Waziri ailete ili kuhakikisha kwa Watanzania, hii nchi ni yetu wote. Haiwezekani baadhi ya watu wakawa na maheka mamilioni, wengine hata heka mbili au heka moja hawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala lingine la nini? Leo asubuhi kuna mtu alisimama akawa anazungumza anasema nyumba za *National Housing* uzeni kwa bei ya soko, mimi imenisikitisha sana. Sisi Dar es Salaam hatuna pamba, korosho wala mifugo. Sisi Dar es Salaam siasa ni nyumba. Sasa unaposimama mtu unatetea pamba unaacha kutetea nyumba kwa sababu mnazo pamba, sisi hatuna hela za pamba, tunataka wale wapangaji wauziwe nyumba kwa bei rahisi na nyumba mpya zinazojengwa, zijengwe kwa bei rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la Kigamboni. Serikali mpaka sasa hivi haijaonesha dalili zozote zaidi ya kubana, lini mtaachia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine. Nalisema hili kwa watu wote wanaohusika na Wizara yote husika walielewe. Mpango huu wa Kurasini wa kupanua Bandari, ebu Viongozi wa Serikali rudini mkalitazame upya na mpime haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango wa nchi jirani, wameshaingia mkataba na nchi za Asia kuboresha Bandari yao na Bandari hii ikishaboreshwa unafanywa mpango unaitwa *Transhipment Port*. Bandari hii itazuia meli kuja Dar es Salaam, itakuwa sasa meli zote zinakwenda

kwenye Bandari hiyo na kufanya mizigo ya Tanzania tukaichukue kwenye Bandari hiyo. Ina maana tutakosa biashara za Malawi, Zambia, tutakosa biashara zote za *transit goods* na hivi sasa inaweza ikaonekana mpango wa Kurasini ukafa sababu Serikali itakuwa haina cha kufanya. Sasa naomba Serikali waende wafanye utafiti je, mpango huu upo? Maana yake tayari upo, sisi tunajua upo. Nchi hii ya jirani ina-*lobby* sasa hivi kwa kusema Tanzania meli zinakaa zaidi ya wiki mbili Bandarini. Sio tija kwa meli kukaa kipindi chote hiki, ndiyo maana wanafanya mpango sasa *transhipment* iwe kwenye nchi yao, watunyang'anye biashara yetu sisi na tukiwa hatuna biashara yetu sisi, sidhani kama kutakuwa na mpango mwingine wa kupanua Bandari, itakuwa hakuna haja kabisa. Kwa hiyo, naomba, Waziri uko hapo na viongozi mpo na watu wanaohusika wapo hebu jaribuni kwenda kutizama tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya narudia tena kusema sitaunga mkono mpaka tupate majibu, majibu sahihi ya kutazama hali ya watu. Watu wetu wana imani na Serikali, watu wetu wana shida, mkombozi wao ni Serikali. Wanapokuja watu kutokujali watu wa chini, watu wa kuja kudai maslahi yao, wanateseka, mtu anakuwa mpangaji kwenye nyumba baada ya miezi mitano anasoma ndani mle, anakwenda kubadilisha hati ya mazabe, Wizara hii ni wiki moja, hati ya mazabe ni wiki moja, hati halali miaka minane. Bado Makatibu wapo, bado Makamishna wapo, bado watumishi wapo, kila unayemkuta Wizara hii asubuhi anachokonoa meno. Wanakula dhambi na hili hatutalikubali hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka Waziri ameingia ana uzoefu mkubwa sana upo unapotoka, atumie uzoefu wake aachane kabisa na kanyaboya ambao wako kwenye Wizara yake, wasimpotoshe. Pili narudia, hakuna mtu, hakuna kiongozi anayekataa maendeleo ya kwenye Jimbo lake, lakini maendeleo haya lazima ashirikishe viongozi, washirikishwe wadau waliokutwa, wadau waliokutwa waone *benefit*, waone *fruits* za mradi huu na wao zinawagusa. Sio unamtoa mtu hapa unamwambia nyie mmevamia ondokeni, watu wako pale miaka 50, hakuna aliyevamia, wote ni wakazi halali wa maeneo yale na nawa-*support* kama Mbunge wao. Ikibidi kwenda Mahakamani kama hamkutushika, kwanza nchi hii ina viongozi wanne tu; Mwenyekiti wa Mtaa, Diwani, Mbunge na Rais. Waziri sio Kiongozi, Mkuu wa Mkoa sio kiongozi, ni watendaji wanasikiliza maagizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka hili mlielewe hatutakubali watu hawa kunyanyasika, kuna watu pale zaidi ya 10,000 hivi saa hizi ninavyozungumza, hawajijui wafanye nini, wamepakata watoto wao tena mama maskini, wamebeba watoto wanalia Yarabi Mungu tusaidie mpango huu usiwepo. Kama mpango huu mnao kweli, wajengeeni makazi, wapeni *replacement* najua Mheshimiwa Waziri ametoka *UN Habitat* huruhusiwi kumfukuza mtu mpaka unampa eneo lingine na sio kuwapeleka kwenye hema, mjengeeni pale pale Jangwani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Kengele ya pili Mheshimiwa Azzan. Waheshimiwa Wabunge sasa sijui makofi hayo ni baada ya Mwenyekiti kusimama, kwa maana na yeye yanamhusu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge naomba nikiri kwamba mmejitahidi kuchangia kwa hisia tofauti, kuwawakilisha wananchi wetu wa Tanzania kwa ujumla wetu kwa maana ya mgawanyo wa Majimbo ya kila mmoja anakotoka na matatizo ya ardhi jinsi yalivyojiri katika eneo lake. Nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri amechukua nafasi nzuri ya kusikiliza, basi kesho atakapokuja hapa atakuwa na majibu ya kutosha ili kuweza kutusaidia sisi wawakilishi wa wananchi kwa mujibu wa Katiba, lakini atae maelezo kwa mujibu wa kanuni za Bunge. Muda wetu kwa leo umekwisha, sasa naomba niseme yafuatayo:-

Tangazo nililoletewa na Ofisi ya Bunge nimeshawatangazia, lakini naomba tu niseme Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiwasiliana na wale ambao hawapo. Kwa hiyo, uchangiaji mnaona ile orodha imekwenda katika utaratibu tofauti, lakini ni baada ya kuletewa taarifa rasmi hapa mezani.

Kwa hiyo, kesho mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Wenje, atafuatiwa na Mchungaji Nshama, atafuata Mheshimiwa Mchungaji Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, nilitaka kusema Mchungaji, lakini Susan bado sio Mchungaji, labda yuko njiani kusomea Uchungaji.

Kwa hiyo, baada ya hao niliowataja Makatibu wetu wataendelea kuiweka ile orodha vizuri kama ilivyo na tutaendelea na mjadala huu kesho. Kwa hiyo, baada ya kutoa matangazo haya na maelekezo haya ya Kiti, naomba sasa niahirishe shughuli hizi za Bunge. Waheshimiwa Wabunge, tutakutana tena kesho saa tatu asubuhi, ndani ya Ukumbi huu. Ahsanteni sana.

*(Saa 12.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 16, Agosti, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*